ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
47.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.

48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.

68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Tano – Tarehe 30 Machi, 2010

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani kuhusu Mswada wa Kufuta Sheria ya Uvuvi na Kuweka masharti bora yanayohusiana na usimamizi na maendeleo ya uvuvi ndani ya Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi juu ya Mswada wa Sheria ya Uvuvi na Kuweka masharti bora yanayohusiana na usimamizi wa maendeleo ya uvuvi ndani ya nchi ya Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani juu ya Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Uvuvi na Kuweka masharti bora yanayohusiana na usimamizi na maendeleo ya uvuvi ndani ya Zanzibar. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 86

Upotevu wa Kompyuta Ofisi ya Mrajis wa Serikali

Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi - Aliuliza:-

Mnamo tarehe 19 – 23/06/2008 katika Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali ulitokea upotevu wa kompyuta *(CPU – 3 Monitor 1na mause 1).*

(a) Mhe. Waziri, pamoja na kuwa taarifa hiyo imepelekwa polisi tokea kipindi hicho. Je unafahamu kuwa hakuna taarifa (*feedback*) yoyote iliyopokelewa katika Afisi ya Mrajis kuhusu maendeleo ya upelelezi wa polisi kuhusu upotevu wa kompyuta hizo.?

(b) Wizara yako imefanya juhudi gani kuona upelelezi unakamilika na hatua zinazohusika zinachukuliwa kutegemea na matokeo ya upelelezi?

(c) Kwa kuwa Kompyuta zilizopotea huenda zilikuwa na taarifa muhimu za Afisi ya Mrajis. Je, ni athari kiasi gani iliyopatikana kwa kupoteza taarifa hizo?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 86 lenye (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli mnamo tarehe 19-23/06/2008 kipindi ambacho Zanzibar kulikuwa hakuna umeme kwa takriban mwezi mzima kulitokea wizi wa kompyuta katika Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali. Baada ya kubainika kutokea wizi huo Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali ilichukua hatua ya kutoa taarifa Kituo cha Polisi cha Malindi kwa mdomo pamoja na kumuandikia barua rasmi Mkuu wa Kituo cha Polisi Malindi yenye kumbukumbu Nam. IMS/JFV/3/VOL.II/101 ya tarehe 24/6/2008 kumtaka afanye upelelezi pamoja na kuchukua hatua zinazofaa juu ya suala hilo.

Mhe. Spika, wizara yangu inafahamu kuwa hakuna taarifa (*feedback*) yoyote kutoka Kituo cha Polisi inayohusiana na upelelezi wa upotevu wa kompyuta hizo.

b) Mhe. Spika, wizara yangu imechukua hatua ya kumtuma afisa wake kufuatilia suala hili kwa Mkuu wa Kituo cha Polisi cha Malindi. Mkuu wa Kituo aliitaka wizara kumuandikia barua rasmi kumkumbushia suala hilo. Wizara yangu imefanya jitihada ya kumuandikia barua Mkuu wa Kituo cha Polisi cha Malindi kumkumbushia suala hilo. Kwa sasa wizara yangu inasubiri taarifa hiyo ili kujua hatua za upelelezi zilizofikiwa na polisi, pamoja na hatua zilizopendekezwa katika taarifa hiyo.

c) Mhe. Spika, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali imeathirika kwa kuibiwa kompyuta lakini kiasi cha athari ya kupoteza taarifa zilizokuwa katika komyuta hizo ilikuwa ndogo kutokana kuwa taarifa hizo haziathiri utendaji wa kazi wa afisi kompyuta zilikuwa bado hazijaingizwa taarifa muhimu za Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atueleze kwa kina sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuamini vipi kwamba kompyuta hizo zimeibiwa wakati afisi haikuvunjwa na mlinzi hakukamatwa na kupigwa. Mhe. Spika, asubuhi baada ya kwishatokea tukioa hili afisi ilikuwa imefungwa kama kawaida na hakuna kilichovunjwa lakini kompyuta zimeibiwa. Ni mazingira gani kompyuta hizo zimeibiwa?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, ni kweli wizi huu unatatanisha na umetokea katika mazingira ambayo ilibidi polisi wafanye upelelezi wa kina, na ni kweli palikuwa hapakuvunjwa na kompyuta ndani hazimo. Hilo ni kweli kabisa lakini polisi ndio bado hawajatukamilishia suala hilo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba kompyuta hizo zimechukuliwa na wala hazikuibiwa kwa sababu katika kompyuta hizo tatu zimechukuliwa kwa siku tofauti, leo imechukuliwa moja, kesho ikachukuliwa nyengine na kesho kutwa ikachukuliwa nyengine. Mhe. Spika, kwa mazingira hayo inaonesha dhahiri kwamba kompyuta hizi hazikuibiwa isipokuwa zimechukuliwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, maneno anayoyasema ni ya kweli lakini tuliitegemea polisi kufanya upelelezi juu ya suala hilo. Ingeweza kuwachukua wafanyakazi katika sehemu zile na ikawahoji, lakini hawakuifanya kazi hiyo. Mhe. Spika, ni jambo la kusikitisha sana na nadhani sasa hivi ipo haja katika afisi zetu kuimarisha ulinzi wa kutumia *machine* za kisasa za *CCTV* ambazo zinarikodi kila kinachotokea ndani ya ile afisi. Hii ndio peke yake itasaidia kukamata watu wabadhirifu wa namna kama hii katika afisi zetu. Mhe. Spika, bahati mbaya hatujaweza kufanya kitu kama hicho.

Mhe. Omar Ali Jadi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii kuuliza swali moja kwa Mhe. Waziri. Mhe. Spika, Mhe. Waziri kwa sababu amekiri kama zimeibiwa kompyuta kwa mazingira ya kutatanisha. Ni hatua gani kwa wale waliokuwepo pale kazini iliyochukuliwa?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, ni kwamba wafanyakazi walioko pale ilibidi wachukuliwe hatua lakini baada ya kupata tetesi kutoka polisi, polisi wametuangusha juu ya suala hili mpaka sasa hivi. Lakini sisi bado tunakwenda nao ili watupe angalau tetesi nani ameondoka na kompyuta zetu, bado hawajatujibu wanatwambia subiri na huku siku zinakwenda.

Nam. 2

Usafishaji wa Mitaro

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza**:-**

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa nia njema imejenga mitaro ya maji ya mvua na maji machafu katika maeneo mbali mbali katika Manispaa ya Zanzibar chini ya usimamizi wa wataaalamu wa manispaa hiyo.

(a) Mhe. Waziri, kwa nini mitaro hii mingi haifanyiwi usafi?

(b) Mtaro unaotoka Kwahani Uwanja wa Farasi unaopitia Kiwanja cha Kufurahishia Watoto Kariakoo kuelekea Kilimani hadi pwani ni mbovu. Je Mhe. Waziri jambo hilo watendaji wa Manispaa wanalielewa na kama wanalielewa wamechukua hatua gani kuufanyia matengenezo?

Mhe.Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 2 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, mitaro ya mvua yote mipya na iliokuwapo kabla inaendelea kufanyiwa usafi kama kawaida kwa mujibu wa idadi ya wafanyakazi waliokuwepo. Hata hivyo, lipo tatizo kubwa la baadhi ya wananchi wenye tabia ya kutupa taka ovyo hasa wakati wa mvua. Napenda kuchukua fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge, Masheha na Madiwani pamoja na viongozi wa vyama vya siasa tushirikiane kuwaelimisha wananchi wetu juu ya ubaya wa kutupa taka ovyo katika mitaro.

b) Mhe. Spika, mtaro unaotoka Kwahani kupitia Kariakoo kuelekea Kilimani hadi pwani sio mbovu kama anavyodai Mhe. Mwakilishi. Mtaro huo ni mzima na unapitisha maji wakati wa mvua kama kawaida. Tatizo kubwa ni lile lile la wananchi kutupa taka katika mtaro jambo ambalo husababisha mtaro huo kuziba na kujitokeza kasoro ndogo ndogo ambazo zimefayiwa marekebisho na mkandarasi.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mimi bado

naipongeza serikali kupitia Wizara ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ kwa kuhakikisha kwamba kero ambazo zimejitokeza huko nyuma zinapatiwa ufumbuzi katika ujenzi mzuri wa mitaro yetu ambao kwa asilimia kubwa wananchi wetu wanaishi katika hali ya amani katika maeneo mbali mbali.

a) Mhe. Spika, namuuliza Mhe. Waziri kwamba kuna mtaro ambao umetoka Miembeni Branch hadi Jasmine Hotel mtaro huo umejengwa lakini umezibwa haukufikia mwisho. Hili mheshimiwa analielewa na husababisha maji yale kutuama yakaingia katika baadhi ya maeneo?

b) Katika mtaro uliotoka Kwahani Uwanja wa Farasi hadi kupitia Kariakoo mpaka kuelekea Kilimani hadi Kizingo atakubaliana na mimi kwamba katika eneo hilo la Kizingo mtaro wake sasa hivi umevunjika na unaendelea kuvunjika mvua zinapozidi. Je, ana utaratibu gani wa kufuatilia na kulijua suala hilo?

Mhe.Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Spika, mtaro wa Miembeni Branch unaangukia barabara ambao unatokea Kilimani kwendea Rahaleo huu uko kama ulivyotengenezwa kasoro ndogo ndogo ziko katika mtaro ambao umetokea Kwahani Uwanja wa Farasi, Kariakoo, Kilimani Mafunzo, Kilimani Maisara mpaka tunafika baharini kumwaga uchafu. Mhe. Spika, taarifa hiyo ipo kuhusu matengenezo hayo na hatua zinazofaa zinachukuliwa. Lakini kwa hii mitaro mengine ambayo inatokea Miembeni maji yake inatoa kama kawaida.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swai moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika majibu yake mama alisema kwamba wananchi wanatupa taka ovyo ndio sababu ya mitaro kuziba na bahati nzuri anasema kwamba mitaro yote ni mizima na inasafishwa lakini bado ina taka.

a) Haoni kwamba kule kukusanya pesa kwa wananchi kila mwezi au wengine kila siku ndiko kunakosababisha kuona tayari wameshailipia kazi hiyo ifanywe na watu wake hawaifanyi?

b) Ili sasa kuufanya mji wetu uwe safi katika maeneo yote haoni kama hayo mapato ambayo yanakusanywa yasiyofanya kazi sasa yaondoke ili wananchi wawe na majukumu yao binafsi moja kwa moja?

Mhe.Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Spika, ukweli kukusanya taka ambazo zilizozolewa na zikatupwa katika

mitaro hiyo naendelea kusema kwamba ndio moja ya sababu kubwa sana ya kukwama kwa maji, hilo bado kwa utafiti wetu ni kosa kubwa sana. Mhe. Spika, mvua zinazokuja na taka zinazotupwa utaona kwamba hali iko hivyo na kwa juhudi kubwa ambayo imechukuliwa kupanuliwa baadhi ya milango ili kuzidisha uendeshaji kwa kasi maji na kuingia baharini. Kwa hivyo, suala la urekebishaji wa maeneo hayo ya Maisara na Kilimani juu hali inakwenda vizuri na kama tutashirikiana sote kwa pamoja kuhusiana na mitaro hiyo ya kutotupa taka basi hasara au mafanikio makubwa yatakuwa yamepatikana kutokana hilo.

Mhe. Spika, kuhusiana na mapato ni kwamba kila sehemu kuna mapato huwezi ukayachanganya mapato yote yakawa ndio sababu ya maji kukwama kwenda baharini. Mhe. Spika, kila taasisi inalipa kodi kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizowekwa katika nchi.

Nam. 48

Athari za Uharibifu wa Mazingira

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Wanasayansi duniani wamekuwa wakipiga kelele kuwa tabaka la hewa *(Ozone Layer)* liko hatarini kutokana na uharibifu wa Mazingira. Kuharibika kwa tabaka hilo kunasababisha kuongezeka kwa hali ya joto duniani, na miongoni mwa athari za ongezeko hilo la joto ni kuongezeka kwa kiwango cha kujaa maji ya bahari na kuathiri maeneo ya nchi, hasa visiwa.

(a) Je, Mhe. Waziri, Tabaka la *Ozone* limeathirika kwa kwa kiwango gani hadi sasa?

(b) Kwa kuwa baadhi ya visiwa vidogo vidogo kama vile Maziwa Tanzania vimekwisha kuzama baharini. Je, ardhi ya Zanzibar imeathirika kwa kiasi gani hadi sasa?

(c) Je, serikali imefanya tathmini ya kimazingira *(Environmental Impact Assessment)* ili kugundua ukubwa wa tatizo la uharibifu wa ardhi ya Zanzibar unaotokana na uharibifu huo wa mazingira?

(d) Katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu kama vile eneo la Mwambe, Serikali, Makampuni na watu binafsi wanaendelea kuharibu mazingira na kusababaisha bahari kupanda juu kutokana na uchimbaji wa mawe na vifusi. Je, Serikali sasa ina mpango gani kunusuru hali hiyo?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 48 lenye kifungu (a), (b), (c) na (d). Kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, kutoboka kwa tabaka la *Ozone* kunasababishwa kwa kiasi kukibwa na kuvuja kwa hewa zenye asilia ya "*Organic*" kama vile *Chloro – flouro – Carbon (CFC)* ambazo hutumika katika viyoyozi, vipoza joto pamoja na mitambo ya kufukizia madawa (*Fumigants*).

Matokeo yake hewa hizo huiharibu hewa *Ozone* ambayo iko kiasi cha masafa ya mita 500 kutoka usawa na dunia na kuifanya mionzi ya jua *(Ultra violeng rays*) kupenya duniani na hiyo kupelekea matatizo mbali mbali ya kiafya kama vile kensa ya ngozi, matatizo ya macho pamoja na watoto kuzaliwa na matatizo. Hivyo, mabadiliko ya hali ya hewa hayana mahusiano ya moja kwa moja na kutoboka kwa tabaka la *Ozone*.

Baada ya kutoa maelezo hayo, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Tabaka la *Ozone* limeathirika kwa kiwango kati ya asilimia 5–15. Hata hivyo, kuna taarifa ya kisayansi zinaonyesha kuhusika kwa tabaka hilo kutokana na juhudi zinazochukuliwa za kimataifa na kitaifa za kuacha kutumia hewa hizo.

(b) Mhe. Spika, Zanzibar tayari imeshaanza kuathirika na kupanda kwa kina cha maji ya bahari. Dalili zake ni pamoja na mmong'onyoko wa fukwe katika maeneo mbali mbali ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Yakiwemo ya Nungwi, Uroa, Jambiani, Michamvi na Maruhubi kwa Unguja na Kisiwa Panza, Wambaa na Mwambe kwa Pemba. Aidha, maeneo mbali mbali yaliyokuwa yakitumiwa kwa shughuli za kilimo hivi sasa hayatumiki tena kwa sababu ya kuingiliwa na maji ya bahari.

(c) Mhe. Spika, serikali imefanya tathmini ya mwanzo na hasa katika maeneo yaliyoathirika zaidi ambayo ni Nungwi, Kilimani na Jambiani kwa Unguja na Kisiwa Panza na Muwambe kwa Pemba. Aidha, wizara imetayarisha mpango wa kufanya tathmini ya maeneo yote ya ukanda wa pwani kuona ukubwa wa athari ulivyo na baadae kuweka mikakati ya kukabiliana na athari hizo.

(d) Mhe. Spika, kwa kawaida serikali hairuhusu uchimbaji mchanga katika maeneo yote mbali na yale yaliyotengwa na kutangazwa maalum kwa shughuli za uchimbaji na uchukuaji wa mchanga. Mhe. Spika, wizara kupitia Idara yake ya Mazingira imo mbioni kuendelea na juhudi zake za kuelimisha na kutoa mafunzo juu ya athari za uharibifu wa mazingira. Hivyo tunaomba Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Masheha na viongozi wote wa chama na serikali kushirikiana na wizara yetu katika kupiga vita athari zinazofanywa na wenzetu katika maeneo ambayo uharibu umekithiri.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, naomba nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana na yakitaalamu ambayo yanatuelimisha athari za mazingira zilizokuwepo hivi sasa.

Mhe. Spika, hivi karibuni kulifanyika mkutano wa mazingira nchini Denmark na katika mkutano huo ilizungumzwa athari kupanda maji ya bahari wanasema karibu wastani wa mita 1.2 kwa mwaka. Sasa katika mazungumzo yaliyoendelea huko Kisiwa cha Unguja nacho kilizungumziwa na wataalamu walisema kutokana na kupanda kina cha maji na visiwa ambavyo tayari vimeshapotea wanasema Kisiwa cha Zanzibar baada ya miaka 25 kitakatika pande mbili. Yaani bahari ya kutoka huku Chwaka Bay na upande wa pili zitakutana na tutakuwa na visiwa viwili katika kisiwa kimoja cha Unguja. Kwa hivyo, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri je, hili ni kweli na baada ya miaka 25 tunatarajia mambo hayo yatatokea?

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kwa bahati nzuri mimi nimehudhuria mkutano huo na kabla ya mkutano huo kulikuwa na mkutano mwengine Geneva kuhusu masuala hayo ya kupanda kwa joto duniani. Mhe. Spika, kwa ujumla lililozungumzwa pale ni kwamba joto linaendelea duniani na matokeo yake barafu inamong'onyoka kwa wingi sana na matokeo yake inasababisha mafuriko katika nchi mbali mbali na kujaa kwa bahari na upo uwezekano baadhi ya visiwa kuweza kupotea. Lakini sikumbuki kama imesemwa *specific* kwamba Kisiwa cha Unguja kitakatika, hilo sikumbuki lakini napenda kumuhakikishia kwamba ni kweli kuwa baadhi ya visiwa vitaathirika na vimetajwa baadhi ya visiwa vyengine.

Nakubali kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba Zanzibar mmong'onyoko upo na haukuanza jana usipokuwa unaendelea tu na kama ilivyozungumzwa kwamba wizara kupitia idara yetu inafanya utafiti na imeshamaliza utafiti wa kwanza na kugundua kwamba sehemu nyingi sana mmong'onyoko upo na unaendelea. Pia wizara yangu imechukua hatua ya kuishauri serikali na serikali imeliona suala hilo na kusema kwamba basi

tutayarishe ripoti ya kina ili tuipeleke serikalini kutazamwa yakuweza kuhifadhi suala hilo. Hilo limo katika kuyarishwa na serikali yenyewe ima itashirikiana na nchi rafiki na wahisani kuweza kupata fedha kuweza kukabiliana na hali hiyo.

Mhe. Spika, mkutano ule kwa kweli mataifa yote yalihudhuria tangu mataifa makubwa mpaka madogo na mada kubwa ilikuwa ni hiyo kwamba hali mbaya na wamekuja watu wa sayansi pale wanaohusika na mambo hayo na wakatoa hadhari kwamba lazima nchi husika hasa imetajwa Marekani na China ndio mwanzo lakini nyengine zinafuatilia lazima wapunguze kutumia gesi joto kwa kiasi fulani. Pale wao wameji-*commite* kwamba wataanza kuondoa kwa awamu. Mhe. Spika, mkutano mwengine unaofuata utafanyika Mexico mwaka huu hapo watasema hasa kwamba sisi wataweza kupunguza kwa kiasi fulani ambacho kitasaidia usumbufu wa kupanda kwa joto la dunia.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba maeneo ya Uroa na Mwambe bahari inapanda juu kwa kasi.

a) Naomba kujua ni lini atafanya ziara ya makusudi kwenda kuona hali hiyo pamoja na wawakilishi wa maeneo hayo?

b) Mwaka 1990 serikali walikuwa na mradi uliojenga gati ya Mkoani kifusi na mawe kilikuwa kinatoka Mwambwe, mwaka 2007 ni ujenzi wa barabara Mkoani-Makombeni kifusi kimetoka Mwambe na hivi sasa tuna ujenzi wa barabara sita za Kusini Pemba kifusi kinatoka Mwambe na kila mradi ukija basi mashimo ya vifusi hubakishwa Mwambe na kuchukuliwa nafasi hiyo na bahari. Kwa sasa kwa sababu kuna barabara sita zinajengwa na kifusi chote kinatoka Mwambe ni lini hatua ya serikali ya kuhakikisha kwamba bahari wanaidhibiti ili isipande juu.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kuhusu ziara napenda kumuhakikishia kwamba ziara zimefanywa Unguja na Pemba na sehemu zote zilizokuwa zinamong'onyoka nazijua. Kwa hivyo, kama nilivyosema kwamba hatua ya wizara yangu imo katika kutekeleza ikishirikiana na Idara yake ya Mazingira kuweza kumaliza hii ripoti na kuipeleka serikalini kuweza kutafuta *funds* ya kuweza kukabiliana na hali hiyo.

Mhe. Spika, suala la uchimbaji wa vifusi hivi karibuni mimi nilikwenda Pemba na nilipelekwa kuna sehemu kule kwa kweli jografia ya pale ilinishinda lakini nimekwenda nimeona kweli kuna uharibifu mkubwa sana wa mazingira kwani mashimo ni makubwa sana.

Sasa nilichofanya pale nimeagizia kwamba Pemba kule washirikiane baina ya Afisa Mdhamini wangu na Idara ya Mawasiliano na mimi mwenyewe tunakutana na Mhe. Waziri mwenzangu wa Mawasiliano na Uchukuzi kuweza kuikabili na vipi tutafanya ku-*arrest* hali halisi endelevu. Lakini kwa kweli nakubaliana kwamba hali ni mbaya sana.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa ndani imelaumiwa sana juu ya ujengaji wa barabara na kutumia malighafi ya jiwe kutoka Mwambe, lakini ninavyoamini kwamba Wizara hii ya Mawasiliano ni hodari sana ya kufanya utafiti kabla ya kufanya shughuli zake.

Je, kwa eneo hilo la Mwambe hivyo wizara haikufanya utafiti ili kuondokana na mjumbe kwamba anailalamikia sana Wizara yake ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwa kawaida sehemu zote ambazo tunajenga barabara na kuchimba kifusi, hatuanzi kuchimba kifusi mpaka tuwasiliane na watu wa mazingira ambao wako chini ya Wizara ya Kilimo. Kwa hivyo, tunaruhusiwa rasmi na serikali kuchimba kifusi. Tatizo unaloliona kwa Pemba ni ukataji wa matofali ardhini, ni eneo kubwa la ukanda wa Kusini Pemba kuanzia Vitongoji, Mwambe mpaka jimboni kwa Mhe. Hamad Masoud wamekata sana ardhi.

Sasa nafikiri hili Wizara ya Kilimo kama Mhe. Waziri alivyolizungumza, watalifanyia kazi lakini sisi mawasiliano tunachimba baada ya kuruhusiwa na kawaida yetu tukichimba halafu huwa tunasawazisha. Tatizo la Mwambe Mhe. Hija Hassan Hija hajalisema vizuri, kuna mtu nafikiri ndio kamtuma huyo, ana madai ya muda mrefu kwamba ni eneo lake, lakini kenda Mahkamani kashindwa, kenda Wizara ya Ardhi kashindwa, sasa nafikiri ndio katumia njia nyengie ya kufikisha ujumbe. Lakini hilo ndilo tatizo kubwa la Mwambe.

Nam. 63

Kurejeshewa Gharama za Ujenzi wa Banda la Madarasa Nungwi

Mhe. Ali Abdalla Ali (Kny. Mhe. Ame Ussi Juma) - Aliuliza:-

Katika kupunguza tatizo la uhaba wa madarasa Wananchi wa Nungwi wamefikia hatua ya kukopa fedha ili wakamilishe ujenzi wa banda la madarasa ili kuharakisha ujenzi wa madarasa na kuwawezesha watoto wao kupata pahala pa kusomea.

(a) Je, Mhe. Waziri unalijua suala hili.

(b) Kama unalijua ni hatua zipi wizara yako itachukua kurudisha gharama ambazo wametumia wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 63 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, wizara yangu haina taarifa ya kwamba wananchi wa Nungwi wamekopa fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la madarasa. Wizara inaelewa kuwa wananchi wakishirikana na uongozi wa skuli wameamua kuezeka madarasa waliyoanzisha kwa nia ya kuwapatia wanafunzi nafasi za kusomea. Mhe. Spika, wizara inawapongeza sana kwa mwamko wao wa kuamua kuendeleza ujenzi huo.

b) Kama nilivyotangulia kujibu kuwa wizara haijapokea taarifa kuwa wananchi wameendeleza ujenzi huo kwa kutumia fedha za mkopo. Hivyo, wizara yangu haina mpango wa kurejesha gharama zilizokwisha kutumika.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba hivi sasa maeneo mengi ya skuli huwa tunajenga mabanda, na hii inasababishwa na kwamba hivi sasa nchi yetu ina ongezeko kubwa la uhamiaji pamoja na uzazi.

Mimi katika jimbo langu nina skuli zangu sita na zote zina mabanda bado hayajaezekwa vyumba vinne, vinne. Je, hilo analijua. Kama analijua atanipa msaada gani ili tatizo hilo limalize.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nakubaliana naye kwamba hivi sasa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba vina ongezeko kubwa la watu ambalo linatokana na uzazi au uhamiaji. Jambo hili ndilo linalopelekea kuwa na wanafunzi wengi katika skuli zetu, lakini pia kuwa na harakati kubwa za ujenzi katika skuli zetu ambapo inatokana na mwamko wa wananchi.

Mhe. Spika, naelewa kwamba kuna ongezeko kubwa la ujenzi wa madarasa katika jimbo lake lakini sio katika jimbo lake tu, hata katika majimbo mengine yakiwemo na Jimbo la Mtoni.

Mhe. Spika, napenda kumueleza Mhe. Mwakilishi kwamba tunachukua jitihada ya kuweza kuhakikisha kuwa madarasa haya yanamalizika kadiri inavyowezekana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali naomba kuuliza swali la nyongeza. mimi kwanza naipongeza Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri ambazo kupitia Mhe. Waziri na watendaji wake wanajitahidi, kuhakikisha kwamba watoto wetu wanapata elimu kila panapohitajika. Lakini pia nampongeza Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kuhamasisha kamati za skuli kusimamia vyema ujenzi na mambo mengine ya maendeleo kwa ajili ya wanafunzi wetu.

Lakini kwa swali lililoulizwa hapa Mhe. Spika, nataka niombe tu kwamba. Je, kwa kuwa kamati ina hamu ya kufanya jambo la maendeleo kwa njia yoyote ikiwa kwa mkopo au kwa njia wanazozijua wenyewe wananchi, na tendo lile wanalolifanya likawa zuri limefanikisha watoto kupata elimu. Je, Mhe. Waziri ana mpango gani labda wa kuwaonea huruma katika huo mkopo waliokopa ili wakazipata zile pesa zikarudishwa na kuweza kufanyiwa mengine ya baadae ya kuleta maendeleo katika skuli hiyo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kabla ya hapo naomba nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wangu kwa kweli amejibu vizuri sana isipokuwa mimi naongeza hili ambalo Mhe. Ali Suleiman na yeye kaongeza.

Mhe. Spika, taratibu kama hizi kiserikali inabidi kabla hujafanya kwanza uje utoe taarifa uombe, kama kuna dharura ya kwamba basi fanyeni, itakuwa ni kibali hicho au ruhusa hiyo imetoka serikalini. Tatizo linalotukabili sasa hivi endapo tukisema kwamba tutalipa mfano, kwa sababu hivi sasa wananchi katika majimbo yote 50 Unguja na Pemba wanafanya kazi wanatafuta pesa wao wenyewe na njia mbali mbali ili kujenga madarasa na sisi huwa tunakwenda kukamilisha.

Sasa katika ile hatua ambayo pengine Mheshimiwa amekamilisha lakini hakuezeka, ingekuwa vizuri kabla hajafika hatua ile ya kuezeka basi atuletee taarifa ili tufuate taratibu zote zinazohusika za kisheria na kiserikali ili tufanye malipo.

Hata hivyo, Mhe. Spika, bado tunaweza tukalifikiria suala hilo katika njia za kibinadamu kama kweli kulikuwa na matumizi yametumika na vielelezo vipo basi tunaweza tukalifikiria.

Nam. 18

Wilaya Zenye Watoto Wanaozaliwa na Pepopunda

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Katika Tafiti mbali mbali zilizofanywa na Wizara ya Afya Tanzania imebaini kuwa Wilaya 16 za Tanzania ikiwemo Wilaya 3 za Zanzibar yaani Wete, Mkoani na Micheweni baadhi ya watoto wanaozaliwa huwa na maradhi ya Pepo punda "*tetnus*".

(a) Je, Mhe. Waziri, wizara yako inazo taarifa za utafiti huu.

(b) Je, matokeo ya utafiti huo yana ukweli gani kulingana na data ambazo Wizara yako inazo.

(c) Je, wizara ina mkakati gani wa kuliondoa tatizo hilo ili lisienee maeneo mengine ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 18 lenye vifungu a, b na c kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wizara yangu inazo taarifa juu ya tafiti mbali mbali za maradhi ya pepopunda kwa kuwa zilijumuisha wataalamu kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Zanzibar, Tanzania Bara na wale kutoka Mashirika ya Kimataifa (*UNICEF* na *WHO*). Tafiti zilizofanyika ni kama zifuatazo.

1· Mnamo mwaka 2000, kulifanyika utafiti dhidi ya maradhi ya pepopunda visiwani Zanzibar ambapo Wilaya za Wete na Micheweni ziligundulika kuwa hazikufikia vigezo vya kutangazwa kuwa zimefikia lengo la kupunguza ugonjwa wa pepopunda.

2· Yaliyogundulika katika utafiti huo ni pamoja na :-

· Kiwango kidogo cha chanjo ya pepopunda kwa kinamama (chini ya asilimia 80)

· Kiwango kikubwa cha kinamama wanajifungulia majumbani. Kuna zaidi ya mgonjwa mmoja wa pepopunda ya watoto wachanga kwa kila vizazi hai 1000.

3· Kufuatia utafiti huo, wizara yangu ilishauriwa kufanya kampeni ya chanjo ya pepopunda mwaka 2001 na kampeni hio ilifanyika katika wilaya hizo mbili kuanzia Disemba, 2001 na kumalizikia Julai 2002.

4. Utafiti mwengine ulifanyika mwaka 2008 na matokeo yameonesha kuwa Wilaya 19 za Tanzania zikiwemo 3 za Zanzibar (Mkoani, Chake Chake na Micheweni) na sio Wilaya ya Wete kama ilivyoulizwa kwenye swali, bado hazijafikia vigezo vya kupunguza ugonjwa wa pepopunda.

a) Matokeo ya tathmini hizi yameonesha ukweli wa hali ya ugonjwa huu kwa hapa Zanzibar, kwani vigezo nilivyoeleza hapo awali vipo chini sana katika Wilaya ya Mkoani, Chake chake na Micheweni. Kiwango cha chanjo ya pepopunda kwa kina mama wenye uwezo wa kuzaa kiko chini. Mkoani asilimia 45, Chake Chake asilimia 60 na Micheweni asilimia 47.

b) Bado kiwango cha kinamama wanaojifungulia hospital kiko chini sana katika wilaya hizi. Mfano mwaka 2007 Mkoani ilikuwa 46.1% Chake-Chake 74.5 na Micheweni 17.4%. Hivyo, takwimu hizi pamoja na vigezo vyengine vya kitaalamu vinathibitisha uhakika wa taarifa za tathmini hizo.

Mhe. Spika, wizara yangu imo katika kutekeleza mikakati ya kupambana na ugonjwa huu wa pepopunda ambayo ni pamoja na:-

- Kuendelea kuwachanja mama wajawazito wote dhidi ya pepopunda. (Lengo ni kufikia asilimia zaidi ya 80 katika wilaya hizi).

- Tunaendelea kutoa chanjo ya pepopunda kwa akina mama wote wenye umri wa kuweza kuzaa kati ya miaka 15 – 49, ikiwa ni pamoja na kuchanja maskuli. Lengo ni kufikia zaidi ya asilimia 80.

- Wizara imeweka mikakati ya kuelimisha kinamama wote wajifungulie hospitalini. Eelimu ya afya inatolewa katika kliniki za huduma za mama na watoto (*RCH clinic*).

- Wizara yangu inaendelea na ufuatiliaji wa karibu wa ugonjwa wa pepopunda kwa watoto wachanga.

- Wizara pia imeanza mkakati wa kufanya uchunguzi wa vifo vyote vya watoto wachanga ili kugundua kama walikufa kwa sababu ya ugonjwa wa pepopunda.

Aidha Wizara ya Afya na Usatwi wa Jamii Zanzibar kwa kushirikiana na Washirika wengine wa Maendeleo (*UNICEF*) iliandaa kampeni ya chanjo dhidi ya ugonjwa wa pepopunda katika Wilaya za Mkoani, Chake Chake na Micheweni, ambayo itafanyika kwa awamu 3. (Awamu ya kwanza ilifanyika tarehe 5-7 Disemba 2009, awamu ya pili ilifanyika tarehe 23-25 Januari 2010 na awamu ya tatu itafanyika Julai 2010.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Tumeambiwa kwamba Wilaya ya Mkoani, Chake Chake na Micheweni katika utafiti uliofanywa ni wilaya ambazo zinaongoza kwa kinamama wanaoweza kuzaa kuwa hawajapata ile chanjo ya pepopunda na hawazalii hospitali kama inavyotakiwa.

Je, kuna utafiti wowote uliofanywa kuona kwamba akinamama katika wilaya hizi kniniwanapenda kuzalia majumbani.

Vile vile ile elimu inayotolewa pale katika klinii, inawafikia wale wanaofika kliniki tu. Je, kuna njia yoyote inayofanywa na Wizara ya Afya kuwafikia akinamama vijijini wale ambao hawafiki hospitali na wakapata ile elimu nao na wakaona umuhimu wa kufika hospitali.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, unajua utaratibu wa kuzalia majumbani hili suala lilikuwa limezoeleka sana huko nyuma. Baada ya sasa hivi kutolewa taaluma kwenye kliniki na timu zetu kupita kutoa taaluma kwenye vijiji hili kidogo linasaidia. Na sisi viongozi pia tunasaidia, tunapokaa na akinamama hao kuwaeleza katika athari zinazowapata mama kuzalia majumbani. Jitihada pia pengine hivi sasa inayofanywa kufikisha hii huduma katika sehemu ambazo ilikuwa huduma hii haifiki.

Kwa hivyo, hayo ndio masuala ambayo yalikuwa yakichangia mwanzo kuwa kinamama walikuwa wakizalia majumbani. Lakini sasa hivi tunashukuru kinamama wengi wanapata taaluma na wanazalia katika hospitali.

Mhe. Spika, Mhe. Najma Khalfan alitaka kujua kuwa wale waliokuwa hawafiki katika kliniki je, taaluma hii wanaipataje. Ni vile vile nilivyosema kuwa tunafanya ule utaratibu wa kutembelea kwenye vijiji kupita kutoa elimu. Huo ndio utaratibu tunaotumia wizara yetu na hili linatusaidia Mwenyezi Mungu anatujaalia tunafanikiwa. Ahsante.

Nam. 20

Wagonjwa Wanaosubiri Huduma ya Uchunguzi

Mhe. Ali Denge Makame - Aliuliza:-

Serikali imejitahidi kupata vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa wagonjwa vikiwemo Mashine za *X-Ray, Ultra - Sound*, na *CT Scan*. Lakini kuna tatizo la mlundikano wa wagonjwa wanaosubiri kupata huduma ya vifaa hivyo.

(a) Je, Mhe. Waziri, nini tatizo la msingi linalosababisha mlundikano huo.

(b) Kama tatizo ni wataalamu je, kuna mpango gani madhubuti wa kupata wataalam hao.

Ahsante Mhe. Spika, kwa kuwa swali hili jana liliwahi kujibiwa katika kipengele hiki cha *Ultra sound*, kwa faida ya wananchi ambao wale waliokuwa hawakusikia jana wakiwemo katika shughuli zao mbali mbali za kilimo na makazi, na kwa kuwa kitengo hiki ni muhimu sana kwa wagonjwa na wananchi ili wapate kufahamu zaidi basi ningeomba swali hili lijibiwe tena kwa faida ya wananchi waliokuwa hawakusikia.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 20 kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mhe. Spika nakubaliana na Mhe. Mjumbe kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imejitahidi kupata vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa wagonjwa kama, mashine za *X-ray, Ultra sound* na *CT Scan*.

Mhe. Spika kuimarika kwa huduma za uchunguzi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja zikiwemo huduma za *X-ray* na *Ultra Sound* pamoja na kuanzishwa kwa huduma ya *CT Scan*, kumewafanya wananchi wengi kufika hospitalini hapo kwa ajili ya kufaidika na huduma hizo muhimu na za kisasa.

Aidha, katika kwenda sambamba na ongezeko hilo la wananchi wanaohitaji huduma hizo za uchunguzi wa *X-ray, Ultra Sound* na *CT Scan*, wizara yangu inaendelea na mikakati yake ya kuwasomesha wafanyakazi zaidi katika fani hiyo ambapo tayari mfanyakazi mmoja yupo nchini Kenya akimaliza masomo yake ya shahada ya juu katika fani hizo za mionzi.

Nam. 43

Vipindi vya Televisheni vya Mahojiano

Mhe. Hija Hassan Hija (Kny. Mhe. Abass Juma Muhunzi) - Aliuliza:-

Vipindi vya Televisheni vinavyokutanisha watafiti, wanataaluma na wachambuzi wa masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii vinavyoendeshwa kupitia Televisheni mbali mbali za Tanzania Bara kama vile vipindi vya *Redet*, Jenerali Ulimwengu na *Kasongo Hour*, vinawavutia sana watazamaji wa Televisheni hizo.

(a) Je, Mhe. Waziri, ni kwa kiasi gani Wizara yako (ambayo inasimamia vyombo vya Habari) inaweka vipindi vya aina hiyo katika mipango yake ya kazi.

(b) Je, kuna malipo yoyote yanayotozwa kwa vipindi kama hivyo kuwa hewani, kwa taasisi zinayotayarisha vipindi hivyo ambavyo vinaelimisha jamii yetu kwa kuishirikisha.

(c) Ili vipindi hivyo viwe hewani, Je, ni wajibu wa Wizara ya Habari kuwaalika waendeshaji wa vipindi hivyo au ni jukumu la taasisi inayotayarisha kuomba nafasi ya kurushwa vipindi hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 43 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Idara yetu ya Televisheni haina mpango wowote wa kuweka vipindi alivyotaja Mheshimiwa katika mipango yake, au kukopia vipindi kutoka televisheni nyengine, kwani hiyo ni kinyume cha sera ya chombo cha habari (*broadcasting Internal Policy*). *TVZ* hivi sasa inaandaa vipindi vyake yenyewe kama vile Ongea na TVZ siku ya Jumamosi, kipindi cha Murika siku ya Jumatano na siku ya Alkhamis kuna kipindi ambacho *TVZ* hushirikiana na *TBC* kurusha kipindi cha “Tuambie”.

(b) Mhe. Spika, malipo kwa vipindi vinavyotayarishwa na kituo chengine cha TV hutegemea makubaliano yaliyokuweko baina ya kituo hicho na *TVZ*. Kwa mfano, kipindi cha “Tuambie” cha *TBC* huwa kinarushwa bure kwa vile tuna makubaliano maalum na ndugu zetu wa *TBC*, makubaliano ya mashirikiano kwamba nao pia watarusha

vipindi kutoka *TVZ*. Makubaliano hayo mara nyingi kitaaluma hujulikana kama, *Internal Broadcasting by Lateral Agreements* ambapo huwa tunasaini pamoja nao. Kwa hivyo, *TVZ* hapa Mhe. Spika, imesaini mkataba wa kushirikiana pamoja na ndugu zetu wa *TBC*.

(c) Utafutaji wa vipndi ni jukumu la kituo cha Televisheni chenyewe na wahariri na wanahabari wake. Kituo kinafanya makubaliano na mashirika yanayouza vipindi kwa mikataba maalum na malipo yanapofanywa kituo kinapewa hakimiliki ya kurusha kipindi husika. Pia vituo vya TV vinaweza kuwa na makubaliano ya kubadilishwa vipindi kama vile ambavyo *TVZ* inafanya na *TBC*, katika mashirikiano ya kitaasisi.

Aidha, *TBC* inainapoomba pia nayo kurushiwa kipindi chake inalazimika kulipa gharama za urushaji, (*air time*). Na kama *TV station* itataka irushe kipindi ambacho sio chake, basi italazimika kulipa gharama na kuonesha kipindi hicho kama hakuna makubaliano maalum.

Hivi karibuni Mhe. Spika, *TVZ* wamekuwa wakitoa mialiko mbali mbali ya vipindi maalum juu ya siasa, uchambuzi, uchumi na jamii. Naomba sana Mhe. Spika, kupitia kiti chako Waheshimiwa Wawakilishi *TVZ* watakapowajia na mialiko kama hiyo naomba wasiwakatalie, wawakubalie ili vipindi hivyo navyo viweze kufanyika. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 32

Ujenzi pacha pacha wa Minara ya Simu

(Swali hili limeondolewa na Mhe. Mjumbe)

Nam. 33

Ununuzi wa Meli Mbadala ya Abiria

Mhe. Ali Denge Makame - Aliuliza:-

(a) Je, Mhe. Waziri, ule mpango wa Serikali kununua meli kubwa ya abiria ili kuondoa usumbufu uliopo wa usafiri Unguja na Pemba baada ya kukosekana Meli ya MV. Mapinduzi na MV. Maendeleo.

(b) Kama mpango huo bado upo utatekelezwa lini.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria kikao cha Baraza ili kutekeleza majukumu ambayo tumepangiwa.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 33 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kuwa serikali kupitia wizara yangu, bado ina mpango wa kununua meli nyengine kubwa na ya kisasa ya abiria inayokwenda kwa kasi, ambayo itaweza kutoa huduma nzuri kwa usafiri wa baharini na kuondokana na usumbufu wa usafiri wa wananchi wetu wa visiwa vya Unguja na Pemba. Pia kutoka Zanzibar na bandari za Tanzania Bara.

Mhe. Spika, serikali inashauriana na Shirika la Meli kuandaa utaratibu wa upatikanaji wa meli mpya, kupitia ufadhili wa taasisi mbali mbali ikiwemo kuangalia pia uwezekano wa kupata mkopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na taasisi za kifedha za ndani na nje ya nchi, ili kuweza kununua meli hiyo.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa umuhimu wa meli unaeleweka na hasa zikiwepo meli za serikali. Nataka kumuuliza Mhe. Waziri, kuna tatizo gani au mkwamo wa meli ya MV. Maendeleo tangu Julai mpaka hii leo hatujajua mafanikio yake ya matengenezo kuwa itapatikana lini au kuna tatizo gani la matengenezo. Wakati ahadi ilikuwa inategemewa meli hii tangu mwezi Oktoba kwa kuja kuhudumia wananchi. Mpaka sasa hivi kuna matatizo mengi ambayo yanatokea ya ajali za meli na maafa ya kuripuka kwa meli.

Je, atatwambia lini meli hii itafanikiwa kuja kufanya kazi hapa visiwani.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba Meli ya MV. Maendeleo iko Mombasa Kenya, wakati ilipopelekwa tulianza na chelezo sio cha *African Marine*, wanaita, imetengenezwa ile ikagongwa chini, lakini kuna kazi lazima iingie katika chelezo cha *African Marine.*

Sasa kuna kipindi walikuwa wana tatizo la uongozi *African Marine* ikawa hawachukui meli yoyote. Baadae baada ya ruhusa kutoka na meli yetu ikaruhusiwa kuingia katika chelezo. Sasa tatizo kwanza lazima watanguliziwe fedha ili waweze kupokea meli. Sisi tumeshawalipa robo tatu, tunataratjia

tutaingia katika chelezo tarehe 15/04/2010, matengenezo yetu yatachukua kati ya wiki moja mpaka mbili, tunatarajia mwisho wa mwezi wa April meli yetu itakuwa tayari. Sasa hivi katika chelezo kuna meli ya Bakhresa ndio ambayo ikitoka hiyo tunaingia sisi.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye kifungu a na b.

(a) Mhe. Spika, suala la ununuzi wa meli kubwa ya abiria tumekuwa tukilisikia au kupata taarifa yake kwa muda mrefu sana. kwa kuwa mipango hii mara nyingi inakuwa katika taratibu mbili, mpango ule wa muda mrefu na mpango wa muda mfupi. Je, Mhe. Waziri, suala hili la ununuzi wa meli liko katika program ipi.

(b) Tumepata taarifa kwamba yule mnunuzi wa meli ya MV Mapinduzi ambaye tulimtegemea kwamba atainunua kishajitoa katika ununuzi wa meli ile. Je, jambo hili ni kweli.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba tumekuwa tukisema tutanunua meli na bado dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kununua meli mpya kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi wa visiwa vya Unguja, Pemba na sehemu za Tanzania Bara.

Kama tulivyojibu katika swali la msingi kwamba hatuna pesa mkononi *cash* za kununulia meli, lakini serikali inazungumza na tulishawahi kuzungumza na Serikali ya China kwamba watupatie mkopo kwa kuinunua meli, lakini bado haijawiva.

Kwa hivyo, hatuwezi tukasema kwamba ni mpango wa muda mrefu au mfupi kwa sababu tukipata kesho au mwakani tutanunua, lakini lengo na dhamira yetu ni kununua meli kwa sababu bado tunahisi kwamba wananchi wa Zanzibar kutokana na uasilia wao ulivyo ni watu wa visiwani na wanahitaji lazima serikali iwe na mkono wake katika usafiri wa baharini.

Jibu (b) ni kweli kwamba mwaka jana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua kuiuza meli ya MV Mapinduzi kwa sababu imeonekana kwamba haiwezi tena kutoa huduma kwa hali iliyo hivi sasa.

Bahati nzuri kazi ya uuzaji iliachiwa Wizara ya Fedha na wao wakatoa tenda akashiriki mtu mmoja akatoa bei yake akabarikiwa meli, lakini tangu mwezi wa Agosti mwaka jana hakuja kununua mpaka mwaka huu.

Bahati nzuri baada ya kufanya juhudi nyengine katokezea mnunuzi mwengine na yeye kafuata taratibu zote ameshabarikiwa, kwa mujibu wa alivyotueleza nafikiri wiki hii anaweza akaingia kuinunua hiyo meli. Matarajio yetu makubwa sana kwamba hadi kati kati ya mwezi Aprili meli ya MV Mapinduzi itakuwa imeshauzwa.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipojibu swali la nyongeza la kwanza alisema kwamba meli ya MV Maendeleo bado haijaingia chelezoni. Kwa maana hiyo, iko baharini. Muda wa meli kukaa baharini inaonesha ni mkubwa sana hivi sasa. Je, fedha hizo za kulipia meli na kukaa baharini mpaka leo ni kiasi gani. Haoni kwamba ni busara meli ile kurudi ili ku-*save* pesa hizo pamoja na *allowances* ambazo zinatolewa kwa wafanyakazi waliomo katika meli ile.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kama nilivyojibu kwamba meli hii imetoka chelezo *to* chelezo. Kwa hivyo, hatuna zile gharama nyengine za uwekaji wa hii meli nje ya bandari kwa sababu tuna makubaliano maalum na ile chelezo cha kwanza. Sasa tunangoja itoke pale meli ya Bakhressa tuingize yetu sisi katika chelezo cha *African Marine.*

Hoja za Serikali

Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kura ya Maoni na Mambo Yanayohusiana na Hayo

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tutaendelea na majadiliano kwa kiasi fulani na hatimaye katika kipindi hichi hichi cha asubuhi tumuombe Mhe. Waziri afanye majumuisho tumeshafanya mawasiliano pale. Kwa hiyo, katika kipindi cha muda kama wa saa moja na nusu kutoka sasa hadi muda wa saa mbili tunaweza tukasikiliza majadiliano.

Wachangiaji waliopo wanazidi 15, sasa tunaweza tukamudu kiasi ya wanane kwa kutumia dakika 15 kila mmoja. Niwaombe basi ili tupate wachangiaji wengi zaidi pengine kwa kuwa mswada umeshajadiliwa vya kutosha, mambo yenyewe ndio yale yale, kama kuna jambo la nyongeza zaidi basi tufanye hivyo. Sasa tujikite kutumia muda mfupi kupata wachangiaji wengi zaidi.

Tumefanya hivi makusudi kwa sababu jambo hili lina umuhimu wake na uzito wake na inafaa wajumbe wakapata kuchangia wengi zaidi na wananchi wakaelewa kinachoendelea katika nyumba yetu hii.

Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Samia Suluhu Hassan na baadae Mhe. Mansoor Yussuf Himid.

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Ahsante Mhe. Spika, nashukuru kunipa nafasi kutoa mchango wangu mdogo katika suala hili. Mhe. Spika, Mswada wa Kura ya Maoni umewasilishwa Barazani lakini niseme kwa kigezo cha demokrasia basi umechelewa kidogo kuwasilishwa.

Ni bahati mbaya kwamba umeangukia katika suala hili ambalo sasa hivi tunalo mikononi, lakini kwa kigezo cha utawala bora ulikuwa uje mapema sana. Kwa sababu kuna mengi ambayo yamepita yangehitaji au yalihitaji sauti ya wananchi wenyewe. Lakini hata hivyo, nichukue nafasi hii sana kumshukuru Mhe. Waziri kwa kuuleta sasa hivi kwa ajili ya hili linalotukabili.

Mhe. Spika, mimi nilifanya kazi ya kupitia *literature* kidogo ya kura ya maoni na nikakuta kuna aina mbili za kura za maoni ambazo nchi inatakiwa kuwa nazo. Moja ni ile ya lazima au wenyewe wanaita *obligatory referendum* ambayo huwa inafanywa wakati wa shughuli kama hii ambayo tunayo sasa hivi. Kuna tatizo la kisiasa tunataka kuliamua. Limekuwa *debated* kwenye Bunge au kwenye Baraza lakini tumeona kuna haja wananchi watie sauti zao. Kwa hivyo, hiyo ni moja.

Lakini ya pili ni ile isiyo ya lazima inaweza ikatoka kwa wananchi wakaomba *referendum* au inaweza ikatoka serikalini au kwenye Baraza. Hii kawaida mtu unaweza kuamua kushiriki au kutokushiriki inategemea *topic* ambayo inapigiwa kura za maoni.

Kwa hiyo, huu ni mtindo ambao nchi ambayo inakuza demokrasia ni lazima wawe nayo. Kama nilivyosema mwanzo ni bahati mbaya kwamba imekuja wakati tuna tatizo hili, lakini ni hatua moja mbele katika mwenendo mzuri wa demokrasia na utawala bora.

Mhe. Spika, tukiangalia kwa nini tuwe na mtindo kama huu kuna faida nyingi. Moja ni kwamba tunapata demokrasia ya moja kwa moja, nchi inatoa demokrasia moja kwa moja kwa wananchi kutoa sauti yao katika jambo la maamuzi hasa ya kisiasa. Kwa maana hiyo, inachangia utulivu ndani ya nchi. Kwa sababu kama *decision* ikitolewa na wananchi hawaji tena ku-*query* kwa nini kumefanywa hivi wakati wenyewe ndio wameamua kama hilo.

Lakini jengine katika kufanya hivyo inaondosha pia mitafaruku ndani ya nchi. Kama nilivyosema hoja zinakuwa chache na kwa hiyo huepusha pia mianya ya rushwa.

Mhe. Spika, kama tunatoa fursa kwa wananchi kutoa sauti yao katika maamuzi yetu, ina maana hata wale ambao kwa lugha ya kigeni wanasema ni *silence skimming of their craft few*. Kuna watu ambao wanafanya mambo yao kimya kimya na linatoka tu kwa wananchi. Kwa hiyo, hili nalo watu watakuwa *very careful* kwa sababu anajua akifanya hivyo wananchi wata-*question* na pengine wataomba kura ya maoni.

Mhe. Spika, wakati napitia literature nimeona kifungu kimoja kinasema *Washington Words of Wisdom* na kwa ruhusa yako naomba nizinukuu. Hizi zinasema hivi: *"The people will always be nearer to right those who have a selfish interest in controlling the issues".*

Kwa hiyo, kama tutatoa hii, ina maana tukitoa fursa ya kura za maoni watu watakuwa karibu zaidi kuwarekebisha wale ambao wanafanya mambo kwa maslahi yao. Kwa hiyo, hii ndio maana ya kuwa na kura za maoni katika nchi. Mhe. Spika, mimi sioni ubaya wa kuwa na kura ya maoni katika nchi.

Mhe. Spika, labda sasa niliunganishe suala la kura ya maoni na hili ambalo linatukabili. Mhe. Spika, kiongozi aliye makini ni yule ambaye anataka kuona nchi yake wakati wote inapiga hatua za maendeleo na inaepukana na mizozo. Kama kuna mizozo basi hatua za maendeleo zinaweza zikawepo lakini si kwa kasi ile ambayo yangetokea kama hakuna mizozo.

Mhe. Spika, kiongozi makini ni yule ambaye anataka kurithisha nchi yake kwa kizazi kijacho, nchi ambayo imetulia ina umoja na ina maelewano. Nadhani hili tulilonalo linaelekea huko.

Mhe. Spika, Samia Suluhu Hassan sasa hivi, Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Mhe. Juma Duni Haji na wengine wote humu ndani tunapita na tumesakuwa miaka imepanda. Kesho na kesho kutwa tunatoka kwenye siasa kwenye utumishi wa serikali. Lakini je, tunawaachia watoto wetu au wanaotufuata kitu gani. Tunawaachia nchi ya mizozo, misuguano na mapambano, au tunawaachia nchi ambayo ina utaratibu. Tunaweka utaratibu ambao wakija wanakuta kama jambo lina utata, basi kuna utaratibu wa kura ya maoni wananchi wataamua, viongozi wanalazimika kufuata hilo.

Kwa sababu kiongozi aliye makini nadhani anataka kuacha nchi katika hali iliyo nzuri, katika hali ya maelewano, katika hali ya utaratibu ulio mzuri kisheria na kiutawala.

Sasa mimi nahisi kwamba kuwa na kura ya maoni kunatuelekeza huko. Nilikuwa napitia nikaangalia kura za maoni zinavyofanywa nchi mbali mbali, hasa niliingia kwenye *European Union*, nikakuta kumbe wenzetu wamekuwa na mtindo wa kura ya maoni toka mwaka 1973. Mara ya kwanza walipiga kura ya maoni ndani ya *European Union* kuangalia kama kuna umuhimu wa kuongeza zile nchi zao ndani ya *European Union.*

Lakini kila baada ya muda kumekuwa na kura za maoni zinapigwa ndani ya nchi zile, nchi moja moja au wananchi katika eneo fulani, kwenye jambo moja au jambo jengine. Kwa hiyo, Mhe. Spika, mimi niseme tu kwamba ni utaratibu mzuri na nadhani utatuweka nchi yetu katika hali ambayo ni ya maelewano na hali ambayo inawapa uwezo moja kwa moja wananchi kutoa mawazo yao katika jambo fulani. Mhe. Spika, mambo mengi yamepita huko nyuma ambapo wananchi wangeshirikishwa pengine yangeamuliwa vyengine na sivyo vile ambavyo wanasiasa tumeamua. Kwa hiyo, huu ni mwendo mzuri.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja, pengine na wanawake wa Unguja na Pemba, sisi tunaunga mkono mtindo huu. Kwa sababu sisi wanawake utatupa sauti kubwa ya kusema yetu kwa kupitia mtindo huu. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa wazima wa afya na siha. Pili Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kunipa nafasi hii na mimi kutoa mchango wangu.

Mhe. Spika, nilijiandaa kwa kusema mengi, lakini kama sote tunavyokubali na hali halisi ilivyo, pengine kusema sasa ni kuharibu. Niwapongeze Wawakilishi wenzangu wote waliotangulia kuzungumza, Mhe. Haji Omar Kheri, Mhe. Haroun Ali Suleiman, Mhe. Mwinyihaji Makame, Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban, Mhe. Burhan Saadat Haji, Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Mhe. Abass Juma Muhunzi, Mhe. Juma Duni Haji na wengineo kwa michango yao sahihi, yenye maana na iliyobeba uzito na matumaini ya wananchi wa visiwa hivi.

Mhe. Spika, kwa mnasaba huo, mimi nisimame tu na kusema kwamba naunga mkono hoja. Fursa na nafasi ya kulisimamia suala hili tutakuwa nayo. Nikiwa Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Kiembesamaki, nikiwa Waziri kwa maana ya Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi, tutakuwa na fursa na nafasi ya kutosha ya kulisemea hili, kulisimamia na hatimaye kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu kufika mwisho ulio mwema kwa maslahi ya nchi yetu.
Mhe. Spika, nitawaachia waungwana waendelee kuchangia. Naunga mkono hoja, ahsante.

Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin: Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo kutuamsha wazima na tukaweza kufika katika Baraza lako hili tukufu. Mhe. Spika, pia nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Baada ya shukrani zangu hizo naomba nichukue nafasi hii pia kumshukuru sana Mhe. Waziri aliyewasilisha mswada huu kwa kuuandika vizuri na kuuwasilisha vizuri ambapo maandishi na uwasilishaji wake unaleta matumaini kwa wale wanaoitakia kheri nchi hii ya Zanzibar. Mhe. Spika, pia naomba niwashukuru Wanasheria waliotayarisha mswada huu. Nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikumshukuru Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mhe. Haji Omar Kheri.

Mhe. Spika, baada ya hapo, nasema nakubaliana na maneno aliyowahi kuyasema Mhe. Mnadhim wa Upande wa Upinzani kwamba "Taarab iliyokwishapigwa kwa vinanda vizuri wewe ukaja ukapiga kinanda itakuwa ni kama unayefanya mchezo".

Mhe. Spika, wengi waliozungumza wamelizungumza vizuri suala hili la kura ya maoni. Mimi nimesimama ili kuwatoa wasi wasi wananchi wangu wa Jimbo la Mtambile. Kwa sababu kabla sijaja kwenye kikao hichi walikuwa na wasi wasi kama kweli mswada huu utawasilishwa Barazani. Nikawaambia kwa kweli sina hakika kwa sababu mpaka naondoka Pemba miswada haijapatikana. Kwa hivyo, sijui kama umo au haumo. Sasa nadhani tokea jana wamekwishaipata hii taarifa kwamba mswada huu umewasilishwa Barazani. Mhe. Spika, kwa mtazamo wangu nadhani kwamba mswada huu utapitishwa na Baraza lako hili tukufu.

Mhe. Spika, wao walikuwa na wasi wasi kweli mswada huu ukifikishwa utapitishwa. Kwa sababu wasi wasi wao wanasema kwamba hawa Waswahili yale wanayoyasema katika vinywa vyao wana mengi waliyoyaficha katika vifua vyao. Nikawaambia hapana, mimi ninavyojua haya wanayoyasema na yale yanayokuwa katika vifua vyao yote huwa yanalingana sawa sawa na nina imani kubwa kwamba mswada huu utaweza kupitishwa kama ilivyopitishwa ile hoja.

Kwa sababu katika mwaka huu wa 2010 Mhe. Spika, tumewaweka wananchi wetu roho juu katika vipindi viwili. Mwezi ule wa Januari wakati inawasilishwa ile hoja walikuwa na wasi wasi kwamba hoja hii itapitishwa kwenye Baraza? Kwa bahati nzuri kwa pamoja sote tuliipitisha ile hoja na tukatoa maazimio tukayapeleka serikalini.

Naishukuru sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kutekeleza yale maamuzi ya Baraza la Wawakilishi. Hii inaonesha dhahiri kwamba Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Sita inawajali wananchi wake na inawatakia maslahi na maendeleo ya kudumu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, napenda nitamke kwamba naunga mkono mswada huu mia kwa mia ili tuweze kuupitisha na hatimaye hatua zinazofuata ziendelee. Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba niwaambie Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kwamba lile analolifanya Mhe. Spika kila asubuhi katika Baraza hili labda wengine waliona kwamba ni la mchezo, lakini lina umuhimu mkubwa la kuiombea dua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Baraza la Wawakilishi.

Katika dua ile ya kuiombea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuna kipengele kinasema kwamba "Tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe hekima na busara Rais wa Zanzibar ili akishirikiana na viongozi wenziwe aweze kuongoza kwa haki".

Sasa Mhe. Spika, hili neno hekima ni neno kubwa sana. Mwenyezi Mungu anapomjaalia kiumbe hekima anakuwa ni mtu mzuri sana. Utakapokosa hekima hata uwe na elimu ya kiasi gani, lakini kama huna hekima kwa kweli ni matatizo. Mhe. Spika, inavyoonekana dua yetu Mwenyezi Mungu ameipokea na kumpa hekima Rais wa Zanzibar aliyepo sasa kwa kushirikiana na viongozi wenziwe mpaka wakafikia katika hatua hii ya kuiweka nchi katika utulivu na usalama.

Kwa hivyo, naomba Mwenyezi Mungu aendelee kumuongezea hekima Rais wetu na yule mwengine atakayemrithi afuate nyayo zake, ili nchi yetu iweze kuwa katika utulivu na amani na tuweze kuendelea.

Mhe. Spika, kwa kumalizia na mimi naomba niombe dua kwa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kulibariki hili. Ewe Mwenyezi Mungu wetu mlezi, tunakuomba usizigeuze nyoyo za viongozi wetu na zetu sisi baada ya kwisha kuziongoza katika njia njema na utujaalie neema na rehema katika nchi yetu, kwani wewe ndie muongozaji na ndie mwenye kutoa.

Mhe. Spika, baada ya dua hiyo nakushukuru, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: *Bismillahi Rahmani Rahiym.* Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii adhimu ya mimi Mahmoud Thabit Kombo kuwa sehemu ya historia inayotungwa na Baraza hili ambayo itakuwa ni historia ya nchi yetu Zanzibar kama wazee walivyotangulia kuweka historia ya Mapinduzi.

Mhe. Spika, pili naomba kwa dhati kabisa kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiongozwa na Dk. Amani Abeid Karume kwa kukubali moja kwa moja maazimio yaliyopitishwa na Baraza lako tukufu, tukiwa sisi sote kwa pamoja tumejumuika katika kupitisha maazimio hayo na leo umeletwa mswada huu wa sheria. Pia naomba nimpongeze wakati huo huo kwa kukubali yale maazimio yaliyopitishwa kabla juu ya suala la mafuta, juu ya suala la maeneo huru na mengineyo yote.

Katika hotuba yake Mhe. Rais kisiwani Pemba siku ya Sherehe ya Mapinduzi alisema suala la mafuta tayari alikwishalimaliza na mwenzake Rais Jakaya Mrisho Kikwete na hilo litaondoshwa rasmi katika orodha ya mambo ya Muungano.

Sasa Mhe. Spika, sheria hii imetokana na maazimio hayo ambayo tumepitisha katika Baraza lako tukufu. Mhe. Spika, naomba kukupongeza wewe binafsi kwa kutuongoza kufika katika mambo yote haya na leo mtu kama mimi mdogo kwa umri kupata bahati ya kuwa sehemu ya historia.

Mhe. Spika, michango imetolewa mingi kwenye mswada lakini mimi nataka kuzungumzia eneo moja ambalo Waheshimiwa Wawakilishi wengi hawajaligusa, nalo ni eneo la vijana.

Mhe. Spika, Mhe. Samia Suluhu Hassan wakati akizungumza sasa hivi amezungumzia rika lake ambalo naamini rika ya wengi humu ndani ukimuacha Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Mansoor Yussuf Himid, Mhe. Amina Iddi Mabrouk na mimi mwenyewe, sisi tuko kwenye *lower generation* ya vijana. Lakini wengi wametupita kwa umri na naweza kusema wengine wanatuzaa ndani ya Baraza hili la Wawakilishi, wengine wanatujukuu kama kina Mhe. Ashura Abeid Faraji.

Kwa nini nasema hivyo? Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu mimi binafsi sina cha kuilipa nchi hii. Nchi hii ndio iliyonikuza, ndio iliyonilea, ndio iliyonisomesha mpaka nikafika hapa.

Mhe. Spika, mimi nilianza masomo yangu hapa hapa Zanzibar, nilianza kusoma Saateni, nikenda Skuli ya Tumekuja, baada ya hapo Skuli ya Hamamni, baada ya hapo nikenda Arusha kwa kipindi fulani Moshi, nikarudi tena Zanzibar nikaendelea Skuli ya Hamamni. Majengo yalipodata Skuli ya Hamamni sisi ndio wanafunzi wa mwanzo kwenda Mwanakwerekwe kwenye Mabanda ya Maonesho wakati ule mpaka vifaa vya kilimo tukavikuta vipo bado. Baada ya hapo nikenda Skuli ya Lumumba nikamaliza na kupata nafasi ya kwenda kusoma nchi za nje.

Mhe. Spika, tulipokuwa tunapata nafasi wakati ule ya kwenda kusoma nje nakumbuka vizuri kabisa Mhe. Waziri wa Elimu alikuwa ni Marehemu Soud Yussuf Mgeni na Waziri Kiongozi alikuwa ni Maalim Seif Shariff Hamad. Wakati ule *scholarship* zilikuwa ni nyingi zaidi kuliko hivi sasa kwa sababu ni nafasi nyingi zilizokuwa zinatangaziwa kuliko ile idadi ya watu waliokuwa wanaomba. Mimi nilikuwa mmoja wapo katika walioomba nafasi zile na chuo changu tulikwenda wanafunzi 32. Mhe. Spika, nina mantiki ya kueleza haya yote na nitaeleza baadae mantiki nini.

Mhe. Spika, tulikwenda vijana 32 kusoma katika chuo changu, katika vijana 32 tulirudi 15 nakumbuka na majina yao wote ninawafahamu tuliorudi. Katika wale vijana 15 tuliorudi hapa wengi wao waliripoti kazi, lakini kutokana na mazingira yaliyokuwepo wakati huo, basi naweza kusema vijana wale waliathirika tumebaki wawili tu tuliokwenda Chuo Kikuu kimoja hivi sasa, 30 ya wale hawapo.

Leo Mhe. Spika, kutokana na matatizo haya tuliyokuwanayo nchini kwetu, sisi wenyewe tume-*create internal refugees*, kila mjumbe mmoja hapa aidha anamjua mtu, au ana mtoto wake, au ana mtu wake kule nje, ikiwa anaitwa kwa jina la Kizanzibari, akiwa anaitwa Nkurunziza au majina mengine hayo ni tofauti, lakini wapo. Hii ni kutokana na ile hali iliyokuwepo hapa.

Mhe. Spika, mimi nimebahatika kuona chaguzi mbili nyengine nilikuwa sipo niko masomoni. Katika chaguzi hizi mbili tumesoma mambo mengi sana. Mhe. Spika, nchi hii tumejaaliwa na neema kubwa sana ya wasomi, tumejaaliwa na neema ya vijana wazuri ambao wote wana nia njema, wana hamu ya kutaka kurudi nchini kwao. Hakuna yeyote anayependa kukaa katika mazingira aliyokuwanayo.

Mhe. Spika, nilimsikia juzi Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali akijibu maswali juu ya walimu ya Sayansi. Mhe. Spika, sisi tuna wanasayansi wengi sana, hawapo tu hapa lakini tuna wanasayansi wengi sana. *Bench* yangu mimi niliyokwenda kusoma watu wote 32 tuliotoka Skuli ya Lumumba tulikwenda Sayansi. Mhe. Spika, Maalim Juma Duni Haji amenisomesha mimi kwa hiyo anaelewa.

Leo kila mtu ana mtu mmoja ameguswa nae nje. Mimi mwenyewe nina watoto wa dada zangu wawili wako kule nje, majina yao hata siyaelewi, maana yake nikenda naambiwa nisiwaite kwa majina yale *public* na wao. Bahati nzuri nakwenda kuwatembelea na ninawaona na hii ndio hali tuliyofikia. Lakini wale wote wana hamu, wanaungana na sisi, wanatupongeza katika mambo haya na wanatuunga mkono kwa sababu leo tunaweka historia.

Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu akitujaalia tumezungumzia suala la mafuta kesho kutwa hapa patakuwa na visima kadhaa wa kadhaa vya mafuta, tutakuwa tunachimba sisi mafuta yetu wenyewe. Mwenyezi Mungu akitujaalia atatuongoza kwa neema zake, neema ile tuitumie vizuri, tuwe kuliko hao Dubai wanaosifiwa wanaojenga maghorofa makubwa, tuwe kuliko hawa Abu Dhabi ambao wanachimba mafuta mengi.

Mhe. Spika, Mhe. Mansoor Yussuf Himid alizungumzia kushukuru kupata nafasi kutoka Norway ya kuwapeleka vijana kusoma *Egineering* katika masuala ya mafuta. Lakini Mhe. Spika, nikuhakikishie kwamba kuna vijana ambao tumesoma nao wazalendo waliosomea mambo ya *petroleum engineering*, mambo ya *chemical engineering*, mambo ya *geological sciences* ambao tumekwenda pamoja na wote wana hamu ya kurudi.

Mhe. Spika, mimi nipo katika mtandao wa *internet* ambao unazungumzia masuala haya ya kisiasa sana, hali ya Zanzibar na kadhalika, mtandao wa *Zanzinet* ambao ni maarufu sana na Wawakilishi wengi wanaufahamu humu ndani. Mtandao ambao unatoa mambo mengi sana ambayo yote haya tunayozungumzia huku Mhe. Spika, utashangaa kwenye mtandao ule yapo pamoja na hizi picha ambazo zinapigwa humu ndani kwenye mtandao huo zinatolewa picha hizi.

Mhe. Spika, juzi nilikuwa nawajibu wana mtandao huo, kuna mmoja alileta kidogo kama kutoamini amini hivi, kama kauli ya Mhe. Muhyddin alivyosema kwamba wengine wanatamka kwa mdomo, lakini kwenye moyo tofauti. Sasa huyo mmoja kidogo alileta kauli kama hiyo nikamwambia hapana, katika jambo hili sote tuko pamoja na *new generation* ya nchi hii, vijana wa nchi hii wote wako tayari.

Mhe. Spika, kwa niaba ya vijana wote wa nchi hii, narudia tena kwa niaba ya vijana wote wa nchi hii wanaliunga mkono jambo hili. *Generation* inayopita iweze kuwaachia amani na utulivu ili hayo mafuta na mambo mengine mazuri kama hayo tutakayoingia, basi yaweze kutuneemesha sisi vijana, wazee wetu wakati huu ambao mtakuwa ni nyinyi tunawalea pamoja na kuwaachia kizazi kijacho. Mhe. Spika, hii ni historia ya aina ya pekee ambayo inawekwa hapa na Baraza lako tukufu la Wawakilishi.

Mhe. Spika, azimio jengine ambalo nadhani tunatakiwa tujiwekee sisi wawakilishi ni kuhusiana na huu mfumo mzima ambao naamini Mhe. Rais atakuwa na mkono wake katika kuuharakisha na kufanyika haraka iwezekanavyo. Kwa sababu thamani ya amani ni kubwa mno kuliko hasara ya kukosa amani. Kwa hivyo, naamini hilo nalo litapitishwa.

Mhe. Spika, naomba pia nikupongeze wewe mwenyewe binafsi nilikusikia unafanya *interview* na *Voice of America* Mhe. Spika, nilibahatika kusikiliza *interview* yako. Katika *interview* yako umeeleza hasa kwamba nini msimamo wa chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi juu ya suala hili zima. Pia uliulizwa swali la habari ya kura za maoni kama litafanyika sambamba na uchaguzi. Ukasema maamuzi yatakayopitishwa ndio yatakayoheshimiwa. Nakupongeza sana Mhe. Spika, kwa kauli yako ile.

Mwisho kabisa kwa kuwa Mhe. Spika, tunaweka historia, mimi ni mdogo kiumri, kwenu wengi hapa mimi ni mdogo kwa umri. Mhe. Spika, katika kuweka historia naomba na mimi jina langu liwemo. Kwa hivyo, nilikuwa nakuomba sana. Mara nyingi huwa tukitizama vipindi vya Bunge huwa tunaona kuwa zile hoja nzito ambazo zinawagusa wananchi wote au miswada mizito ambayo inagusa serikali na kadhalika kama huu. Maana huu uliwaalika hata watu kutoka nje nao kutoa maoni yao. Naomba katika kuunga mkono hoja tufanye kama ule mfumo pia wanaotumia wenzetu, tuunge hoja mkono mmoja mmoja ili jina la kila mjumbe liweze kuingia katika orodha yako ya kihistoria.

Mhe. Spika, hilo naliomba sana kwako na ninatumai ombi hilo utalizingatia na inawezekana katika kanuni tumetazama, kwa hisani yako tunakuomba tunataka tuingie katika historia hiyo ya kuunga mkono jambo hili.

Mhe. Spika, kwa niaba yangu binafsi, kwa niaba ya Chama changu cha Mapinduzi, kwa niaba ya Jimbo langu la Mpendae na kwa niaba ya vijana wote wa Kizanzibari waliokuwepo Zanzibar na nje ya Zanzibar, naomba kuunga mkono mia juu ya mia hoja hii, ahsante Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba: Mhe. Spika, kwanza kabisa nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetuwezesha siku ya leo kuweza kukutana hapa.

Pili, Mhe. Spika, nichukuwe nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii adhimu kuchangia katika mswada huu ambao kwa kweli ni muhimu kwa taifa letu.

Mhe. Spika, nichukuwe nafasi hii tena kumshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Rais wa Zanziabr na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu wa Chama cha CUF, Maalim Seif Sharif Hamad kwa uungwana, utu na ubinadamu ambao wao wameuonesha. Ninaamini haya yote ambayo tunayajadili leo basi yasingekuja kama sio watu hawa wawili kukaa kwa pamoja na kuweza kutafakari na kuona nini tunatakiwa tufanye katika nchi yetu.

Mhe. Spika, madhumuni ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa ni kuwakomboa Waafrika wa visiwa hivi ambao walikuwa wanaishi katika hali duni. Lakini sio kuwakomboa ili wao wawakandamize wengine hapana, kuwakomboa ili washirikiane na makabila mengine katika kukiendeleza kisiwa hiki. Ndio maana Mzee wetu Mzee Karume moja katika hatua aliyochukua, aliueleza umma kwamba sasa umefika wakati tuoaneni nchini makabila mbali mbali. Muhindi akamuowe Muafrika, Muafrika akamuowe Muarabu ili kuondoa tofauti zilizokuwepo kabla ya Mapinduzi.

Mhe. Spika, ni kweli tukitaka tusitaka tofauti hizo zimeondoka. Mimi mara nyingi huwa napenda kuzungumza ukweli tu, yale yote ambayo tumekwenda kinyume na yule mzee basi nchi hii inalaanika. Mzee Karume aliyajua haya kwamba vitakapokuja vyama vingi ni lazima Wazanzibari kwa tabia zao zilivyo watarudi kule kule kwa zamani, pamoja na vyama vingi. Lakini vyama vingi sio cheti cha watu kuhasimiana.

Ninachoshangaa tena ninashangaa sana Mhe. Spika, kuna baadhi ya watu wanalibeza hili suala. Hivi kuwa kiongozi ni mtihani kwa Mwenyezi Mungu. Mimi kama Mkuu wa Mkoa nitatakiwa niende nikajibu siku ya siku nilifanya nini nikiwa kama Mkuu wa Mkoa kwa waja wake Mwenyezi Mungu. Hivi jamani hatuone kuwa wakati wa uchaguzi hali inakuwaje, hatuoni.

Mimi ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba wakati wa uchaguzi hali naiona, tangu wakati wa maandalizi mpaka wakati wa uchaguzi wenyewe na pengine mwaka mmoja baada ya uchaguzi, basi hali haiwi nzuri, watu wanahasimiana, watu wanauana, watu wanapeana vilema ndio malengo ya Mapinduzi hayo?

Hivi karibuni nilizungumza na Masheha wangu wa Wilaya ya Mkoani nikawaambia mimi nitashangaa kama kuna Sheha atakayelipinga suala hili, kwa sababu kati ya watu wanaoathirika wakati wa uchaguzi ni Masheha wangu. Utapigiwa simu saa 8 za usiku mheshimiwa Sheha fulani kavamiwa, Sheha fulani kapigwa.

Sasa nikawapa mfano Micheweni daftari limepita, limemalizika salama. Je, kuna Sheha au kuna mtu yeyote aliyeguswa, Wete halikadhalika limemalizika jana kuna mtu ambaye aliguswa na ninaamini pia Chake Chake na Mkoani hakuna atakayeguswa. Haya yote ni kutokana na mazungumzo tu ya watu wawili hawa.

Lakini halikadhalika Tumbatu. Awamu ya kwanza tulisikia hasa mama katoka jicho. Hali hii tutaendelea nayo mpaka lini. Wallahi wasababishaji ni sisi viongozi, lakini wanaopata hatia sio sisi viongozi, kwa sababu wengi wetu kati

yetu unapofika wakati tunalindwa. Upande ule wa wapinzani wanalindwa na maaskari wao na huku chama tawala tunalindwa. Wanaoathirika maskini ya Mungu ni watu ambao hawana hata hatia ya aina yoyote, ndio malengo ya Mapinduzi?

Leo wenzetu hawa wawili wanataka kukurejesha katika yale malengo. Watu wanasema, inashangaza sana Mhe. Spika. Au kuna mradi unapatikana wakati fujo zinapotokea, ni lazima kuna mradi unapatika wakati fujo inapotokea na ndio maana kuna wengine hawataki kuunga mkono suala hili. Kule bila shaka kuna michango hupewa watu maalum ili kuweza kusimamia harakati za mapambano na huku halikadhalika. Sasa wale ambao wanapokea hawatoweza kufurahi. Lakini hivi hayo unayoyapata na unahakika kwamba kuna watu wanaathirika je, Mwenyezi Mungu atakuwacha.

Mhe. Spika, ni lazima tufikie pahala tuelezane ukweli, hali ya visiwa sio nzuri. Muda mfupi tu hawa viongozi walivyokwisha zungumza unaona raha yake. Kuna viongozi pale wana shida chungu nzima ambazo mimi kama Mkuu wa Mkoa naweza kutekeleza, Wallahi walikuwa wanaogopa kuja afisini kwangu. Lakini leo wanakuja kwa mapana, Alhamdullilahi nashukuru, na uongozi kwangu unakuwa mgumu kwa sababu wale ndio wenye Pemba, huo ndio ukweli wenyewe, wale ndio viongozi wa Pemba. Nilihitaji msaada wao, lakini kutokana na siasa ilivyokuwa chafu, basi msaada wao huo siupati.

Mhe. Spika, nasema humu ndani na hao viongozi wa nje yeyote mimi naamini anayekwenda kinyume na kitu hiki basi Mwenyezi Mungu anajua vya kumlipa. Lakini ninachoomba nia zetu ziwe safi kwa sababu lengo la kuwepo katika uongozi, uongozi unakuja kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Wewe kama ni waziri aliyekupa ni Mwenyezi Mungu sio mtu mwengine.

Mhe. Amani amepewa tu uwezo na Mwenyezi Mungu kukuchagua wewe. Pia Mwenyezi Mungu atakuja kukuuliza siku ya siku umefanya nini. Kumbe cha kufanya unataka hii nchi iwe na fujo na watu wauwane ndio unavyotaka. Tumuogope Mwenyezi Mungu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, hata viongozi hawa wa huku CCM wanapokuja Pemba siku za uchaguzi kila mmoja huwa tumbo joto. Uchaguzi wa mwaka 2005 Mhe. Spika, ndugu yangu huyu Mhe. Samia Suluhu Hassan na Zainabu Khamis Shomar na bi Asha Bakar, walikuwa katika nyumba tayari watu wameshasema wale viongozi wa CCM wako twendeni tukawashambulie. Haraka sana Mhe. Samia Suluhu alinipigia simu. Tena tizama hatari iliyokuwepo. Mimi binafsi siku kama hizo kusali ninasali kwa njia ya mtego.

Nakumbuka hivi hivi sisahau nilikwishafunga sala ya Adhuhuri Allahu Akbar. Basi niliwacha sala nikasikiliza simu. Hii ndio nchi inavyokwenda. Nikasikia sauti ya Mhe. Samia anasema Mheshimiwa njoo utuhami hali ni mbaya, watu wanakuja kutuuwa. Pale pale nikakata sala nikaondoka na maaskari. Ni kweli niliwakuta njiani watu na mapanga wanaelekea katika nyumba ambayo wamefikia. Aah! Jamani tumefikia hapo.

Sasa leo Mhe. Spika, imekuja neema ambayo kaileta Mwenyezi Mungu, kisha wanatokea watu ati wanazungumza mambo ya ajabu ajabu. Haya ni mambo ya Mhe. Amani, nini? Ndio maana nikasema kuna mradi. Kwa hivyo, tutakapopatana huo mradi utakuwa haupo, hizo fedha zilizokuwa zikitumika katika mradi huo Mhe. Spika, itabidi ziende katika maendeleo ya wananchi.

Mimi kule Pemba Mhe. Spika, natumia nguvu kubwa ya vikosi, katika kuhakikisha kwamba amani inapatikana. Pamoja na hayo lakini matatizo yanatokezea. Sasa fedha zile badala ya kutumia na tunamlenga nani Mhe. Said Ali Mbarouk, kwani huyu ni mtu wa Nigeria, tunamlenga nani Juma Duni. Tunaumizana wenyewe kwa wenyewe ndugu baba mmoja mama mmoja.

Mhe. Spika, mimi katika kuzungumza Pemba kule, niliwaambia mimi nitakushangaeni watu wa Pemba mkisema kwamba hili jambo hamlitaki. Nyinyi tayari mna serikali shirikishi ndani ya majumba yenu, mnakataa kitu gani. Utakuta Mwenyekiti wa Wilaya ya CCM ni CCM na mkewe ni CUF si serikali shirikishi tayari. *(Makofi/Vicheko).*

Halikadhalika na CUF. Kuna mmoja kugombea anagombea lakini mkewe CCM, sasa si tayari serikali shirikishi jamani. Sasa kule Pemba mnasemaje hakuna familia hata moja hata kama hapa utawauliza wajumbe, hata ya Mhe. Abubakary ni lazima japo ndugu yake au mjomba yake atakuwa ni CCM. Lakini Mzee wetu Mzee Karume alisema, tushirikiane, tupendane, tuoane ili kuweza kuijenga nchi hii na tuliona kabla ya kuja hivi vyama vingi, hivi vyama vingi nuksi Wallahi, tuliona, tulistarehe. Sheikh Nassor tukikutana naye Ahsalamu Alaykum hapana. Lakini sasa hivi kama tutaendelea hivi itakuwa vizuri sana. Kule tulikuwa hatuangaliani msione hivi leo tunacheka.

Mhe. Abdalla Juma anaona aah! Mkuu wa Mkoa huyu mshenzi kweli yule, ndio. Sasa mpaka lini tutaendelea na hali hii. Turudini kwa Mwenyezi Mungu tushirikiane na tuondowe mashaka ya ndani na tuondowe mawazo potofu. Ooh! Sijui labda watabadilika, wakibadilika si tupo tutaitana tuelezane ukweli.

Mhe. Spika, nisipoteze muda wako, nasema mimi naunga mkono hii hoja kwa asilimia mia tano kwa mia tano. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Spika: Ingekuwa Meja Mstaafu Juma Kassim Tindwa ni msemaji wa mwisho, basi ingekuwa ni jambo jema sana. Lakini kumbe nilikwisha waahidi na kuna wengine nimeshawataja tayari, kwa hivyo sitaki kwenda kinyume na ahadi hiyo.

Mhe. Aziza Nabahan Suleiman: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kunipa nafasi niweze kidogo kutoa mchango wangu kwenye mswada huu.

Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii. Wallahi naumwa leo, lakini nimefurahi kunipa nafasi hii ili nikipata kidogo na mimi kuchangia.

Mhe. Spika, kwanza niwape hongera walioyaanzisha wakayaandaa, wakayakubali, wakaweka mswada, wakatunga na sheria wakatuletea Baraza la Wawakilishi. Nikisema hivyo maana yake tuliyoyaanzisha sisi Baraza, ikatoka ikenda serikalini, serikalini ikaenda mahakamani. Kwa hivyo, mihimili yetu yote mitatu ilichangia kufanya jambo hii kwa maslahi ya Wazanzibari.

Pia Mhe. Spika. Huyu Mhe. Juma Kassim Tindwa sijui yuko wapi alinikopia mambo yangu mengi na tungekuwa tunakaa pamoja basi ingekuwa labda tumekopiana, kama watoto watundu wa shuleni. Lakini mimi nataka niseme kwamba yale maneno aliyoyasema Mhe. Tindwa ni ya kweli matupu.

Mhe. Spika, ukishafika wakati wa uchaguzi hapa tunatafunana, tukishamaliza uchaguzi basi tunaowana. Ndio, tunaowana tunakuwepo pamoja tunashirikiana. Watu wengi hapa ndio hayo aliyosema Mhe. Tindwa, kuna CUF ana CCM na kuna CCM ana CUF, katika familia hakuna CUF watupu wala hakuna CCM watupu.

Mhe. Spika, haya sio kwa sababu ya lolote, isipokuwa ni kwa sababu ya vipi tunaishi Zanzibar. Zanzibar tunaishi sote ni ndugu na huwezi kwenda kwenye familia moja au nyengine usije baadae mwisho mkakutana, mtakutana tu. Mimi familia yangu nusu CCM na nusu CUF, tumegawana sawa kwa sawa. Lakini tunafanya kazi zetu za kifamilia hatutiliane mambo yetu ya itikadi, kila mtu anafanya lake analoliona linamfaa kwa maslahi yake.

Kwa hivyo, naona ajabu Wazanzibari tulivyo, sisi Mwenyezi Mungu hasa visiwa vyetu katuweka pamoja tokea tulivyoumbwa katika dunia hii, halafu ametupa imani kubwa sana ni tofauti na watu wengine. Ukienda hapa na Bara tu utakuta sisi kidogo ni tofauti. Sisi tuna imani ambayo alitupa mwenyewe Mwenyezi Mungu. Sasa leo naona ajabu tumekuwa tunaziondosha tu kwa lazima maana yake. Leo unampiga ndugu yako au unamwendea kinyume ndugu yako unamfanyia machafu ndugu yako ni kwa sababu ya siasa. Ni nini

kwani tunatafuta, tunatafuta maendeleo ya nchi hii. Ukisimama wewe CCM unapiga kelele natafuta maendeleo na akisimama CUF anapiga kelele anatafuta maendeleo na ni maendeleo ya nani ni ya Wazanzibari. Sasa leo kwa nini tutofautiane kupita kiasi.

Mhe. Spika, mimi ninasema mswada huu umekuja kuikomboa Zanzibar ili irudishe ile Zanzibar njema atakae aje. Siti biti Sadi aliyeimba nyimbo hii hakuwa ana wazimu. Alikuwa kaiimba hii nyimbo kwa kujua anafanya nini na anasema nini. Sisi toka hapo tunapendana ni ndugu na ndio maana mtu akaweza kuimba nyimbo kama hiyo. Anayetaka na aje kwa sababu sisi ni visiwa, kwa hivyo watu wanaingia na kutoka hapa na kwa sababu tulikuwa ni watu wa huruma, Mwenyezi Mungu katupa imani alikuwa hakatazwi mtu kuja. Kwa hivyo, sisi tunataka kuiondoa hapa kwa sababu ya siasa na ambapo siasa haitupeleki huko.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nina mashauri mawili au matatu madogo tu. Ushauri wangu wa kwanza ni vitambulisho na vyeti vya kuzaliwa ni muhimu kupewa Wazanzibari wote. Kwa sababu kuna Wazanzibari hawana vyeti vya kuzaliwa. Mimi nina mwanangu mwenyewe hana cheti cha kuzaliwa kwa sababu kimepotea nakwenda nikirudi mpaka nimeshaambiwa hakuna karatasi za kufanyia vyeti na sasa hivi ana umri wa miaka 18 hawezi kupata kitambulisho. Kwa hivyo, jamani hili tulifanye liwe ni rahisi kwa Wazanzibari ili tuwajengee misingi mizuri watoto wetu huko tunakokwenda tunawadhulumu, tusiwadhulumu haki zao.

Lakini la pili Mhe. Spika, mimi naomba jamani tusisikilize fitina. Penye zuri lolote hapakosi fitina, fitina wapo na wanafanya kazi za kifitina kuwachonganisha Wazanzibari tusikae pamoja ati wakatae huu mswada. Wengine wanaambiwa mkiukubali mswada basi CCM imekwisha. Lakini mimi nataka niwaambie ndugu zangu wa CCM kwamba CCM haitokwisha kwa mswada huu, CCM itaimarika kwa mswada huu, CUF itaimarika kwa mswada huu kwa sababu wanawatafutia mema Wazanzibari waliochoka kukosa maendeleo, waliochoka kupigwa kila ukifika wakati wa uchaguzi.

Mhe Spika, huyu fitina mbaya kaimbwa mpaka na nyimbo za taarabu, lakini kwa sababu naumwa ningekuimbieni kidogo. Fitina mbaya hana haya na wapo waliokuwa mafitina. Sasa mimi nataka niwaambie hili jambo limeletwa na Mwenyezi Mungu, kwa hivyo wamuogope Mwenyezi Mungu, ikiwa yumo humu humu Barazani, ikiwa nje ya Baraza, ikiwa kiongozi au ikiwa raia. Lakini mimi nafikiri raia hawezi kufanya haya kama sisi viongozi hatujafanya hivi, ni kuwa tunawapitia raia wetu na tunawaambia mipango isiyokuwa na mpango. Kwa hivyo, tujitahidi kabisa kusema na wananchi wetu wakubali hili ili tuweze kukaa pamoja, tunafarikiana kwa nini.

Mhe. Spika, tupo sisi tulikuwemo ndani ya Baraza, lakini pia kuna vyama vingine vidogo vidogo, tafadhali tukubaliane sote tukae na wananchi wetu au tukae na raia wa Zanzibar kulikubali hili la mswada ili tuweze kufanya serikali ya pamoja ya umoja wa kitaifa. Kwa sababu hivi sasa tukijitizama sisi wenyewe huku kukosa na kupata tuko namna gani, hakuna aliyemzidi mwenziwe sana. Tunajua na tunaona. Kwa nini sasa tusikae pamoja tukajenga nchi yetu na tukafanya serikali ya umoja na tukaweza kujenga nchi yetu, ili wakapata maendeleo watu wetu na watoto wetu na vizazi vyetu vijavyo ambapo wao ndio watakwenda kutushtaki kwa Mwenyezi Mungu, kwamba sisi tumeondoka hapa na tumewaacha katika matatizo makubwa sana ya kugombana ndugu kwa ndugu.

Mhe. Spika, mimi nafikiri hawa ambao waliobeza huu mswada au waliobeza hili jambo tuwafanye kama yule mwanamke mwenye wivu. Mhe. Spika, mwanamke mwenye wivu alikuwa na mke mwenziwe, sasa mke mwenziwe kafa, akapita njiani na wenziwe akasema aah! Kaburi lile zuri. Mwenziwe akamwambia unalijua ni la nani lile, akaambiwa ni la mke mwenzio, akasema ndio maana limekwenda upande eti. Kwa hivyo, na hawa wanaobeza huu mswada ndio hao wenye wivu wa kike. Kwa sababu hakuna sababu. Una nini mswada.

Mhe. Spika, tulipitisha hapa hoja sote kwa pamoja, tukarudi. Waheshimiwa Mawaziri wamekuja hapa wametuambia maneno mazuri, wenyeviti wamesema maneno mazuri. Kwa hivyo, sisi hawa tuwaache kama walivyo, tuwafanye kama yale madebe shinda hayaachi kutika yatike huko nje. Sisi kama viongozi tuchukuwe juhudi kwenda kwa wananchi wetu kuwapa nafasi yao ya kutoa maoni yao na tuyasikilize maoni yao yanasemaje, tena nina hakika kwamba maoni mengi yatakuwa ndio na wala sio hapana, kwa sababu watu wetu wamechoka na mambo haya.

Mhe. Spika, siku moja kwangu alikuja mgeni ambaye anatoka South Africa, alikuja na mwanangu ambaye ni rafiki yake. Siku hiyo ilikuwa ni moja miongoni mwa siku ya kampeni za uchaguzi. Sasa kwangu kule upande wa Magogoni mabomu huwa mengi na risasi zinalia sana, wakati wanatoka kwenda kusubiri daladala basi yalipigwa mabomu na walirudi mbio nyumbani.

Kutokana na hali hiyo, yule mzungu alisema kumbe nyinyi mnaishi namna kama hii Zanzibar, kuna kitu gani mpaka watu wanapigwa mabomu ya machozi wakati wanatoka kwenye kampeni. Kwa hivyo, nilimwambia kwa sababu hatufahamu nini tunafanya ndio maana tuko hivi, basi nilimwambia wewe tulia na mabomu haya yatakwisha hewa ya pilipili na baadaye utaondoka. Mhe. Spika, alisema kesho nakwenda nyumbani mpaka wishe uchaguzi ndio nitakuja tena.

Sasa tunafanya nini wakati nchi hii ni yetu sote na kilichokuwemo humu ni chetu sote. Kwa hivyo, tufanye kitu cha maslahi ya watu wetu, ili tufanikiwe.

Mhe. Spika, naona nikisema sana nitayaharibu matamu yaliyozungumzwa. Isipokuwa na mimi ushauri wangu kwamba, tuwaachie mafitina na fitina zao na Mwenyezi Mungu atawaalani na tuyaachie madebeshinda yatike nje na sisi tufanyekazi zetu kama alivyotuamrisha Mwenyezi Mungu.

Kwa sababu bila ya Mwenyezi Mungu haya yasingekuja, lakini Mwenyezi Mungu aliwaona waja wake kwamba wameshachoka, sasa ametupa njia kupitia Maalim Seif Sharif Hamad na Mhe. Rais Amani Abeid Karume, ili wakae na wakubaliane na sisi tuweze kufanya mambo yetu bila ya matatizo. Kwa hiyo, tumshukuru Mwenyezi Mungu na kila tukikaa kusali rakaateini kwa ajili ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kutupa salama. Amin.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kama wenzangu wa CCM walivyozoea. Ahsante sana *(Makofi)*.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi: Mhe. Spika, na mimi kama wenzangu naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii japo kuwa mwanzo ulitaja jina silo la mtu ambaye hayupo kumbe ndio mimi na ulisema Abdallah Juma Khamis. Mhe. Spika, ndio mimi na nipo naomba kukushukuru sana.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, mimi nimejifahamu kwamba nilisema Abdallah Mwinyi Khamis *(Kicheko)*.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi: Mhe. Spika, ninashaka na masikio yangu *(Kicheko)*.

Mhe. Spika, na mimi kabla sijasahau naunga mkono haya yote kwa asilimia mia moja, pia napenda kuithamini michango yote iliyotolewa na wenzangu. Vile vile napenda kuuthamini mchango wa Mhe. Haji Omar Kheir ambao umetaka kumtoa machozi mjumbe mmoja wa upande wa Upinzani *(Makofi)*.

Kwa sababu machozi nayasababishwa na *emotion*, wakati unapoambiwa kitu na kikakuingia kuna kitu kinaitwa *emotion* kinakupanda na hiyo inakwenda kwenye *tear gland* na ku-*irritate*, sasa wengine huwa *irritate* kwa *Tauhid* au mapenzi ama kwa mfano, mimi bado kidogo nikote machozi kwa maneno waliyosema Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba *(Kicheko/Makofi)*.

Lakini nathibitisha kwamba hao wote nawapenda na maneno yao yalikuwa mazito na sauti ilikuwa muafaka. Kwa mfano, sauti ya Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba ilikuwa imekaribiana na Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ambaye anamuiga Fidel Castro, yaani zinaingiliana zilikuwa na nguvu sana. Kwa hivyo, naunga mkono yote na ninathamini yote yaliyotolewa *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika, kilichotokea nini mpaka ukaja mswada huu nadhani turudi nyuma kidogo. Nitatoa mfano mmoja kwamba na mimi nimepata bahati sana ya kusomeshwa na *Afro Shirazi Party* na CCM, tena nimesafiri sana bila ya kiasi na nimekwenda sehemu nyingi sana na nimejua humo nilimokwenda kwamba Mzanzibari ni mtu muhimu. Kwa sababu heshima zetu wakati tunapokwenda kule tunatofautiana sana na watu wengine, yaani tunakuwa na heshima sana na tunapendwa kwa sababu ya heshima zetu.

Nilikwenda pahala pagumu sana wakati nilipokuwa nikishughulikia masuala ya michezo. Mhe. Spika, nilikwenda pahala na nilitaka kuonana na *Football Association of England* ni mtu mgumu sana kuonana naye na nilipelekwa na nilipelekwa na Kampuni ya *Meter Sports* ambayo ni kubwa inajulikana na ilikuwa ikitoa mipira yote ya *F.A.*

Mhe. Spika, nilikwenda pale na kufika kwa *secretary* wake mwanamke *alhamdulillah* kidogo halati, basi nilipokwenda pale na mwenyeji wangu akaniambia utajitambulisha na kuomba mwenyewe kwa sababu hatukuleta habari mapema. Kwa hivyo, nilikwenda kwa ajili ya kutaka kuonana naye, basi yule bibi aliniambia *is very difficult*, isipokuwa ungeleta habari kutoka Zanzibar kabla ya kufika hapa, lakini tutakufikiria nadhani haiwezi kuwa.

Mhe. Spika, mzungu akikwambia hivyo kwamba atakufikiria maana yake hupati. Kwa kweli mimi sikuwa na kitu isipokuwa nilikuwa na kipaki cha karafuu nikampa na nikamwambia hii zawadi yako chukua, maana nilikusudia wewe nikupe zawadi na Croca nimpe zawadi, basi ali-*appreciate* baada ya kumpa kile kipakti cha karafuu kama aliyepewa donge la dhahabu. Kutokana na hali hiyo aliniambia kwamba '*I think you can come tomorrow?" (Kicheko/Makofi)*.

Kwa kweli hiyo inadhihirisha kwamba Wazanzibari ni *very manipulate*, yaani lugha zao zina-*manipulate* watu pamoja na kuwafanya watu watamani na kutaka. Kwa hivyo, nimepata kuonana na huyu Croca kwa kipakti cha karafuu na ulimi wangu mtamu ambao umefundishwa na *Afro Shirazi Part*, CCM, mama pamoja na baba yangu *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika, nilipokwenda kule nimestaajabu nimekiona kibao juu ya meza yake huyu Croca ambacho kimeandikwa *think* lakini kwa dhahabu, yaani kibao na zile hati za dhahabu pembeni kimekaa. Kwa hivyo, tukaulizana hali na kuzungumza mambo mbali mbali na vile vile nikalipa *fee* ya *Football Association*, kwa sababu sisi ni *Member* wa *F.A*, lakini nadhani wenyewe Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo hawaitaki sana, lakini ni *member* na wala hatuzitumii *facilities* zao mpaka leo *member* sisi.

Baada ya kumaliza mazungumzo yetu basi mwisho nilimuuliza hiki kibao kilichoandikwa *think* maana yake nini? Kwa kweli aliniambia binadamu anatarajiwa kuna wakati akae na kufikiri, yaani atokane na matatizo yake, mambo ya ulimwengu na afikiri mwenyewe tu, basi alinifahamisha mpaka nikafahamu.

Kwa hiyo, baada ya kunifahamisha na kufahamu nikaona ile ku-*think* ni kutulia na kama unaletewa Ilhamu, kwa sababu ukifikiri huwezi kuwa kichwa chako kitupu. Kwa mfano, baada ya njaa, unataka fedha, kura, jimbo pamoja na mambo mengine, basi unapata wakati unafikiri na kichwa chako kinakuwa kitupu inakuwa kama unaletewa Ilhamu.

Mhe. Spika, watu hawa wawili Mhe. Amani Abeid Karume na Maalim Seif Sharif Hamad wame-*think* na wameletewa Ilhamu na ndio maana wakafanya kukutana *no matter* nani kwenda kwa nani, lakini Ilhamu imewakutanisha. Hii imetokana na *theory* gani, kwa sababu kuna *theory* inayosema *enough is enough* na kwa Lugha ya Kiswahili lazima utumie lugha nyepesi kwa kusema si basi tena na ukitumia lugha ya amri siyo *(Kicheko/Makofi)*.

Nyengine ipo *Theory* ya Biashara na watu wa biashara wanaitumia sana "*If you can't win him join him*" na huo ni ustaarabu wa hali ya juu sana na wala hafanyi mtu isipokuwa awe mstaarabu wa hali ya juu. Lakini mtu *crock and rogue* na mwenye kutaka ubinafsi hafanyi abadani.

Kwa mfano, wewe unauza mafriji mabovu na mwenzio anauza mafriji mabovu, watu wote wanakwenda kwake kwa sababu lafdhi yake nzuri mzungumzaji wa watu na yako hayatoki isipokuwa yanaota kutu. Kwa nini watu wote wanakwenda pale, *I can't win him I must join him*.

Sasa ukichukua mafriji yako na kwenda kwake yeye na kumwambia kwa nini hatuuzi pamoja na yule *gntalemen* akikubali basi biashara itakwenda vizuri sana na mafriji yatatoka. Sababu yake nini? Ni kwamba umeamini kuwa huwezi, yaani *I can't win him and I must join him*. Huu ni ustaarabu wa hali ya juu na wala hafanyi mtu mwenye tamaa ya binafsi *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kama tulivyoona nusura imemletea matatizo kidogo, yaani siku aliyotamka tu kwamba tumeamua kumtambua imetaka kumletea matatizo kidogo watu walilia na mambo mengine, kwa sababu ni ngumu sana. Lakini kaiweza na *alhamdulillahh* imekuja *(Makofi)*.

Lakini katika haya Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Amani Abeid Karume alisema tena kwa sauti ya kujiamini, kwamba katika haya hakuna mshindi na aliyeshindwa, yaani sote ni washindi kwa sababu tunataka maslahi ya nchi hii na ile ilikuwa ni nzuri sana ya kumuunga mkono Maalim Seif Sharif Hamad. Kwa hiyo, kama mwanzo alifahamika kuwa ni ameshindwa, lakini ilimuunga mkono na kuonekana kwamba na yeye ni mshindi na sote tunashinda pamoja Sasa hii *theory* ya *enough is enough* na ile ya *If you can't win him join him* zimesaidia sana. *(Makofi)*.

Mhe. Spika, nyengine ili iliyosaidia kuna msemo unaosema hivi "Mtaka cha mvunguni sharti ainame". Kwa hiyo, wote hawa wawili wametaka cha mvunguni na lazima wainame, ndio hii kukubaliana. Wametaka nini? Wametaka amani, salama pamoja na utulivu, ambayo *originality* yetu sisi ni amani, salamu na utulivu *(Makofi)*.

Mhe. Spika, nimesahau hapa kuleta picha moja hapa ambayo ni nzuri sana na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali angeonesha yake na mimi nikaonesha yangu, lakini si yangu mimi. Kuna picha moja imepiga Msikiti, Kanisa, *Temple* na nyumba zote za dini 1963, yaani tumepata sifa sisi kwa Wakoloni kwamba hatuna ubaguzi wa dini na ile *stamp* imeitwa *Zanzibar Religious Tolerance*.

Hivi kipo kinachouma sana kuliko *religion*, lakini tulikuwa na *Religious Tolerance from time memorial*, yaani kabla ya wakati wa Wakoloni na hao Wakoloni kufika kwamba hapa kuna *Religious Tolerance* ambacho ni kitu kikubwa sana. Kwa hivyo, hapa kimepita nini? Kimepita kitu kinachoitwa mtaka cha mvunguni sharti uiname. Kwa maana hiyo, sote tumekitaka cha mvunguni na tumeinama.

Siku hizi wanasema kwamba vitanda vya sasa haviinamiki kwa sababu vya mabao, lakini ile ilikusudiwa kitanda cha samadari na *theory* ipo pale pale mtaka cha mvunguni sharti ainame *(Makofi)*.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nililisema mwaka wangu wa mwanzo nilipochaguliwa kuwa Mkuu wa Mkoa katika Uwanja wa Amani nilisema hivi, kwamba Marekani kuna sehemu inaitwa California na imepandwa miti mingi sana ya mbao na kati ya ule mwitu umepita mto ambao unatiririka.

Sasa Wamarekani wametengeneza ule mto na wanautumia wakati wanapokata mbao wanazitia kwenye ule mto na unakwenda mpaka kwenye Kiwanda cha Msumeno. Katika hali hiyo wamefanya usemi wenyewe Wamarekani na kusema kwamba, "*Don't be like a log driven with other logs to ward the sawmill*".

Mhe. Spika, niliisema hiyo katika Sherehe za *May Day* Uwanja wa Amani na iliwafurahisha watu wengi sana na wakati huo niliwafurahisha CUF na CCM. Jamani tusiwe *logs* sisi tukawa *driven* katika mto tunajijua tunakwenda kwenye *sawmill*, tunakwenda tu.

Kwa kweli haifai kwa sababu ile ni mizigo na sisi ni watu kwa hivyo tukijiona tunakwenda kwenye *sawmill*, basi tupige *fullstop* na hii ndiyo *fullstop* ya kwenda kwenye *sawmill*, maana yake hatima yake isingekuwa nzuri *(Makofi)*.

Mhe. Spika, pamoja na matatizo hayo tulikuwa tunayo amani sote tokea *January, February, March, April come October* basi inakuwa ni msimu kama maua yamekuja wadudu wa kepu hao, yaani miembe ikitoa maua basi ndio msimu wa wadudu wa kepu na kila mmoja anahofu ya wadudu wa kepu.

Kwa kweli inapofika *October* basi roho kila mmoja si yake na wala hatujuani na mambo mengine mbali mbali. Kwa hivyo, mswada huu unapita na *inshaallah* ukeshapita basi amani ya kudumu itakuwepo, watu watapendana na tutarudi katika hali ile kama tulivyo sasa *(Makofi)*.

Lakini nini chengine kilichopo sisi tunayafahamu hayo, basi na watu wayafahamu hayo, kwa sababu kufahamu sisi na kupitisha mswada bado haijawa. Kwa maana hiyo, watu wetu wafahamu vizuri na tayari watu wameshafahamu, na tusichukulie kwamba watu wote wafahamu kama watu wa Mjini Magharibi kwamba wote *Form VI*. Aaa! Wapo watu wengine jambo hili hawajalifahamu na akili zao ziko tayari *consume* unachowapelekea. Kwa hivyo, tukipeleka uzuri basi wallahi watu watafahamu.

Mhe. Spika, nataka kutoa mfano kwamba kuna watu hawafahamu na utastaajabu kwa nini hawafahamu. Mhe. Spika, nataka utikise kichwa kidogo na halafu nitoe mfano, umeitikia ahsante *(Kicheko/Makofi)*.

Kwa kweli watu hawafahamu. Kwa mfano, mimi nilikuwa na marehemu dada yangu amesoma juzuu zote amemaliza, lakini kusoma *Quraan* na Lugha ya Kiarabu ni vitu viwili tofauti. Sasa jinsi watu walivyokuwa hawafahamu ndio natoa mfano huu.

Kuwa na Nyimbo ambayo alikuwa akiimba Moh'd Abdulwahab na ilipendwa sana na watu mpaka Makaarii wa *Quraan*, kwa sababu mlikuwa na mifano kama ya *Quraan* na mimi alinileta rafiki yangu marehemu Wajihi, lakini alikuwa nayo marehemu Sheikh Said Hassan muda mwingi akisikiliza aliletewa kutoka Cairo.

Mhe. Spika, naomba kunukuu hiyo nyimbo kwa ruhusa yako, kwa sababu mimi naweza kuimba sio kama Mhe. Aziza Nabahan Suleiman. Hiyo nyimbo aliyokuwa akiimba Abdulwahab kuna sehemu inasema hizi "…*laa laa laa laksidi inni raaitukumma amaa*, *ini samiitukuma amaa* …" Maana yake usinisute nimekuoneni, nimekusikieni, ainaini fiainai, macho yake na macho yako.

Sasa palipochekesha wapi, kwamba dada yangu akenda Uzini anasema yule Abdallah kila nikenda mjini nyimbo yake inatukana tu. Kweli juzuu thalathini amesoma na Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora anamjua dada yangu Zaituni, basi akenda kunitangazia. Kwa hivyo, nikaitwa na kuulizwa nyimbo gani unapiga wakati anapokuja dada yako, mimi ninasema siijui, kumbe vile kile kipande kinachosema ini raaitukuma amaa na ini samiitukumma amaa, maana yake nimekuoneni na mimekusikieni *(Kicheko/Makofi).*

Mhe. Spika, huu ni mfano wa mtu unayemtaraji kwamba afahamu, lakini hafahamu na anahitaji kufahamishwa na wala tusichukulie kila mtu anafahamu *is not easy*. Kwa kweli dada yangu amemaliza juzuu thalathini ini raaitukumma haijui, maana yake nimekuoneni na samiitukuma, maana yake nimekusikieni. Nyimbo yenyewe ilikuwa ni kuhusu fumanizi.

Kweli hao ni watu mfano wanafahamu kila kitu tena wajuzi na mimi amenilea na kunifundisha busara, lakini hiyo imemshinda.

Mwalimu mmoja na kuonesha mfano hata mwalimu anakuwa hafahamu, amewachukua wanafunzi wake katika ufinyanzi. Kwa mfano, sisi tunafinyanga vyungu, vyetezo na wengine wanakuwa wanafinyanga vitu hivi na vile. Sasa mwalimu wa ufinyanzi waliwachukua wanafunzi wake katika sanamu kubwa lililofinyangwa na pahala hapo panawekwa masanamu tu na wala sio kwenye *public*.

Kwa hivyo, sanamu lile lilikuwa ambalo ni jipya, basi mwalimu akawaambia anataka mwende na mlitizame sanamu lile na kila mmoja a-*note down* yule mfinyanzi nini amekifanya uzuri na kipi amekikosea. Wanafunzi wale wakenda na kulizunguka lile sanamu limekaa kama lilivyozaliwa na ku-*note down* kila kitu tena wako *seriuos* lakini hawakukunja uso, mwisho wakarudi darasani.

Mhe. Spika, hapa natoa mfano, wakati mwengine hawa walimu hawafahamu au sisi inawezekana hatufahamu tupo tunapiga makofi, lakini hatufahamu na tukashindwa kufahamika si ndio walimu basi ndio sisi.

Kwa hiyo, baada ya kurudi darasani, mwalimu akaanza haya nataka mniambie nini amekifanya uzuri na kipi amkifanya vibaya mfinyanzi yule. Mmoja akanyanyua mkono, akaulizwa nini amekifanya uzuri, alisema ile sehemu ya paya ameitia udongo laini, mwalimu akamwambia toka mchimvi. *(Kicheko/Makofi)*

Wapili akasema, nimehisi pale kwenye kifua amefanya vizuri, lakini kuna pahala alikuwa atie kidoto, mwalimu akamwambia toka mchimvi. Watatu akasema, nimemuangalia mgongoni, lakini yule mtu hakunenepa na wala hakutiwa *rabbis* hakutiwa kwenye mgongo mpaka kwenye mteremko. Wanne akamwambia mimi natoka mwenyewe kabla sijasema *(Kicheko/Makofi)*.

Judgment iliyokuja kumbe mchimvi alikuwa ni mwalimu na yule mtoto aliyesema kwamba natoka mwenyewe ndiye alikuwa na *IQ* kubwa na kusema kama hawa wametaja haya na wametolewa, basi mimi natoka mwenyewe kabisa, sasa Mhe. Spika alikuwa ataje nini na hiyo tutazungumza baadaye *(Kicheko/Makofi)*.

Lakini tunachokipitisha hapa ni kwamba tunataka jamii inayokuja iishi kwa salama na huu utamu uliofanyika katika awamu ya sita juu ya matatizo yetu. kwa mfano, barabara zote kuwa nzuri pamoja na kila kitu Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Amani Abeid Karume ameweka vizuri, basi wanatakiwa watu waje waiendeleze na wala hatuwezi kuiendeleza mpaka iwepo amani pamoja na masikilizano ya kutosha *(Makofi)*.

Mhe. Spika, mwisho napenda kusema kwamba Waingereza wamesema kwamba "*Uneasy leas head that way the crown*". *We are wearing the crown* sisi ndio wakubwa ambao tumevaa *crown and our head become always uneasy*. Kwa hivyo, linalotokezea jambo ambalo linataka kukabiliwa kwa mafahamisho basi sote tuwe *serious* na tulifahamishe linavyotakiwa na wala tusigeuke yule mwalimu kumbe mchimvi yeye anayewasingizia wanafunzi wake. Mhe. Spika, naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja *(Makofi)*.

Mhe. Zahra Ali Hamad: Mhe. Spika, nakushukuru naamini nitaheshimu dakika ambazo nimeomba na kwa sababu mimi ni mjumbe wa kamati, basi ni mengi ambayo nilichangia kwenye kamati. Sasa hili ambalo nataka kuchangia nisingekuwa na uwezo wa kulitia kwenye mswada wala marekebisho yenyewe ya mswada wenyewe ndio maana nimeomba dakika saba kwa ajili ya kuchangia.

Mhe. Spika, yanetosha ambayo wamezungumza wenzangu. Lakini kama ni mwanamke wa nchi hii pamoja na watoto ndio ambao tunashuhudia au tunaathirika kwa kiasi kikubwa sana kufeli kwa siasa zetu za Zanzibar. Kutokana na hali hiyo, nimeona sitowatendea haki wanawake wenzangu ambao wamenileta hapa ikiwa sikuwasemea lolote katika jambo hili muhimu *(Makofi)*.

Kwa kweli tumeathirika sana wanawake kwa siasa za Zanzibar. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora jana nilimsikia akisema kutokana na kufeli kwetu kwa siasa zetu basi baada ya uchaguzi wengi huwa wanaomba hifadhi na kukimbilia shimoni na sehemu nyengine.

Mhe. Spika, suala hili ni kweli, lakini shimo linaloingia mwanamke na mwanamme ni shimo na guruguru tu, ndilo ambalo mwanamke na mwanamme huingia na wakati vinapotokezea vishindo basi yule mwanamme akamuuliza yule mwanamke kuna nini huko juu *(Kicheko/Makofi)*.

Lakini Shimoni hili la Mombasa ambalo watu wanakimbilia baada ya uchaguzi ni shimo ambalo wanaingia hao wanaume tu, sisi wanawake hubakia huku nyuma na watoto tena athari zote zinazotokea basi huwa sisi ndio tunaozikabili kwa sababu hatuna pakukimbilia Mhe. Spika. kwa mfano, utaondoka vipi wakati watoto 10 au 7 wapo wanakutizama wewe na kukufuata, basi huwezi kwenda *(Makofi)*.

Mhe. Spika, siku zote hapa tunapokaa kwenye Baraza lako tunaomba dua na naomba ninukuu harahara kwa ajili ya kuwakumbusha wenzangu dhamana tuliyonayo, yaani huwa tunaomba dua ya kuitakia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sehemu moja inasema hivi; “Uibariki Zanzibar iwe nchi ya Amani na wote wanaoishi humo wawe na upendo halisi na umoja, utuepushe na tamaa mbaya, chuki na ubinafsi na utulinde na maadui wanaoitizama Serikali ya Mapinduzi kwa jicho la husuda”.

Vile vile kuna ile ambayo tunaomba kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi inayosema hivi: “Tunakuomba kwa unyenyekevu utupe hekima na busara sisi waja wako tuliokusanyika hapa tukiwa Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi la Wananchi wa Zanzibar, utuongoze daima katika kujadili mambo yetu yanayoletwa mbele yetu, ili tuweze kushinda matatizo yetu kwa manufaa na ustawi wa nchi hii pamoja na watu wake” *(Makofi)*.

Mhe. Spika, mswada huu uliopo mbele yetu ndio unalenga katika hii dua ambayo wewe mwenyewe unaiomba kila siku. Kwa sababu adui Mhe. Spika hawezi kuingia ndani ya nyumba ikiwa sisi wenyewe tuko imara tumeshirikiana, isipokuwa nyumba lege lege ndio anayoingia adui, lakini nyumba imara hawezi kuingia adui.

Kwa hivyo, ni lazima kama viongozi sisi basi tujilinde na ubinafsi na tutizame lile ambalo limetuleta hapa kwa maslahi ya wananchi wetu waliotuleta pamoja na taifa kwa jumla.

Mswada huu unalenga mambo mazuri na katika draft ya kwanza kabla ya marekebisho ya kamati nilisema kwenye ufafanuzi maana ya Kura ya Maoni, kwamba ni utaratibu wa kupeleka suala la hoja ya kisiasa. Kwa hivyo, tukaona hapana nchi kama Zanzibar si tatizo la kisiasa tu, ijapokuwa kwa hivi sasa tatizo ambalo tunalo kubwa ni la kisiasa, lakini inaweza kutokezea baadaye tukawa na matatizo mengine.

Kwa maana hiyo, huu ni mswada ambao tunaekelea kuwa ni sheria. Kwa mfano, kuna masuala ya kiuchumi pamoja na yale ya kijamii na wakati mwengine kuna haja ya kuyapeleka kwenye Kura ya Maoni, lakini tukasikia sauti ya wananchi. Kwa sababu siku zote sauti ya watu tunaambiwa kwamba ni sauti ya Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, naona unaangalia muda, kwa hivyo naomba Wajumbe wa Baraza hili tukufu na nitashangaa sana kwamba mswada huu ni wetu na sisi ndio ambao tumeleta hoja na tukauunga mkono sote kwa kusema ni
ndio. Sasa leo aje atokee mtu apige basi itakuwa ni sawa na uuchukua ulimi wetu na kuutia ndani ya pua yetu. Vile vile wale waliotuleta hapa kwa kweli watatuona si viongozi barabara kwa sababu lile ambalo tunalisema kumbe hatuliamini ndani ya nafsi zetu.

Mhe. Spika, wapo wanaosema kwamba mswada huu ni Rais Amani Abeid Karume na Maalim Seif Sharif Hamad na Rais Amani ameshamaliza muda wake na anataka atuachie mambo ambayo hatuyapendi. Kweli anamaliza muda wake tukijaaliwa na inshaallah atamjaalia atamaliza muda wake kwa salama *(Makofi)*.

Lakini anawatakia wenzake mazuri na ndio maana hataki lile lililomkuta yeye na wenzake walionje, kwamba anawaekea njia safi. Kwa hivyo, jamani kama viongozi naomba tulichukue hili ni leo kwa maslahi ya nchi yetu pamoja na wale waliotuleta hapa. Kwa maana hiyo, tuwaunga mkono viongozi wetu wanatutakia maslahi ndani ya nchi hii *(Makofi)*.

Mhe. Spika, ahsante sana, inawezekana tutimize wajibu wetu sote *(Makofi)*.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu na kuchangia mswada huu wa Sheria ya Kura ya Maoni.

Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi pamoja na watendaji wake wote, ambapo walikaa na kufikiria juu ya kuuleta mswada huu ambao ni muhimu, hasa tukiangalia kwamba amani ni wito wa Kiislamu, pia ni maendeleo pamoja na utulivu *(Makofi)*.

Kwanza niishukuru serikali kwa kufikiria juu ya mswada huu ambapo Kura ya Maoni ndio itakuwa ushahidi tosha kwa wananchi kwa maoni yao kwamba yataheshimiwa kwa matokeo yoyote ambayo yatatokea.

Lakini napenda kusema kwamba Mfumo wa Vyama Vingi katika nchi yetu ulianza kwa kufanywa Kura ya Maoni mbali mbali kwa wananchi na matokeo yake yalivyotokea, ambapo tuliambiwa kwamba asilimia 80 ya Watanzania walikataa na asilimia 20 ndio waliokubali.

Kwa wakati huo tuliambiwa kwamba tunaelekea kwenye mwelekeo mwengine na yaheshimiwe haya matokeo ya asilimia 20 ndiyo yaliyotukuta leo katika mfumo huu tunaendelea nao, tulikukwa katika mfumo wa vyama vingi lakini kumbe naweza kusema wengi wape ambao hawakupewa ndio imetuletea leo kurudia katika mambo haya ambayo tunaanza leo na *inshallah* kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu labda yatafanikiwa na namuomba yafanikiwe ili kuleta nzuri katika nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi ushauri wangu kutoka mwaka 1995 tumeanzia katika mfumo wa vyama vingi katika Baraza hili na kwa bahati mimi kipindi hicho nipo hapa. Hapa palifanyika mikutano mbali mbali ya kutafuta amani na umoja basi yalishindikana. Lakini mwaka 2000 hivyo hivyo tulikwenda mpaka dakika ya mwisho mambo yakaharibika, lakini mwaka 2005 mpaka hivi karibuni tuliendelea na hayo hayo kwa kauli ya Chama cha CUF walithubutu kusema kwamba hawatokaa meza moja na CCM hasa baada ya kuja mswada ambao azimio hili lipelekwe kwa wananchi ili waliamua wao.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri naweza kusema Mwenyezi Mungu mtu kama amepotea anaweza kumrudisha katika anga za pepo kama atajikosoa, baada ya kukaa viongozi hao wa juu wa CUF walikubali yale matakwa yote ya azimio lilotoka katika Chama cha Mapinduzi kwamba wananchi waamue wenyewe kwa maslahi ya nchi yao. Mhe. Spika, agizo hilo ndio lilosemwa na bahati nzuri Maalim Seif katika kumuendea Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyatamka hayo yote, akakubali, akaelekeza kwamba niko tayari. Mhe. Spika, mimi ombi langu kwa kuwa kauli hii njema aliyoitoa isijetokea hii miaka ya nyuma yaliyotokea. Kwa hivyo, naomba awe na kauli thabiti na Mwenyezi Mungu amtoe katika kundi lile gumu ambalo alikuwa nalo wakati huo amuelekeze huko tunakotaka kuunda umoja.

Mhe. Spika, kura ya maoni ni uchaguzi na ni matokeo ambayo yanakubalika kisheria. Mimi nataka niseme kwamba naomba matokeo yatakayotoka hapa yahishimiwe. Matokeo yatakayotoka hapa yasijekuwa na utata kwa sababu tumeona katika ulimwengu wetu huu tuliokuwa nao. Kuna hata mataifa makubwa wanapigana mpaka Iraq hivi juzi wamekwenda kwenye uchaguzi kwa mara ya kwanza lakini matokeo chama tawala kikashindwa mfano kwa viti viwili, basi kiongozi aliyekuwepo madarakani anasema hakubaliani nalo.

Kwa hivyo, madhumuni yangu mimi kusema hivyo isijekuwa wananchi asilimia 80 wamesema hivi na asilimia 40 wamesema hivi wakaambia ata tuache huku twende huku. Mimi naomba kura ya maoni ndio muamuzi na matokeo yaheshimiwe.

Mhe. Spika, jengine nitalolisema hapa mimi nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tokea kuwa Rais mwaka 2000 hadi kufikia leo adhma yake na madhumuni yake wananchi wa Zanzibar ni kuwaweka sawa. Hata tukiangalia katika maendeleo ya nchi hii sisi wajumbe wa kamati zako

Mhe. Spika tunatembelea katika miradi ya maendeleo utashangaa matokeo tunayoyaona kwa upande wa Unguja tofauti sana na upande wa Pemba. Kwa sababu watu wamekubaliana kufanya kazi na kuendeleza miradi ya maendeleo mbali mbali katika sehemu zao. Kwa hivyo, mimi nataka niseme kwamba faida kubwa ya umoja na faida kubwa ambayo italeta amani na utulivu katika nchi yetu ni kuleta maendeleo kwa umoja huo tunaotegemea.

Mhe. Spika, pamoja na juhudi hiyo nzuri narudia tena kusema kwamba taaluma kwa wananchi wetu waelimishwe, waelewe na tunapokwenda kwa wananchi wetu tusiwatumie vitisho. Mhe. Spika, mwananchi ana uhuru wa kutoa maoni yake, mwananchi ana uwezo wa kutoa ushauri wake na tuusikilize una mwelekeo mdogo tuelekezane mpaka ufanikiwe. Kwa hivyo, ningeomba sana haya yafanyike lakini juhudi ya Mhe. Rais isiachiwe ikapotea kwa sababu tunategemea kwamba katika dunia yoyote na hali halisi ya nchi tegemeo kubwa ni amani na utulivu katika nchi.

Mhe. Spika, hata katika nyumba yako kwa mfano hakuna maelewano basi tija haiji katika nyumba kwa sababu tumezaa watoto wanataka kulelewa pamoja, wawekwe pamoja lakini pakiwa na mfarakano mmoja kati yetu basi chuki na uhasama utakuja mpaka kwa vizazi vyao. Kwa hivyo, mimi ningeomba sana hili liendelezwe kwa manufaa ya nchi yetu hasa tukiangalia kwamba wakati umefika tutokane na siasa za chuki, fitna na mambo mbali mbali.

Mhe. Spika, Mhe. Tindwa ameeleza maneno makubwa sana na kama ulivyosema ingelikuwa ndiye mchangiaji wa mwisho ingekuwa basi, lakini mimi namuunga mkono kwa asilimia kubwa kwa sababu nategemea na mimi huko nyuma ninakotoka tulikuwa jeshini wote.

Mhe. Spika, katika maisha ya kibinadamu hakuna mtu anayepata shida kuliko askari na mimi katika maisha yangu yote anayemchukia askari wa aina yoyote basi sina imani naye. Kwa sababu askari ni mtu ambaye amejitolea nafsi yake kulinda taifa lake, askari analinda rasilimali za serikali na mambo mengineyo. Lakini kwa bahati mbaya kuna watu askari wetu hawawafahamu na hawajui shida zao.

Kwa hivyo, mimi ningeomba sana pamoja na juhudi hizi ambazo zimetolewa katika mswada huu kwani madhumuni yake ni moja tu kura ya maoni. Hivyo mimi nawashauri wananchi wasiwe na wasi wasi waangalie maslahi ya nchi, waangalie maendeleo ya nchi na waangalie lolote ili kuleta kheri katika nchi yetu basi wataliamua wao.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka niseme kwa ufupi kabisa ni kwamba busara ni jambo zuri sana na busara ndio suala ambalo linamuweka mtu katika mwelekeo mzuri, bila ya busara tukitumia jazba, tukitumia chuki na uhasama basi hatwendi. Kwa hivyo, mimi naomba tuwe na busara, tuwe na mwelekeo mzuri kwa wananchi wetu ili walielewe hili.

Mhe. Spika, naamini muda mdogo ambao umekuja mswada huu lakini kama itatumika busara na taratibu nzuri basi ujumbe utafika kwa wananchi wetu na wataelewa manufaa na maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, tukizingatia mambo mengi hasa nitasema upande wa upinzani kwa mara ya kwanza umecharuka sana na kusema kama atatokea mtu mmoja kuupinga mswada huu basi watamshangaa. Mimi niseme hizo kuwa sio kauli mzuri niseme tu kwamba hili ni jambo la demokrasia sawa sawa na kumshawishi mtu nje ukamwambia lazima fanya hivi au fanya hivi.

Mimi nasema tu tuwe na lugha ambayo si ya kulazimishana kwani kila mwananchi au kila Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ana uhuru wake wa kuamua, sitegemei kama hapa kati yetu tuko watu 77 kuna mmoja amepungukiwa na akili, sote akili zetu ni timamu na tunajua baya na zuri. Kwa hivyo, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani naunga mkono mswada huu na nawaomba wenzangu tuukubali kwa sababu tuangalie hatma ya watu wetu na vizazi vyetu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuandika historia katika siku ya leo ya Baraza la Wawakilishi kwa kuchangia mswada huu muhimu, mswada unaoweka utaratibu wa kura za maoni.

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo naomba kwa dhati sana kumpongeza Mhe. Haji Omar Kheir kwa uwasilishaji wake mzuri kama Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria wa mswada huu. Nawaomba sana Watumbatu wenzangu kama walivyomsikia basi waendelee kuezeka mabati, wasiezue mabati kwa kuezeka makuti. Waendelee kumuungano mkono mwakilishi wao huyu kwa sababu ni mtu makini na mtu mahiri sana.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo mimi sina mambo mengi nina mambo manne madogo madogo na nasema Mhe. Samia alipokuja alisema yeye alifanya *research* na kwa kweli alifanya *research* kutokana na maelezo aliyotuelezea. Mimi pia nimefanya *research* lakini yangu mimi imeelekea katika dini na katika uislamu kwa mintarafu ya hoja hii tunayoizungumza. Nitazungumza mambo mawili muhimu sana. Kwanza nitazungumza ile aya aliyoizungumza Mhe. Mulla na nitaitolea ufafanuzi kidogo na sababu nzuri ili ipate kufahamika vizuri. La pili nitazungumzia kuhusu Mkataba wa *Hudaybia* kati ya Makuraish na Mtume Muhammad (SAW). Haya mawili yanalingana sana na huu wakati hadhir tulionao wakuujadili huu mswada na kura za maoni.

Mhe. Spika, Mhe. Mulla alinukuu aya inayosema baada ya *audhubilahi* inasema *waataswimu bihamdlillahi jamiaan walaa tafarraqu.* Ukiendelea mbele na ukizungumza juu ya aya hii kwa ufupi sana ni kwamba Mtume Muhammad (SAW) alipohajiri Makka kwenda Madina alikuta kule Madina kuna makabila mawili ya Al-aus na Hadhraji wako katika vita vya kupigana wenyewe kwa wenyewe kila siku ya Alhamis au siku ya Ijumaa. Katika ugomvi huu wanaangamizana, wanaumizana na wakati mwengine wanauana, Mtume Muhammad (SAW) alipofika alipata hii taarifa akawaita viongozi wa makundi haya mawili akawaelimisha, akawanasihi mwisho wake wakakubaliana kupatana, Mhe. Spika, wakapatana, wakasikilizana na wakawa kitu kimoja.

Basi alitokea kidudu mtu anayeitwa Al-kaus huyu hakupenda yale mashirikiano ya hayo makundi mawili, akenda kundi la kwanza akawaambia nyinyi mnajua hawa Hadhraji wanasemaje, wanasema mmesalimu amri, akitoka pale anakwenda katika kundi la pili anawaambia Al-aus mnasikia wanasema nini mmesalimu amri. Kwa hivyo, ikawa wanajenga chuki huku na huku basi makundi mawili yale yakarudi kupigana tena na habari ikafika kwa Mtume Muhammad (SAW) akawaita tena akawaambia nyinyi sasa mnajikaribisha katika ukingo wa shimo la moto wa jahanam, msipozindukana mtaangamia.

Kwa hivyo, hawa jamaa wakapiga fatihha, wakamaliza kila kitu na baada ya hapo Madina ikapatikana salama ya kudumu Al-aus na Hadhraji wakawa kitu kimoja wakarudi Makka wakenda wakaiteka Makka, ndio ikapatikana ile Fathhu Makka. Je, haya tunayoyafanya hayalingani na haya/

Mhe. Spika, la pili ni Mkataba wa Hudaybia, mkataba huu kwa ufupi Mtume Muhammad (SAW) alifunga safari na watu wake kwenda Umra Makka kutoka Madina kwenda Makka. Kufika Hudaybia ambao ni ukingoni mwa mji wa Makka Makuraish wakamsubiri, walipomsubiri kwa ufupi wakamwambia Mtume itabidi urudi, leo huna nafasi ya kwenda Makka kwenda kufanya Umra. Masahaba zake kina Omar na wenzake wakalalamika lakini Mtume Muhammad (SAW) akasema wacheni tuwakubalie walivyotaka na kama mwakani tutarudi basi tutakuja kufanya Umra yetu.

Mhe. Spika, Masahaba walikasirika sana kwamba Mtume unakubali hawa Makafiri wanafanya mambo haya na wewe unawakubalia, lakini Mtume akaongoza kikosi chake wakarudi na mwakani wakarudi tena kwenda kufanya Umra na wakaruhusika kwenda kufanya Umra. Hiyo ni hadithi ya pili zinazolingana na haya tunayoyazungumza na tunayoyafanya.

Mhe. Spika, kwa mantiki hiyo Rais wetu mpendwa amekaa na Maalim Seif kama kwamba sitaki nifananishe yupi Kuraish na yupi Mtume hapana, lakini wamekaa na kuzungumza na kukubaliana basi Rais Karume akamwambia Maalim Seif rudi kwa watu wako uzungumze nao na mimi nitarudi kwa watu wangu nitakwenda kuzungumza nao.

Mhe. Spika, yaliyotokea yametokea lakini hatimae shuwari ikapatikana. Mhe. Spika, leo mkataba wa Hudaybia tunaujadili na inshaallah mkataba huu tutaufikisha pahala ndipo ili siku ya pili yake tupate kurudi tufanye Umra yetu kwa salama na amani.

Mhe. Spika, ibara ya 15 ya mswada huu inazungumzia serikali kubeba gharama zote za shughuli hizi za kura ya maoni. Nalitaja hili kwa sababu nataka nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa maamuzi yake haya kwa sababu tulipoletewa hoja katika kifungu kimoja kilitutaka twende kwa wafadhili tukaombe fedha kwa ajili ya kufanya haya. Rais Karume amesema anazo pesa za kutosha kabisa za kufanya mambo haya na ni kweli kabisa kwa wale tunaofanya kazi za serikali tunaopokea mishahara kuna mtu mpaka leo hajapokea mshahara.

Kwa hivyo, pesa zipo na amesema na sisi tumeandika katika hii ibara ya 15 ya mswada huu kwamba fedha zote za shughuli hizi zitalipwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nampongeza sana Rais wetu, nawapongeza na

wasaidizi wake wa fedha kwa jinsi walivyozitunza fedha zetu hadi tukafikia mambo haya mawili mazito ya uchaguzi, ya kura za maoni zote tutazikabili wenyewe. Huo ndio uhuru na huo ndio uungwana na huo ndio uongozi.

Mhe. Spika, mwana falsafa mmoja wa somo la *political science* jina nililihifadhi lakini limenitoka sasa hivi alisema hivi 'Akili finyu hupenda kuzungumza mtu fulani ana hivi, fulani ana tatizo hili, akili ya kawaida *average* huwa inazungumza *invent* jana *Manchester United* iliifunga *Chelsea* magoli manne kwa bila sasa tena hapo mashabiki watakaa wanazungumza *invent* iliyotokea. Lakini akili atimamu iliyoiva yenye thamani inazungumza hoja. Hapa sisi tunazungumza hoja na sote tuna akili timamu, lakini nastaajabu wengine wanaanza nadiriki kusema kutunyooshea sisi vidole tuliokuwepo huku kwa nini?

Kwani kuna mtu huku alisema haungi mkono huu mswada, tunaelimishwa, tunatishwa na wengine wanadiriki kusema kama hatukuunga mkono nchi hii itakuwa na nakama, itazama. Hizi lugha mheshimiwa si lugha sahihi wakati watu wanazungumza sheria yenye muala mzuri kama huu. Mhe. Spika, Mhe. Rais Karume alisema katika hili hakuna aliyeshinda na kwa maana hiyo hakuna kuoneshana vidole, tunazungumza sheria hii basi tuizungumze hii sheria, tuisadie halafu tuende tuitumie tukapige kura za maoni. Jamani tuaminiane kwamba kwa mtazamo wa hapa sote tunaunga mkono.

Mhe. Spika, kama utakubali rai aliyoitoa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo itakuwa jambo la maana sana, lakini ukidhani hatuna haja ya kufanya hivyo si tutaonekana hapa atakayeinua mkono na aliyekuwa hakuinua mkono. Mhe. Jussa hivi karibuni aliandika makala kwenye gazeti kuwakemea watu wake akasema watu wangu baadhi yao hawataki kuunga mkono hili suala wana ajenda za siri, nawaomba waunge mkono hili suala ili twende pamoja.

Ile makala nimeifanyia *cutting* na nimei-*save* na kuanzia hapo ndipo nilipobaini kumbe Mhe. Jussa ndiye mshauri wa Maalim Seif Sharif Hamad kwa sababu aliyoyasema ni mambo yenye muala, ni mambo ya kuwakemea wenzake wenye matatizo kwa wakati huu tuliokuwa hapa sisi hatuna matatizo tusikemewe. Mhe. Spika, hili jambo mimi limekuwa linaniuma sana sitaki kutaja watu lakini kuna watu watatu upande wa upinzani bado hapa tulipofika wanajenga tabia ile ile ya kushtumiana na kusingiziana.

Mhe. Spika, nasema tumefika pahala pazuri Mwenyezi Mungu azibariki sana juhudi zetu, imani zetu na azibariki nia zetu na wananchi tuwaachie wenyewe sisi tukawafundishe, tukawaelimishe maamuzi tuwaachie wenyewe. Lakini nataka tusiwe na hofu kwani wananchi wengi wa Zanzibar hawataki vurugu wanataka amani na utulivu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na mimi narejea tena ule msemo wangu maana mimi ni Mwakilishi wa Donge atakayenihoji kwa nini nasema hivi shauri yake. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Donge na kwa niaba yangu binafsi na kwa bahati nzuri chombo hiki leo kiko hewani wananisikia naunga mkono mswada huu mia fil mia.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni wote, nakushukuru Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo. Nilipata maombi ya wachangiaji 36 tumemudu kuwasikiliza 29, 7 hawakuweza kupata nafasi kutokana na muda na makubaliano ambayo tumeyajenga tangu jana. Niombe radhi basi wale ambao waliniomba na ikawa hawakupata nafasi waone hali halisi na turidhie kwamba michango iliyotoka imejumuisha pamoja na maoni yao. Lakini hata wale ambao hawakuomba nafasi isionekane kwamba wao kwa nini hawakuomba nafasi, tusingeweza kuchangia wote.

Kwa hiyo kutowasikia wengine na wala kutopata majina hapa isionekane kwamba hivyo labda kuna wengine ndio wamepinga ndio maana hawakusema, hapana ni kawaida vyombo vyetu hivi huwa tunajitahidi kuwasikiliza wajumbe kufikia kiasi fulani tukasema kwamba sasa inaelekea kuwa tumeridhika na michango iliyokwisha toka. Kwa hivyo, bila ya kuwataja naomba wote wale ambao wamekosa nafasi waridhie na nikirudia tena Mhe. Abass Juma Muhunzi jana nilimkatisha kwa sababu ya muda ulikwisha na sikupendelea kwamba tuwe tunaendelea leo, lakini nae sauti yake imesikika. Baada ya hayo na baada ya shukurani nyingi sana ambazo nazileta kwenu Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi kufanya majumuisho kwa muda tuliokubaliana.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi kwanza napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe binafsi kwa kuweza kuniruhusu kusoma mswada huu muhimu kwa nchi yetu. Vile vile naendelea tena kumshukuru Mhe. Waziri Kiongozi kwa kuweza kuniongoza na kunipa baraka zote katika kusoma na kusimamia mswada huu pamoja na shghuli zake nyengine zote ambazo anazoniongoza nizisimamie.

Mhe. Spika, tatu nataka niwapongeze Waheshimiwa wote Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia na wale ambao hawakuchangia.

Mhe. Spika, nne nataka niwapongeze vyombo vya habari ambavyo tangu jana baadhi yao wako *live* bila ya kulipwa gharama yoyote na Baraza la Wawakilishi kwa kuwawezesha wananchi ambao waliotuleta hapa kusikia ni namna gani waheshimiwa wao wanavyowakilisha katika chombo hiki adhimu.

Mhe. Spika, tano nataka niwapongeze wananchi wote wa Zanzibar pamoja na Watanzania nzima kwa sababu leo tunaweka kitu cha historia katika nchi yetu ambacho tunaweza tukasema kwamba tunajivunia kwa Tanzania Zanzibar ndio tunaanza. Kwa hivyo, Zanzibar ni mwalimu wa demokrasia.

Mhe. Spika, nisije nikakosa fadhila nataka nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye yeye ndiye aliyeniwezesha kusimama hapa kuweza kusoma mswada huu na kuweza kusimamia suala hili zito katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwanza kabla sijaanza kuwasomea Katiba kwa sababu Katiba ndio iliyotuweka hapa, katiba ndio inayotuongoza na tukiikiuka katiba basi wananchi watatuhukumu. Sasa Mhe. Spika, kama kuna watu walikuwa wana hofu, wasi wasi, sasa katiba hii ndio itayowatoa hofu, na katiba hii hii ndio itakayowatoa wasi wasi.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu nisome Katiba ya Zanzibar kifungu cha 9(1) kinachosema Serikali na Watu, hiyo *sub heading*.

Kifungu cha 9(1) **"**Zanzibar itakuwa ni nchi ya kidemokrasia na haki za kijamii".

9(2) "Kwa hivyo hapo inaelezwa rasmi kwamba:

(a) "Mamlaka ya kuendesha nchi ni ya wananchi wenyewe ambapo nguvu na uwezo wote wa serikali kufuatana na katiba utatoka kwa wananchi wenyewe".

(b) "Usalama na hali nzuri kwa wananchi itakuwa ndio lengo kubwa la serikali".

(c) Katiba hii itahakikisha kwamba wananchi wanashiriki katika serikali yao.

Hii katiba sikuitunga mimi, katiba hii imetungwa mwaka 1984 na chombo hiki kimewekwa kwa mujibu wa katiba hii.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, leo tumeleta mswada huu wa kura ya maoni tunatekeleza kifungu cha 9(1) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Kwa sababu sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tumeletwa hapa kikatiba na wananchi kuwawakilisha. Lakini sasa hivi chombo hiki hiki kimeamua kutoa uwazi wa demokrasia kubwa zaidi, yaani demokrasia pana sana, kurejesha maamuzi yale ambayo ni mazito zaidi kuwarejeshea tena wananchi wafanye maamuzi.

Mhe. Spika, kwa mswada huu, basi leo tumeweza kutekeleza vizuri sana Katiba yetu ya Zanzibar. Baada ya dibaji hiyo, sasa naomba niendelee katika kuanza kutoa majumuisho ya mswada huu.

Mhe. Spika, kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi, Mhe. Haji Omar Kheir pamoja na kamati yake yote ya Katiba na Utawala Bora.

Mhe. Spika, kazi kubwa ambayo iliyofanywa na kamati hii imeweza kurahisisha mswada huu ukawa hauna mwahala mwa kutoa koma au kusema hapa ongeza *full stop*. Ndio maana Mhe. Spika, kama ulikuwa unafuatilia michango ya Waheshimiwa Wajumbe wote wengi wao walikuwa hawendi kwenye mswada, wengi walikuwa wanaelezea hisia zao, wengine wanaona raha, wengine wanaona ladha, mpaka Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora mwalimu wangu alisema, yeye alitoa mfano.

Yeye alisema unapojifundisha baskeli mwanzo unaiona ngumu, na sio baskeli tu, kitu chochote, kinakuwa kigumu na unaweza kukaribia kughairi. Lakini unatakiwa uwe na moyo wa ujasiri, ukishajaribu mara ya kwanza, ya pili na ya tatu unakwenda dede tena unaachia mikono barabarani na gari zinapita. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Spika, jambo hili kwa wananchi wetu litakuwa zito lakini hebu kuweni wajasiri kama sisi wenzenu, nadhani baada ya muda mchache kwa kuwa linakuja kwenu hili basi mtaachia mikono *free* kabisa yaani *peddle* pia unaziachia baskeli inakwenda wenyewe.

Sasa Mhe. Spika, nataka nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti pamoja na wajumbe wake wa kamati kwa kuweza kunisaidia sana kuweka sawa yale makosa madogo madogo yaliyokuwemo katika mswada huu na ndio maana mswada umekwenda vizuri sana.

Kwa ruhusa yako naomba sasa niwaseme wote waliochangia mswada huu pamoja na wale waliochangia kwa maandishi.

1. Mhe. Haji Omar Kheir (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala)
2. Mhe. Abubakar Khamis Bakari (Waziri Kivuli, Afisi ya Waziri Kiongozi).
3. Mhe. Said Ali Mbarouk
4. Mhe. Haji Faki Shaali
5. Mhe. Ahmed Nassor Mazrui
6. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali

7. Mhe. Ali Moh'd Bakari
8. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
9. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi
10. Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii
11. Mhe. Juma Duni Haji
12. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
13. Mhe. Mohamed Ali Salim
14. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak
15. Mhe. Zakiya Omar Juma
16. Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira
17. Mhe. Rashid Seif Suleiman
18. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora
19. Mhe. Abass Juma Muhunzi
20. Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji
21. Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi
22. Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin
23. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo
24. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba
25. Mhe. Aziza Nabahan Suleiman
26. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi
27. Mhe. Zahra Ali Hamad
28. Mhe. Ali Suleiman Ali
29. Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo.

Waliochangia kwa maandishi ni:-

1. Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii
2. Mhe. Salim Abdalla Hamad
3. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
4. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
5. Mhe. Ali Mzee Ali
6. Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi
7. Mhe. Hasnuu Moh'd Haji
8. Mhe. Najma Khalfan Juma
9. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja

Mhe. Spika, kuna wengine ambao sikuwataja humu lakini majina yao unayo wewe, lakini wote kama nilivyosema naomba na wao niweze kuwatambua kwamba michango yao tunaithamini.

Mhe. Spika, nikienda kwa haraka haraka kimsingi wajumbe wote wamekubaliana na mswada wangu. Sasa kuna mambo madogo madogo lakini

namshukuru sana Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa sababu zaidi wengi walikuwa wakikizungumzia kifungu cha 8. kifingu hicho walikuwa wakizungumzia labda tu yale aliyozungumza Mhe. Naibu Waziri Kiongozi bado tuna makole yale ya zamani zile dhana.

Sasa mimi nadhani kwa ufafanuzi alioutoa Mhe. Waziri wa Mawasiliano ameweza kunisaidia sana. kwa sababu kwa mujibu wa wale ambao wataweza kupiga kura ya maoni ndio wale wale ambao wenye haki ya kupiga kura katika Daftari la Kudumu la kupiga kura.

Mhe. Spika, nataka niende haraka haraka kwa baadhi ya yale mambo yanayohitaji ufafanuzi. Suala la vyeti vya kuzaliwa hili halihusiani na mswada wangu, hili bado liendelee katika utaratibu wa sehemu ya vitambulisho.

Lakini vile vile limezungumzwa suala la gharama katika vyeti vya kuzaliwa. Hili Mhe. Spika, nilikuwa nataka nilitolee ufafanuzi kidogo, suala hili sisi wenyewe tumeshalipitisha katika bajeti ya Baraza la Wawakilishi ya mwaka 2009/2010.

Kwa hivyo, kusema kupunguza bei ya *birth certificate* kwa kweli labda mapendekezo hayo tuje tuyatoe katika kikao kinachokuja cha bajeti ya mwaka 2010/2011. Kwa sababu fedha hizi tayari zilikwishakufanyiwa makisio na tayari sisi tulikwishaipa baraka afisi ya mrajis kuweza kukusanya fedha hizi.

Kwa hivyo, kusema kwamba sasa hivi apunguze kwa kweli itakuwa lile ambalo tumelifanyia maamuzi tutakuwa tunajisuta sisi wenyewe. Sasa hili nilikuwa naomba katika kikao cha bajeti kinachokuja mimi nadhani tunaweza tukashauri hili sasa Mhe. Waziri na yeye atajaribu kuangalia uwezekano wa kuliwezesha suala hilo.

Mhe. Spika, suala Mhe. Said Ali Mbarouk alielezea kwamba wananchi watakaokuwa watapinga suala zima la matokeo ya kura ya maoni, kwamba wao wamepewa uhuru wa kwenda Mahkamani lakini serikali imezuiwa. Hapa serikali imezuiwa kwa sababu serikali tayari imetoa mamlaka kwa wananchi wao wenyewe. Kwa hivyo, wananchi wakishatoa maamuzi yao serikali haina namna yoyote ya kufanya isipokuwa kukubaliana na maamuzi hayo. Kwa hivyo, ufafanuzi wa suala hilo zaidi ilikuwa ni huo.

Vile vile walijaribu kuzungumzia kujaribu kuweka mawakala katika vituo. Suala la mawakala kwa sababu suala hili ni suala ambalo si la vyama, suala hili tukianza kulichukulia kama la vyama ndio pale tutakapoanza kwenda kutengeneza upinzani ambao hauna sababu au hauna msingi. Hili ni suala la wananchi wote, Wazanzibari wote wakaamue wenyewe watakavyo. Kwa

hivyo, suala la kuweka mawakala tumeipa mamlaka Tume ya Uchaguzi, kuna watu au taasisi wataomba, Tume ya Uchaguzi wale watakaoona wanafaa wataweza kuwapa mamlaka hiyo kwa kwenda kukaa na kuangalia lile zoezi linavyokwenda.

Kwa sababu haitowezekana kwamba Tume ya Uchaguzi wao wenyewe wajitosheleze tu kwamba wamekusanya zile taarifa, watoe takwimu. Kwa sababu suala unapowapelekea wananchi wanataka hata yale yanayofanyika waridhike na kile kilichofanyika kimefanywa kwa mujibu wa yale matakwa yao.

Kwa hivyo, Tume ya Uchaguzi tuipe mamlaka hiyo na tunaamini kutokana na *spirit* tunayokwendanayo hakuna ubabaishaji wowote ambao utajitokeza. Yale matokeo yatayotoka Tume ya Uchaguzi ndio watakayoweza kuyatangaza na wale watakaokuwemo mule basi watakuwa ni mashahidi wetu ambao watatuwakilisha katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, kama nilivyosema maeneo mengi bado yalikuwa yanazungumzia zaidi ni hisia au utashi kwa mambo yaliyopita. Lakini cha msingi Mhe. Spika, kulikuwa kuna suala la Mhe. Juma Duni Haji.

Mhe. Juma Duni yeye alipendekeza kwamba zile siku za kukata rufaa, zile siku 30 alisema zitakuwa kidogo kwa nini tusiweke siku 60. Mhe. Spika, wazo la Mhe. Juma Duni ni wazo zuri sana, na kama tungekuwa tuna muda mzuri mswada huu au sheria hii tungepata muda mzuri kama hakuna jambo lolote mbele Mheshimiwa hoja yako ningeikubali moja kwa moja. Lakini hapa tukiangalia muda haupo.

Sasa hivi natoa mfano, Tume ya Uchaguzi haijamaliza zoezi la Daftari la Kudumu, Tume ya Uchaguzi ikishamaliza zoezi la daftari kuna muda wa pingamizi, kuna majina itabidi yawekwe pale wananchi wakatoe pingamizi. Kwa hivyo, ina maana pale kuna muda wake siku zinakwenda hizo. Vile vile wale ambao watakaokuwa na mashaka itabidi kesi ziende muda mwengine unakwenda huo. Kwa hivyo, ina maana hapa tukija tukiweka muda huu wa siku 60 sasa hivi hayo ambayo mnayakataa ndio hayo yatakayokuja kutokea.

Sasa kwa *spirit* tunayokwendanayo sasa hivi kama tulivyosema sisi hapa tushakubaliana masuala tukawaachie wananchi waamue, sasa tusiwaachie wananchi waamue matokeo yake huo muda tunaotaka waamue tukaja tukaukosa. Nikisema hivyo nadhani Mhe. Juma Duni amenielewa vizuri, kwa bahati nzuri yeye ni mwalimu na kwa bahati nzuri kamsomesha na mwalimu wangu Maalim Haroun Ali Suleiman na Maalim Haroun akanisomesha mimi sasa ah! itabidi niwe na *discipline* kubwa sana hapa Barazani sasa hivi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kulikuwa kuna baadhi ya hoja tu

Mhe. Spika: Waziri ni mjukuu wa Mwalimu Juma Duni. *(Kicheko)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Kwa hivyo, ndio kuna baadhi ya hoja na vile vile kulikuwa na hoja nyengine ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika suala la kifungu kile cha tatu alisema katika kura za ndio au hapana. Sasa katika marekebisho ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ndio maana nikasema kazi kubwa ilifanywa na kamati hiyo tuliongeza vile vile na zilizoharibika. Kwa hivyo, ndio maana nikasema hizi hoja nyengine kila nikitaka kuzijibu nikiangalia kwenye marekebisho ya mwenyekiti kwa kweli zilikuwa tayari zimeshajieleza.

Mhe. Mohamed Ali Salim kwa sababu najua atakuja kunipigia buti, atanipigia buti kwa lugha tu, na mimi kwa kuwa mwalimu wangu yuko pale sitaki aje anipigie buti kwa lugha. Alisema kwamba Gazeti la Serikali ni lipi, Zanzibar Leo au Gazeti Rasmi la Serikali? Sasa kwa bahati aliuliza swali halafu akanisaidia jawabu.

Mhe. Spika, hapa tumekusudia ni Gazeti Rasmi la Serikali sio Gazeti la Zanzibar Leo. Kwa hivyo, Mhe. Mula sitegemei kama kuna buti ambayo itanishitua roho ambayo itatokea kwa upande wako.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza, kwa sababu kuna hoja nyengine nikizijibu itakuwa kama nataka na mimi kuzusha hoja na mimi sitaki kuzusha hoja. Isipokuwa tu kwa kumalizia Mhe. Spika, nataka kuwaeleza wananchi wote hapa leo hatukuja kufanya maamuzi ya kuwalazimisha au kuwaelekeza wafanye nini, hapa leo tumekuja kuleta mswada kuanzisha hii sheria.

Kuna maoni mbali mbali yalitoka, tunataka mfumo wa serikali shirikishi jamii, wengine wanasema tuendelee na mfumo huu huu. Hata katika michango yetu hoja hii ilipokuja kuna maoni tofauti tofauti yaliyotoka humu. Kwa hivyo, sasa hayo yote mawili hayawezi kutekelezeka bila ya kuwa na kitu maalum, bila ya kuwa na *instrument*, yaani hiki ni chombo ambacho sasa kinawapa mamlaka wananchi wao wenyewe na suala hili sio la kuamua tu, wanataka serikali shirikishi au tuendelee na mfumo tuliokuwanao sasa hivi.

Mhe. Spika, demokrasia ambayo tumeitoa na ndio maana tukasema kwamba rais wetu bado anastahiki, kuna shahada nyengine mimi naamini ziko katika *boxes* hajapewa. Kwa sababu ameanzisha wizara ya Katiba na Utawala Bora, ametoa demokrasia pana sana, lakini sasa hivi anawapelekea wananchi sheria ya kufanya maamuzi wao wenyewe.

Mhe. Spika, sasa hivi serikali inawapelekea wananchi wao wenyewe waweze kufanya maamuzi, sio kwa maamuzi tu ya muundo gani wa serikali iweze kuwaongoza, na jambo lolote ambalo wanahisi kwamba sasa hivi waheshimiwa wetu hili tunataka tuliamue sisi, basi watawaambia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao wataleta hoja hapa na sisi tutajadili na kumuomba rais akiona inafaa basi hoja hii itarudi tena kwa wananchi.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji alieleza vizuri sana, kuna watu wanapiga kura za maoni Ulaya kwa mtaa tu, sisi hatujafikia huko, sisi tunataka yale maamuzi ya wengi yaweze kufanya kazi kwa maslahi ya nchi yetu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nawaomba sana Waheshimiwa kwanza tupunguze jazba, tukipunguza jazba tutakuwa tumewasaidia sana wananchi wetu. Kuna lugha zilikuwa zinazungumzwa humu hata na mimi kidogo sikuzifurahia, kwa sababu unapokuwa Mheshimiwa, unapoongoza watu usitegemee kama watu wote watakubali yote yale unayoyataka wewe.

Nitakupeni mifano, sisi wenyewe Waheshimiwa humu kuna watu tunawahudumia kuliko wazee wetu waliotuzaa, lakini akikaa barazani hivyo anavyokusema huwezi kuamini. Unamhudumia mtu huyo kuliko unavyomhudumia baba yako mzazi, lakini huwezi ukasema kwamba ah, yule kwa kuwa ndio anakaa ananisengenya, ananisema, yeye akija na shida chapa, anakuja na shida chapa. Kwa hivyo, usitegemee kwamba kila ambacho unachokitaka wewe na wale wananchi wako watakifuata.

Lakini wewe kama utakuwa mtu wa busara basi naamini kuna siku wataanza kukusikiliza lakini sasa ukianza kwenda kuwatolea maneno machafu wale wasiotaka mema, wasiofanya hivi, wasioipenda nchi, hee, unafikiri atakusikiliza nani?

Pengine kama upo katika jukwaa hujamaliza watu washatawanyika unabakia peke yako, sasa utajiuliza wale ndio wote wasiotaka mema? Kwa sababu Mheshimiwa unatakiwa uende pahala ujenge hoja watu waikubali ile hoja yako, mtu akakae kwake alie afute machozi, ah kwa vile alivyonambia basi haya, ndio imo hiyo, yaani mtu anakubali lakini kwa shingo upande lakini si kakubali. Kwa sababu ulijenga hoja na ile hoja akaikubali.

Sasa Mhe. Spika, mimi naomba sana, mswada huu ukipita ni uhuru wa wananchi tumewaachia wao wenyewe tusiende kuwafanyia jazba, usije ukenda ukatoa maelekezo unayoyataka wewe wakapingana nayo ukenda ukagombana na watu. Kwa sababu Mhe. Spika, ukiwemo ndani ya Baraza una kinga, lakini ukitoka nje ya Baraza pingu ipo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, waheshimiwa huko tusije tukasikia wamepigwa pingu, kwamba unakwenda unawalazimisha watu kitu unachotaka wewe wao hawakitaki unaanza kurusha makonde pingu itacheza, ukiwa ndani ya Baraza humu pingu anaidhibiti Mhe. Spika.

Kwa hivyo, baada ya hayo machache Mhe. Spika, naomba sana sasa mswada huu umeshajadiliwa naomba kutoa hoja tuupitishe kifungu kwa kifungu ili tumpelekee Mhe. Rais na baadae iwe sheria. Naamini Mhe. Rais baada ya kuupeleka mswada huu, hatochukua muda mrefu, tukiuzuia ndio nakwambieni kweli, atakuwa hatii saini, lakini kama tutaukubali hapa basi Mhe. Rais atautia saini kwa ajili ya utekelezaji. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa yale ambayo ameyafanyia majumuisho ambayo Waheshimiwa Wajumbe wangu hapa naona mmeyapokea vizuri kwa sababu mmeyafurahia majumuisho yaliyofanywa.

Nimeombwa jambo moja la namna ya kupitisha suala hili na likaungwa mkono na Mhe. Naibu Waziri Kiongozi. Tumewahi kufanya kitu cha aina hiyo, *row call* ile. Sasa ile kwa kawaida huwa inatayarishwa, unawa-*caution* wajumbe ili wajumbe wasikose kufika. Matayarisho hayo hatukufanya. Nilipiga mahesabu nikakuta tuko wajumbe kama 62, 63 kama hivyo. Sasa wataokuwa hawapo kwa kweli tutakuwa hatujawatendea haki, ilibidi tu-*caution* mapema kwamba kutakuwa na *row call* hiyo ili tuweze kumsikiliza Mhe. Mjumbe mmoja baada ya mwengine kwa kumwita jina.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naafiki.

Tuliwahi kufanya wakati wa marekebisho ya katiba suala kama hili nakumbuka mwaka 1999. Pale tulikuwa tunataka kuhakikisha tupate ile *two-third majority*, hili linaamuliwa kwa *simple majority.* Mimi nafikiri tukubaliane kwenda, kwa kuwa hatukufanya matayarisho mazuri kabla tukawa-*caution* Waheshimiwa Wajumbe twende kwa utaratibu wa kawaida ambao tunahitaji *just simple majority.*

Baada ya Mhe. Waziri kutoa hoja sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Mswada wa Baraza Zima ili kupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Hiyo ni taarifa uliyosema, kwa hivyo katibu wangu ita kamati.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Kifungu cha 1 Jina fupi na kuanza kutumika

Kifungu cha 2 Ufafanuzi na Marekebisho yake

Kifungu cha 3 Amri ya Kura ya Maoni na Marekebisho yake

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nina wasi wasi tu, labda ukishatolewa nitakuwa sina wasi wasi na hiki kifungu. Kifungu cha 3 hiki mwishowe kina-*refer* jadweli cha 3(2). Na hilo jadweli ambalo liko mwisho wa sheria hii linasema ni amri ya kuitisha kura ya maoni, lakini kifungu ambacho kimepewa nguvu hapa ni chini ya kifungu cha 3(2). Sasa mimi kwa nilivyoifahamu hii sheria ni kwamba, amri ya kuitisha kura ya maoni ambayo anaifanya rais hapa ni kifungu cha 3(1), na kuna maneno hapa kwenye mstari wa nne kwenye hicho kifungu cha 3(1).

"Rais kwa kutoa amri ya maandishi na kuchapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali". Lakini vile vile kwenye kifungu cha 3(3) "amri ya kufanyika kwa kura ya maoni chini kifungu cha 3(1) cha kifungu hiki. Sasa hapo kilichokuwa *quoted* ni kifungu cha 3(2) ambacho kinatoa ule muundo wa ile amri yenyewe, lakini ile nguvu za ile amri nimeona kwa mujibu wa hii sheria iko kama kifungu 3(1), labda nikishatolewa wasi wasi pengine sikufahamu vizuri basi tutaendelea.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Mwenyekiti, kifungu alichosema Mhe. Abass Muhunzi kifungu cha 3(2) labda nikisome kinasema hivi, "Amri ya kura ya kufanyika kura ya maoni itakuwa katika mfumo kama inavyoelezwa katika jadweli ya sheria hii". Yaani katika jadweli ya sheria hii ni jadweli hili la huku nyuma, tunalo katika ukurasa wa nane. Kwa hivyo, nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa kwamba isomeke kifungu cha 3(1). Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.
Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa nadhani tumeifahamu vizuri hiyo kwamba uwezo hasa uko kwenye kifungu cha 3(1). Haya tuendelee.

Kifungu cha 3	Amri ya Kura ya Maoni na Marekebisho yake
Kifungu cha 4	Tume ya Kuwa na Dhamana ya Kura ya Maoni na Marekebisho yake
Kifungu cha 5	Uteuzi wa Maafisa wa Kura ya Maoni na marekebisho yake
Kifungu cha 6	Vituo vya Kupigia kura
Kifungu cha 7	Karatasi za Kura
Kifungu cha 8	Haki ya Kupiga Kura ya Maoni pamoja na Marekebisho yake
Kifungu cha 9	Utaratibu wa Kupiga Kura ya Maoni na Marekebisho yake
Kifungu cha 10	Matokeo ya Kura ya Maoni na Marekebisho yake
Kifungu cha 11	Matokeo ya Kura ya Maoni Kufuatwa na Serikali na Marekebisho yake
Kifungu cha 12	Kuhoji Matokeo ya Kura ya Maoni na Marekebisho yake
Kifungu cha 13	Mtu Hatotakiwa Kueleza Jinsi Alivyopiga Kura
Kifungu cha 14	Katazo la Uvunjifu wa Amani katika Kura ya Maoni
Kifungu cha 15	Maelekezo ya Jumla pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 16	Gharama za Kuendesha Kura ya Maoni na Marekebisho yake
Kifungu cha 17	Kutumika kwa Sheria ya Uchaguzi na Marekebisho yake
Kifungu cha 18	Makosa na Adhabu na Marekebisho yake
Kifungu cha 19	Kanuni na Marekebisho yake

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kukubaliana bila ya mabadiliko yoyote pamoja na masahihisho, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali mswada huu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Kura ya Maoni ya Mwaka 2010

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Kura ya Maoni ya Mwaka 2010 usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaokubali mswada huu katika kusomwa mara ya pili wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Katibu: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa rasmi kwamba, Mswada wa Sheria ya Kura ya Maoni ya Mwaka 2010 na mambo mengine yanayohusiana na hayo sasa umepitishwa rasmi na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kukushukuruni tena kwamba mmoja kati yenu niliyefarajika sana na mambo yetu haya ambayo tulianza kwenye mkutano uliopita wa kumi na nane ni mimi Spika wenu. Mmekuwa mnanisaidia sana mara zote lakini sasa mnanisaidia zaidi.

Shughuli za kiti hiki zimekuwa nyepesi wakati uzito wa kiti bado ni ule ule, lakini shughuli zimekuwa nyepesi. Hii inatokana na mashirikiano makubwa na imani mliyonayo ndani ya nyoyo zenu katika kutekeleza wajibu wa shughuli zetu Waheshimiwa Wajumbe. Nakushukuruni sana kwa mashirikiano makubwa, tuoneshe mashirikiano haya kwa wananchi wetu ili tufike pahala pazuri pa mustakabali wa nchi yetu kwa leo na kesho na kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Waheshimiwa Wajumbe tufikie hapa kusitisha shughuli zetu hadi jioni. Nataka nikupeni taarifa tu kwamba, jioni utawasilishwa mswada wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kuhusu masuala ya uvuvi, ambayo wanaohusika wote wako tayari. Jioni hio hio mtapata faraja ya kiti hiki kuendeshwa na Mhe. Thuwaybah E. Kissasi, Mwenyekiti mpya wa Baraza tuliyemchagua kwenye kikao kilichopita mkutano wa kumi na nane. Kwa hivyo, nimeshamuwekea zana zake hapa tayari mumpe mashirikiano kama vile mnavyofanya kazi hiyo siku zote.

Yeye nimeshamuarifu yuko tayari kabisa amefurahi kuja kukalia kiti hiki na majoho yanatengenezwa. Baada ya hayo machache Waheshimiwa Wajumbe sasa naihirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 6:35 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa11:00 jioni)
(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Hoja za Serikali

Mswada wa Kufuta Sheria ya Uvuvi na Kuweka Masharti Bora Yanayohusiana na Usimamizi na Maendeleo ya Uvuvi ndani ya Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya yote naomba kuchukua nafasi hii kwa mara nyengine tena kukupongeza kwa dhati kwa kuchaguliwa kwako na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar na kuandika historia mpya ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kuwa na Mwenyekiti mwanamke. Kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira, tunakuombea kila la kheri na mafanikio mema katika utekelezaji wa majukumu yako mema ya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwa niaba ya wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira naomba kuchukua nafasi hii kupitia Baraza lako tukufu kuipongeza sana Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi ya Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Salmin

Awadh Salmin, Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni, kwa mashirikiano mazuri waliyokuwanayo na wafanyakazi wa wizara yangu wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yao ya kazi, ikiwa pamoja na michango yao mizuri wakati wa kufanya majumuisho ya ziara yao. Kwa ujumla tumefaidika sana na ziara yao hiyo kutokana na maoni na mapendekezo waliyotupa ambayo yatatusaidia sana katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wafanyakazi wa wizara yangu naomba kuchukua nafasi hii ya kuwapongeza Waheshimiwa Juma Duni Haji na Nassor Ahmed Mazrui kwa kuteuliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, aidha naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa michango yao mizuri wakati wakijadili Sheria ya Uvuvi katika semina iliyofanywa tarehe 28 Machi, 2010.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria ya Uvuvi Nam. 8 ya Mwaka 1988 *(Fisheries Act 1988)* ni sheria ambayo ilihusika na usimamizi na utekelezaji wa kazi za uvuvi na mazao ya baharini kwa maji ya ndani *(Internal Waters)*, maji ya nchi *(Territorial Waters)*, pamoja na eneo la ukanda wa uchumi *(Exclusive Economic Zone).*

Sheria hii hivi sasa ina mapungufu na inahitaji kufanyiwa mabadiliko makubwa. Kutokana na hali hiyo, imeonekana ni vyema kuwa na sheria mpya itakayoweza kwenda na hali ya hivi sasa.

Miongoni mwa sababu zinazopelekea kuwa na sheria mpya ni pamoja na mambo yafuatayo:

- Kuongezeka kwa matumizi ya rasilimali za baharini.

- Kuwepo kwa migogoro mingi katika matumizi ya rasilimali za baharini inayojumuisha na migogoro baina ya wavuvi kwa wavuvi, kijiji kwa kijiji, wavuvi, wakulima wa mwani, pamoja na migogoro inayohusisha baadhi ya wawekezaji wa Sekta ya Utalii.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na sababu hizo za msingi, wizara inawasilisha katika kikao chako mapendekezo ya Sheria mpya ya Uvuvi ya Mwaka 2010 ambayo itaondoa kasoro mbali mbali katika Sheria ya Uvuvi Nam. 8 ya Mwaka 1988.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kabla kufikia hatua ya kutoa mapendekezo ya sheria mpya, ilichukua hatua za makusudi kupata maoni ya wavuvi wenyewe katika ngazi za wilaya zote Unguja na Pemba kwa ajili ya kupata miongozo sahihi baina ya mahitaji na taratibu za kuvua kwa kuzingatia mambo manne yafuatayo:

- Hali halisi ya uchumi wa nchi yetu.

- Hali halisi ya mazingira tunayokabiliana nayo.

- Hali halisi ya wataalam tulionao hapa nchini.

- Utatuzi na ufumbuzi wa migogoro itokanayo ndani ya jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria ya Uvuvi Nam. 8 ya Mwaka 1988 ni sheria yenye sehemu 6 ambayo sheria inapendekezwa itakuwa ni sehemu ya saba kutokana na kuingizwa vifungu vifuatavyo:

1. Katika mapendekezo ya sheria mpya kimeingizwa kifungu kitakachohusiana na kuwepo kwa Idara ya Uvuvi pamoja na kuelezea majukumu yake ya kiutawala *(administration).*

2. Kutakuwa na Kitengo cha Kuhifadhi Bahari *(Marine Conservation Unit)* ambacho kitashughulikia usimamizi wa kazi zote za Maeneo ya Hifadhi ya Bahari *(Marine Conservation Area).*

3. Kurekebisha adhabu ziliomo katika Sheria Nam. 8 ya Mwaka 1988 ambazo zimepitwa na wakati na hivyo imeonekana ni muhimu kufanya marekebisho kufuatana na hali ya maendeleo ya uvuvi ilivyo hivi sasa.

Katika mapendekezo ya sheria mpya imezingatiwa kuingizwa na kupendekezwa adhabu kwa yale mambo ambayo yanadhoofisha mazingira ya bahari na hayakuwemo katika Sheria Nam. 8 ya Mwaka 1988 vifungu vya 28, 32 na 35.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na marekebisho hayo, sheria mpya inayopendekezwa itakuwa na sehemu kuu saba badala ya sita kama ilivyokuwa katika Sheria ya Uvuvi Nam. 8 ya Mwaka 1988.

Madhumuni na Sababu. Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umeandaliwa kwa ajili ya kuzifuta Sheria Nam. 8 ya Mwaka 1988 na Kuweka Sheria mpya ambayo inaweka Masharti Bora yanayohusiana na Usimamizi na Maendeleo ya Uvuvi katika Maji ya Ndani na Maji ya Nchi ya Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo.

Mswada huu una sehemu saba zifuatazo:

Sehemu ya Kwanza inaelezea utangulizi ambao unaelezea Jina fupi na tarehe ya kuanza kutumika. Eneo la matumizi ya sheria na ufafanuzi wa baadhi ya maneno yaliyotumika.

Sehemu ya Pili inaelezea kuhusu Utawala ikijumuisha Idara ya Uvuvi, Kazi za Idara, Uteuzi na kazi za Mkurugenzi.

Sehemu ya Tatu inaelezea Uendelezaji na Udhibiti wa Sekta ya Uvuvi kwamba Waziri anaweza kudhibiti kazi za uvuvi, kuweka Mipango ya usimamizi na maendeleo, Uanzishwaji wa madiko, pamoja na Ridhaa ya maandishi kwa mgeni.

Sehemu ya Nne inaelezea Utoaji wa Leseni kwa Shughuli za Uvuvi ikijumuisha Masharti ya jumla ya utoaji wa leseni, pamoja na Idhini ya kufanya utafiti wa kisayansi.

Sehemu ya Tano inaelezea kuanzishwa kwa Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari, Njia za uvuvi zilizokatazwa, Matumizi ya mitego iliyokatazwa, Kuachiliwa vyombo vya uvuvi kwa dhamana, Kufilisi na kuangamiza mitego iliyokatazwa.

Sehemu ya Sita inaeleza Makosa na Adhabu ikijumuisha Adhabu ya kuvua kwa kutumia baruti na vitu vya sumu, Adhabu kwa kumzuia Afisa aliyeidhinishwa na Malipo ya faini kwa mgeni.

Sehemu ya Saba inaelezea Masharti Mengineyo yakiwemo Msamaha, Kanuni, Kutatua makosa nje ya Mahakama.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha waraka huu wa Kufuta Sheria Nam. 8 ya Uvuvi ya Mwaka 1988 na Kuanzishwa Sheria mpya ya Uvuvi ya Mwaka 2010.
Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waitafakari na waichangie vizuri, kwani tunaamini itatusaidia sana kufanikisha utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi): Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *(Subhana Wataala)* kwa kutujaalia neema zake na kuendelea kuwa hai tukiwa wazima na afya njema.

Pili, nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo kutoa maoni kwa niaba ya Kamati ya Fedha na Uchumi yanayohusiana na Mswada huu wa Kufuta Sheria ya Uvuvi na Kuweka Masharti Bora yanayohusiana na Usimamizi na Maendeleo ya Uvuvi ndani ya Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Aidha, niruhusu nitumie nafasi hii uliyonipa kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa mashirikiano yao ya dhati kabisa waliyonipa kwa muda wote tulipokuwa tunafanya kazi alizotukabidhi Mhe. Spika, ukiwemo mswaada huu ulio mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wawakilishi hao kwa kuwataja majina:

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin - Mwenyekiti
2. Mhe. Ali Abdalla Ali - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Assaa Othman Hamad - Mjumbe
4. Mhe. Ashura Abeid Faraji - Mjumbe
5. Mhe. Said Khelef Ali - Mjumbe
6. Mhe. Aziza Nabahan Suleiman - Mjumbe
7. Mhe. Mwajuma Faki Mdachi - Mjumbe
8. Mhe. Juma Duni Haji - Mjumbe
9. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Mjumbe
10. Mhe. Rashid Seif Suleiman - Mjumbe
11. Ndg. Amour Moh'd Amour - Katibu
12. Ndg. Maryam Hussein Rajab - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira pamoja na timu yake, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi pamoja na wengineo wote ambao kwa juhudi zao zimetuwezesha leo kuwepo hapa tukiujadili mswada huu.
Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba Wajumbe wanaelewa vyema dhana hii ya kuwepo kwa utunzaji bora wa rasilimali za bahari; Wizara hii ilitoa elimu kupitia semina kwa Wajumbe. Nimpongeze kwa dhati kabisa Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini kwa kuiwasilisha elimu hiyo kwa ustadi mkubwa uliomfanya kila Mjumbe kuelewa kwa kina mantiki

ya mswada huu. Kwa kweli Mkurugenzi huyu ni hazina ya Taifa inayohitaji kuenziwa.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na hilo, Kamati yako inaridhishwa kabisa na juhudi kubwa anazozichukua Mkurugenzi wa Idara hii Mussa Aboud Jumbe kwa kusimamia Idara katika utendaji wa shughuli zake za kila siku hususan katika Mradi wa Uhifadhi wa Bahari na Ukanda wa Pwani yaani *MACEMP*. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, jamii ya wavuvi imeweza kunufaika sana na mradi huu kupitia nyanja mbali mbali chini ya usimamizi wake mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, sote tunaamini kwamba uvuvi tangu asili ni moja kati ya shughuli muhimu za kiuchumi inayofanywa na wananchi wa visiwa hivi. Ni dhahiri kwamba mahitaji ya kiuchumi kwa ustawishaji wa jamii yanaongezeka, sambamba na ongezeko la idadi ya watu. Kwa vyovyote vile ongezeko hili la idadi ya wavuvi na idadi ya watumiaji wa rasilimali hizo za baharini haliendi sambamba na uzalishaji na ukuaji wa rasilimali ziliopo baharini na kwa maana hiyo kuendelea na matumizi na uvunaji wa rasilimali hiyo bila ya utaratibu madhubuti wa kisheria wenye kuongoza na kuratibu matumizi bora na endelevu ya rasilimali za baharini haitakuwa sahihi hata kidogo. Ni vyema rasilimali hizo zilindwe na zitunzwe.

Mhe. Mwenyekiti, haya ndio madhumuni makubwa ya mswada huu ulio mbele yetu. Tunataka tuwe na sheria yenye kukabiliana na changamoto zilizopo ambazo ni uharibifu wa mazingira unaosababishwa na uvuvi haramu kama vile wa kutumia juya na baruti. Halikadhalika, uvuvi mwengine ambao unasababisha kuwaua samaki wachanga na mazalio ya samaki hao, au unabomoa matumbawe na makaazi ya samaki kama vile uvuvi wa kutumia nyavu ndogo, gesi, bunduki na utupa (sumu).

Mhe. Mwenyekiti, athari nyengine ambazo wakati mwengine zinapatikana katika matumizi mabaya ya fukwe zetu ni ujenzi wa jeti usiozingatia matokeo ya kimazingira ambayo athari zake kuonekana kwake zinachukua muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kudhibiti hali hii Taasisi inayohusika na utoaji wa vibali vya ujenzi wa jeti *(ZIPA)* inatakiwa ifanye utafiti wa kina na wa kitaalam zaidi ikiwa ni pamoja na kuzishirikisha Idara zote zinazohusika na maeneo hayo kabla ya kutoa kibali hicho kwa muombaji.

Mhe. Mwenyekiti, yaliyomo katika mswada huu yamezingatia udhibiti na uendelezaji wa Sekta ya Uvuvi, kama ilivyoainishwa katika sehemu ya tatu ya Mswada huu. Ambapo sehemu ya nne imehusisha utoaji wa Leseni kwa shughuli za Uvuvi na msisitizo na utaratibu kwa jambo hilo lipo kwenye kifungu cha 14 ikiwa ni pamoja na masharti ya jumla ya utoaji wa leseni kama

ilivyo katika kifungu kinachofuata cha 15. Aidha, kwa utaratibu huo wa matumizi ya bahari na rasilimali zake inatumika pia kupata kibali cha kufanya utafiti wa Kisayansi.

Mhe. Mwenyekiti, leseni kwa tafsiri yake haiishii kama ruhusa ya matumizi tu, bali pia ni moja ya chanzo cha mapato ambacho kitasaidia nchi katika kuongeza pato lake na kusaidia kuendeleza sekta hii ya Uvuvi.

Lakini jengine ni kwamba utoaji wa leseni endapo utaratibiwa vyema basi utatoa fursa ya kuwadhibiti na kuwajua wavuvi wote wenyeji na wageni na hii itasaidia kuelewa hata maeneo ambayo yanawekewa utaratibu kwa kuivuna rasilimali hiyo kwa muda maalum.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu vile vile umeanzisha kuwepo kwa Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari ambacho kitahusika na usimamizi endelevu wa maeneo yaliyodhibitiwa kwa mujibu wa sheria hii. Ufanisi wa kitengo hiki utaratibu vyema maeneo ya uhifadhi na kuyabakisha yakiwa na rasilimali endelevu. Hayo yameainishwa kwenye sehemu ya tano ya mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile lengo la sheria hii tunayoikusudia ni kuilinda rasilimali yetu hii ya bahari, basi adhabu kwa makosa yatakayotendeka kinyume na utaratibu wa maelekezo ya sheria hii watatiwa hatiani na adhabu zimetajwa kwenye sehemu ya sita.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu imeupitia mswada huu kifungu kwa kifungu na kukubaliana na Mhe. Waziri marekebisho kidogo kama tulivyoyaainisha kwenye karatasi tulizozigawa kwa Wajumbe.

Mhe. Mwenyekiti, kama kawaida yangu mara nyingi husisitiza kwamba kutunga sheria ni hatua moja lakini usimamizi ni jambo jengine. Lazima tuzisimamie vyema sheria zetu hizi tunazozitunga ili zilete maana halisi ya kutungwa kwake.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maoni hayo ya Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni naunga mkono mswada huu na kuwaomba Wajumbe wenzangu nao kuunga mkono hoja hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Assaa Othman Hamad (Waziri Kivuli wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira): Mhe. Mwenyekiti, nami niungane na wenzangu waliotangulia kwa kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako kwa kura nyingi za Wajumbe wa

Baraza hili tukufu kuwa Mwenyekiti wetu mwanamke wa mwaka huu 2010. Ni imani yangu utatuongoza kwa umahiri mkubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kunijaalia afya njema na kunipa wasaa wa kutoa maoni ya kambi yangu ya upinzani.

Mhe. Mwenyekiti, ili nisiwe mwizi wa fadhila napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kutoa mtazamo wa kambi ya upinzani.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuleta mswada huu wa kuziba nyufa za sheria ya mwaka 1988. Aidha, inatia matumaini kuona kuwa serikali inaanza kutambua na kuzilinda rasilimali bahari za nchi yetu kwa sababu mswada huu unaonesha dhahiri ya kuwa serikali inaanza kuwa makini katika kuzihifadhi rasilimali bahari zilizopo Zanzibar na sio kuziacha ziporwe ovyo na wageni huku wazalendo wakibaki kuwa mashuhuda.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha kuwa imechukua miaka mingi kidogo kwa serikali kugundua hii mali ya bahari tuliyokuwanayo yaani *Territorial Waters* pamoja na *Exclusive Economic Zone* ya maili 200 ya bahari ni urithi wa mali yetu Wazanzibari. Wakati mwengine meli za nje zimekuwa zikija kuvua kwa kadri wanavyopenda wenyewe kwenye bahari yetu bila ya kizuizi chochote.

Mhe. Mwenyekiti, ni matumaini yangu kuwa sheria hii sasa itajitahidi kuzuia hayo si kwa kuweka tu sheria nzuri, bali kwa serikali kuweka mkazo katika utekelezaji wa sheria hii kwa kuwapatia vifaa vya kisasa hata kikosi chetu cha KMKM ikiwemo na mafuta ya kufanya *patrol*.

Mhe. Mwenyekiti, kumekuwepo na malalamiko mengi juu ya matumizi ya bahari kwa ajili ya uvuvi baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Kimsingi yapo maoni kuwa hakuna mipaka maalum inayoeleweka baharini ya *Exclusive Economic Zone* baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Kwa hiyo, jambo hili lisiposhughulikiwa vyema na mapema linaweza kusababisha migogoro isiyo ya lazima kwa kuwa wavuvi wataombewa leseni Zanzibar wanaweza kuzuiliwa au kukataliwa kukata leseni upya Tanzania Bara kwa ajili ya kuvua maeneo hayo ya bahari kuu.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar sio *signatory* wa *International Treaties* ya *Convention*, bali Tanzania Bara ndio husaini *convention* hizo kwa jina la Tanzania. Kwa bahati mbaya wakati mwengine zile *convention* ambazo

Tanzania Bara inazisaini kwa niaba ya Tanzania huwa zinahusu mambo ambayo si ya Muungano.

Kwa mfano, Tanzania Bara ni *signatory* wa *convention* ya *International Maritime Organization*. Kama ni *signatory* wa *Maritime Organization* imeingia kusaini kama ni *United Republic of Tanzania*.

Katika *convention* hiyo kumetolewa tafsiri nzuri kabisa baina ya Bara na visiwani, *Territorial Waters* na *Exclusive Economic Zone*. Lakini sasa wenzetu huwa hawaizingatii Zanzibar katika mchakato wao.

Kwa mfano, Tanzania Bara wao wamepitisha Sheria ya Uvuvi Nam. 22 ya mwaka 2003 na kamwe hawakuzingatia Zanzibar katika kupanga hizo *Territorial Waters* na *Exclusive Economic Zone*.

Mhe. Mwenyekiti, kamwe hatuwezi kuendeleza Sekta ya Uvuvi bila hasa kujua mambo ya msingi kama vile kutambua aina ya jamii ya samaki iliyopo katika nchi yetu na vile vile ni kiasi gani cha samaki tulionao. Hili ndio suala la msingi litakaloweza kutuhakikishia kwamba tunazungumzia kitu ambacho tunakielewa sote.

Sasa hivi kuna baadhi ya aina ya samaki ambao wanapotea bila ya kuwa kwenye kumbukumbu yoyote ya wataalam. Kuna baadhi ya samaki pengine walikuwa wanapatikana zaidi Zanzibar na hawapatikani kwengineko, lakini hakuna mipango yoyote ya kutafiti na kuhifadhi urithi wa kimaumbile usipotee. Lakini hata takwimu zake pia hazipo.

Nadhani itakuwa ni hatari kama tutadhani kwamba tunaweza tu tukafanya mambo ya kuua samaki bila ya serikali kuweka mambo ya msingi nayo ni *stresses in identification and how much can be harvested.* Najua mambo haya yanagharimu fedha, lakini ni muhimu mno katika kuhakikisha kwamba hii rasilimali yetu ya uvuvi tunaivuna kwa njia zilizo endelevu na kwa maslahi ya watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi ni miongoni mwa sekta za uzalishaji ambayo ni muhimu sana katika nchi yetu. Sekta hii kama zilivyo sekta za Kilimo na Mifugo inawahusisha wananchi wengi na kutoa ajira, lishe, kipato na kuchangia hata pato la taifa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sheria hii tofauti na ile ya wenzetu wa Tanzania Bara haianzishi mfuko wa uvuvi. Kwa vyovyote vile nionavyo ni kuwa utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Uvuvi yamelengwa kufanyika kwa kuzingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, Dira ya Taifa ya

mwaka 2020, Malengo ya Milenia, pamoja na utekelezaji wa MKUZA. Kwa kutambua mchango unaoweza kutolewa na Sekta ya Uvuvi nchini katika kuwapunguzia wananchi umaskini na kuongeza pato la uchumi wetu Ilani ya CCM ya mwaka 2005 imetamka pamoja na mambo mengine kuwa itatengeneza mazingira mazuri yatakayosaidia upatikanaji wa zana za kisasa za uvuvi bila ya vikwazo.

Sasa swali linajitokeza. Hivi tutawezaje kuandaa mazingira mazuri bila ya kuwa na mfuko maalum wa uvuvi utakaowasaidia wavuvi kukopa ili kununulia vifaa vya uvuvi. Tunafahamu sote kwamba masharti na taratibu za mikopo kwa benki nyingi hazimpi nafasi mvuvi kukopa. Watu wengi wanafahamu benki anakopa mkulima kwa kuwa yeye ana shamba la kuweka rehani, lakini mvuvi hana nafasi kwa kuwa yeye hawezi kuweka rehani kipande cha bahari.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya ukosefu wa mitaji baada ya kuwaimarisha wavuvi ambao ndio kazi yao ya asili waendelee kuvua, tunaweza kuwafanya wawe manamba katika vyombo vya watu wenye pesa ambao asili yao sio kuvua. Kwa hiyo, kuwe na utaratibu wa kuwawezesha wavuvi wasio na uwezo mkubwa ili wakomboke. Tuwatengenezee mazingira wavuvi wetu wadogo wadogo waweze kuondokana na umaskini wa kumiliki vyombo vya kisasa.

Mhe. Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 inaelekeza Sekta ya Uvuvi kutekeleza maeneo muhimu ambayo ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wavuvi kutumia maarifa ya kisasa ya uvuvi ili kuongeza ufanisi na mapato yao. Lakini tatizo liliopo ni kuwa Zanzibar hadi sasa hatuna chuo cha uvuvi na wala sheria hii tunayoijadili leo haikusudii kuanzisha chuo cha uvuvi. Hivi tutawezaje kuimarisha na kukuza Sekta ya Uvuvi wakati hatuna hata chuo kimoja kinachotoa taaluma katika fani zinazohusiana na uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu Bara wanacho Chuo cha Uvuvi Mbegani. Tunashauri kuwa na sisi tuanzishe chuo cha uvuvi ambacho kitasaidia pamoja n mambo mengine katika kutoa wavuvi wazuri na ambao wataweza kusaidia katika kuimarisha Sekta ya Uvuvi. Nadhani hiyo itakuwa ni sehemu nzuri ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, udhibiti wa usalama na ubora wa mazao ya uvuvi pamoja na masoko ni muhimu kusimamiwa kikamilifu ili kulinda afya ya walaji, thamani ya mazao ya uvuvi na kudhibiti viwango vya ubora vinavyokidhi mahitaji ya soko.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa maoni hayo ya jumla kuhusu mswada, napenda niende kwenye baadhi ya vifungu vya mswada. Kifungu cha 2 kinatamka wazi kuwa sheria hii tunayoitunga leo itatumika Zanzibar.

Tunakubali kuwa kanuni za uandishi mzuri wa sheria *(good legislative drafting)*zinaelekeza kuwa sheria ziandikwe kwa uwazi juu ya ukomo na matumizi *(scope and application).* Kifungu kinachohusu ukomo wa matumizi ya sheria kinasaidia kufahamu maeneo ambayo sheria inayotungwa inakusudiwa kutumika.

Hata hivyo, imekuwa si jambo la kawaida sana kwa sheria tunazozitunga katika Baraza kuweka kifungu cha matumizi kama hiki cha 2 kilicho katika mswada huu. Sababu kubwa ni kuwa kifungu cha 78 cha Katiba ya Zanzibar inaweka wazi kuwa nguvu za kutunga sheria kwa mambo yote yasiyokuwa ya muungano katika Zanzibar yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni kusema kwamba mamlaka ya Baraza kutunga sheria ni kwa mambo ambayo si ya Muungano tena kwa ajili ya Zanzibar tu. Kwa bahati nzuri uvuvi si katika mambo ya Muungano kwa kuwa jambo hili halimo kwenye Mkataba wa Muungano wala katika nyongeza ya kwanza iliyo katika ya Muungano inayohusu mambo ya Muungano. Sasa sheria haikulazimika sana kutamka kuwa itatumika Zanzibar kwa kuwa jambo hilo halina mjadala.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu Tanzania Bara wana sheria mbili zinazohusu uvuvi. Sheria ya kwanza inaitwa *Fisheries Act, No 22 of 2003* na Sheria ya pili inaitwa *The Deep Sea Fishing Authority Act*, No 1 of 1998. Kambi yetu haina tatizo sana na sheria ya mwaka 2003 bali zaidi ile ya mwaka 1998. Kwa namna ilivyoandikwa, tunawasi wasi mkubwa kwamba utekelezaji wa sheria ya *Deep Sea Fishing Authority* itaiviza sheria hii tunayokusudia kuipitisha hapa leo.

Kama nilivyosema kuwa hadi sasa hakuna mipaka inayoeleweka ya *Exclusive Economic Zones* baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Sheria hii tunayoipitisha katika kifungu cha 14 kinaeleza kuwa chombo chochote kitachotaka kuvua katika ukanda maalum wa kiuchumi wa *Zanzibar Exclusive Economic Zones* lazima kikatiwe leseni Zanzibar. Sheria 1 ya 1998 nayo katika kifungu cha 4 inasema kuwa leseni za vyombo vyote vinavyotaka kuvua katika *Exclusive Economic Zone* ya *United Republic* ni lazima vipewe leseni Tanzania Bara. Sasa jambo hili halitoleta migongano katika utekelezaji wake? Leseni ikakatwe wapi Bara au Zanzibar?

Mhe. Mwenyekiti, zaidi ya hayo, sheria ya 1998 imeweka adhabu kwa mtu ambaye atavua katika eneo la *exclusive economic zones* bila ya kupewa leseni na Mamlaka ya Tanzania Bara. Sasa hatuoni kuwa mvuvi anaweza kukata leseni yake Zanzibar lakini akajikuta anapewa adhabu kwa mujibu wa sheria ya 1998 kwa kuvua katika *Exclusive Economic Zones ya United Republic* bila ya kupewa leseni na Mamlaka ya Tanzania Bara?

Aidha, Waziri wa Bara wa Uvuvi ndiye mwenye mamlaka ya kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi kwa rufani zote zinazohusu mtu kunyimwa leseni au mambo ya uvuvi katika ukanda wa bahari katika *United Republic*. Neno Waziri katika sheria hiyo limetafsiriwa kuwa ni Waziri mwenye dhamana ya mambo ya uvuvi katika Jamhuri ya Muungano. Kama tunavyojuwa sote kuwa uvuvi si katika mambo ya Muungano sasa mambo haya yatakuwaje na sheria hii tunayoipitisha itasaidia vipi kutatuwa matatizo haya?

Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 11 cha Mswada kinaeleza kuwa Waziri "atadhibiti" uvuvi wa kienyeji na wa kiviwanda". Kwa bahati mbaya Mswada haukufafanuwa atadhibiti vipi uvuvi huo lakini shaka inayojitokeza ni kuwa hivi akiamua kudhibiti uvuvi wa kienyeji hii maana yake wenyeji hawatakuwa na haki ya kuvua katika bahari inayowazunguka? Hivi ikiwa uvuvi wa kienyeji na wa kiviwanda tutaudhibiti kwa maana usiweko?

Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 14 cha Mswada kinaeleza kuwa Mkurugenzi atamteuwa Afisa Leseni ambaye ndiye atakayetowa leseni ya chombo cha uvuvi. Hata hivyo, Kifungu hiki hakikwenda mbali zaidi kuelezea kuwa endapo Afisa leseni atakataa kutoa leseni kwa chombo chochote cha uvuvi na ikawa mvuvi aliyenyimwa leseni hakuridhika na maamuzi hayo, basi ni wapi atakata rufaa kupinga maamuzi ya Afisa Leseni. Sheria ilitakiwa iweke kifungu kwamba "endapo mtu yeyote hatoridhika na maamuzi ya kunyimwa leseni na Afisa Leseni basi atakata rufaa kwa Waziri kupinga kunyimwa huko".

Aidha, Kifungu cha 15(6) kinaeleza kuwa kila chombo ambacho kimepewa leseni chini ya sheria hii kitawekewa alama kwa utaratibu utakaoelezwa. Suala linajitokeza ni kuwa huo utaratibu utakaowekwa utawekwa na nani na atauweka wapi. Sisi tunadhani kifungu hiki kingeweka wazi ikiwa utaratibu utawekwa na waziri kupitia kanuni atakazozitunga au vyenginevyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kusimama hapa nikiwa ni mzima. Pili nikushukuru wewe kwa kuchaguliwa na pia leo ukiwa katika kiti cha Mhe. Mwenyekiti, umekaa vizuri tu.

Mhe. Mwenyekiti, tatu nimshukuru Mkurugenzi wa Uvuvi kwa kazi zake nzuri na jinsi anavyozimudu, Mwenyezi Mungu amsaidie na azidi kumuongoza.

Mhe. Mwenyekiti, ninakuja katika mchango, lakini itakuwa michango yangu ni midogo tu kwa vile ni mjumbe wa kamati hii na mimi sina budi nichangie kwa sehemu zile ambazo nazielewa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu unaonesha umelenga kwa wavuvi tu, lakini haukulenga hasa kwa wale wanaoleta zile zana za uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, tunao uvuvi wetu huu wa juya, uvuvi mwengine wa baruti na uvuvi mwengine wa kutumia bunduki pamoja na gesi. Lakini tukiangalia uvuvi wa gesi, juya na baruti huu ni uvuvi haramu, tena nakubali kuwa ni uvuvi haramu. Kwa sababu uvuvi huu wa juya ni uvuvi ambao unakokota na unakokoa kilichomo na kisichokuwemo, huvua mpaka samaki wachanga ambao hawajafika hata umri wa kuvuliwa. Mhe. Mwenyekiti huu ni uvuvi haramu tena ni uvuvi mbaya.

Mhe. Mwenyekiti, cha kusikitisha ni kwamba hawa wanaoleta hizi zana za kuvulia, kwanza ndio wanaohitajika kuambiwa kwamba hizi zana hazifaa kwa uvuvi huu. Kwa hivyo, ningeomba kwanza tupige vita kwanza kwa wale wanaozileta hizi zana ili wananchi wetu waelewe kwamba huu uvuvi kweli ni haramu. Kwa sababu ikiwa zana zitakuwa hazimo madukani basi itakuwa na ule uvuvi watu hawavui.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 17 kifungu cha 22(1) kinachosema kwamba;

Kifungu cha 22(1)

> "mtu yeyote hatoruhusiwa kukamata, kushusha, kuuza, kupokea au kumiliki samaki yoyote mwenye ukubwa wa chini kuliko kiwango kilichoelezwa kwa aina ile ya samaki".

Mhe. Mwenyekiti, kwa hapa kidogo nitakuwa na wasi wasi, kwa sababu wapo samaki wengine ambao huwa ni umri wao au vimo vyao. Lakini leo mtu atakapomvua samaki yule atakapofika juu tu anaweza kukamatwa na hali ya kuwa samaki yule tayari keshatimia umri wa kuvuliwa. Je, Mhe. Mwenyekiti, hii itakuwaje?

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye uvuvi wa gesi ambao ni haramu, uvuvi huu sio haramu tu bali hata kwa maisha ya binadamu mwenyewe ni tatizo. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, mvuvi yule anapozamia pamoja na gesi, basi gesi ile anapofika nayo chini pindi ikimalizikia huko chini basi hafiki juu tena. Kwa hivyo, tusiangalie tu kwamba ni uvuvi haramu, bali ni uvuvi hatari hata katika maisha ya binadamu.

Mhe. Mwenyekiti, siku nyengine hufika kule chini kuna haya matumbawe, basi kwa bahati mvuvi yule akaganda na matumbawe na gesi ikamuishia, basi tayari

mvuvi yule haji juu na hatimaye watu husema mtu huyo kafa na kaliwa na samaki au kaliwa na shetani. Hii ni hatari kubwa sana.

Kwa hivyo, mimi nadhani suala hili la uvuvi tungeliangalia sana. Hizi njia za uvuvi kama uvuvi wa juya, baruti na gesi huu una matatizo na ni haramu kwa watu wetu kuvua. Lakini kwanza tungewaangalia wananchi wetu wenye shughuli hii ya kuvua, kwa kweli wana matatizo na wengi wao ni wavuvi na hutegemea pwani. Je, Mhe. Mwenyekiti, tutawaeleza nini wananchi wetu?

Mimi naomba kwanza tungewaeleza wananchi wetu na tukawapa elimu na taaluma zaidi ili waelewe nini uvuvi wa haramu na nini kinacho athiri kwenye samaki wetu wadogo wadogo.

Mhe. Mwenyekiti, wavuvi wetu hivi sasa watakuwa katika mtihani mkubwa sana, kwa sababu wengi wao wamezoea pwani, zaidi sehemu za vijijini na wengi wao kazi zao zote ni za pwani. Sasa Mhe. Mwenyekiti, tukisema tunapiga marufuku uvivi huu itakuwa hatujawasaidia. Mimi nadhani tungewapa elimu na tukawapa taaluma wakakaa wenyewe wakafikiri na kutafakari. Kwa sababu tukisema kwamba sisi huku tunajua basi wao wanajua zaidi. Leo tutatunga sheria hapa na hatimaye tutaikiuka hata sisi wenyewe, lakini ukifika kule atakuambia sheria zenu mmetunga wenyewe huko, leo mnatuambia kwamba hiki ni haramu na hiki kinafanyika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mchango mkubwa nimalizie hapo, ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi).*

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nitumie fursa hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia jioni hii kutupa uwezo tukaweza kukutana hapa kwa lengo la kuendeleza masuala muhimu yahusuyo maendeleo ya nchi yetu.

Pili Mhe. Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwa kukupongeza kwa dhati kabisa kwa ulivyoteuliwa katika Baraza hili na inawezekana ikawa ni mwanamke wa kwanza kabisa kukalia kiti hicho.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Bi Zainabu Omar Moh'd keshakikalia hiki kiti.

Mhe. Omar Ali Shehe: Ahsante, alipokuwa amekikalia Mhe. Zainab kipindi hicho sisi wengine tulikuwa hatupo humu, basi nikudhihirisha tu kwamba na wanawake nao wanaweza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu sio mkubwa sana, lakini nataka nianze na kutoa pongezi kwa wizara na serikali kwa jumla kwa kuleta mswada huu katika kipindi hiki.

Vile vile niwapongeze kwa mafunzo mliyotupa juzi, niipongeze wizara juzi Jumapili kwa kutupatia elimu kubwa sana. Hususan nimpongeze Mkurugenzi wa Uvuvi. Kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwamba Mkurugenzi ndugu Mussa ni hazina kwa taifa letu. Kwa hivyo, nimpongeze kwa dhati kwa jinsi anavyoendelea kusimamia shughuli zake na kwa ile elimu kubwa aliyotupatia na ni elimu ambayo kwa kweli imetupunguzia hoja nyingi katika mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kwamba mswada huu umechelewa, kwa sababu umekuja wakati ambao hali ya mazingira katika bahari imechafuliwa mno. Vitu ambavyo katika visiwa vyetu ni muhimu sana kuviangalia ni viwili.

Kwanza mazingira ya nchi kavu na vile vile kwa sababu ni visiwa tunahitaji tuwe na mkakati maalum katika kulinda mazingira ya bahari. Mazingira ya bahari kwa kuwa wananchi wetu wengi ni wavuvi na tumezungukwa na bahari na wananchi wetu wengi wanaitegemea bahari katika maisha yao ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, ili bahari iendelee kuwapa tija wananchi ni lazima bahari iwe na mazao endelevu. Sasa hali ya bahari yetu mazingira yake yamechafuliwa mno, uchafuzi ambao umepelekea upatikanaji wa mazao ya baharini kwa hivi sasa kuwa ni mgumu. Wavuvi zamani walikuwa hawendi masafa ya mbali kutafuta mazao ya baharini kama vile samaki, lakini leo inakuwa ni tatizo kweli kweli.

Mhe. Mwenyekiti, yote hayo yanasababishwa na hali ya watu wetu kuharibu kwa makusudi kabisa mazingira ya bahari. Kitu ambacho kama serikali haikuwa na mkakati maalum na madhubuti wa kuwa na sheria ya kulinda bahari yetu, basi si muda mrefu Mhe. Mwenyekiti, hali ya maisha ya wananchi wetu ambao kwa sehemu kubwa wanategemea bahari itakuwa ni mbaya sana. Maana waliokuwa wanategemea uvuvi kwa maisha yao ya kila siku itabidi warudi juu kwenye kilimo, na wanaotegemea kilimo na kilimo nacho kikishachafuka itabidi wakimbilie kwenye bahari. Sasa hapo kutakuwa kuna mtihani mkubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi kwetu kule siku moja nilimkutia mvuvi kaenda baharini muda wa wiki nzima hapati kitu, ilikuwa kazi yake ni kuchokoa pweza. Kwa hivyo, akasema kwa mtindo ule wa kwenda na vijiti kuchokoa haumpi manufaa, siku hiyo akaenda na mtaimbo na nyumba yoyote aliyokuwa anaiona ilikuwa ni kuangamiza tu, mkubwa mdogo, mpevu au mchanga

twende. Siku hiyo aliyokwenda na mtaimbo kwa kweli alipata, lakini aliharibu kwa kiasi kikubwa. Hili Mhe. Mwenyekiti, nasema sio utani ni kitu ambacho binafsi nilikishuhudia. Kwa hivyo, tunawashukuru wizara sana kwa kuleta sheria hii, japokuwa imechelewa lakini itatusaidia angalau basi kulinda hiki kilichobakia.

Mhe. Mwenyekiti, nasema katika kitu cha msingi kabisa. Wenzangu walieleza hapa kwamba sheria ni kitu kimoja, lakini utekelezaji wa sheria ni kitu chengine na kuna kitu cha tatu nacho ni elimu ni jambo la tatu. Bila ya wananchi wetu hususan wanaokaa katika sehemu na wanaotegemea uvuvi bila ya kupewa elimu, basi itakuwa siku zote ni ugomvi na serikali pamoja na sheria hii ambayo tunaikusudia kuipitisha, na mimi naamini hivyo.

Pamoja na kuwatetea wavuvi, lakini baada ya kuelimishwa sisi waheshimiwa, kwa kweli tulifahamu na ninaamini kwa mwananchi ambaye ana akili timamu na kwa kuwa wananchi wetu wote takriban wana akili timamu basi watakapoelimishwa na wao watafahamu.

Kwa hivyo, kitu muhimu Mhe. Mwenyekiti, ni wizara pamoja na idara inayohusika kutoa elimu katika programu yao ambayo wanatakiwa waiwekee kipaumbele kabisa ni suala la elimu kwa wavuvi. Naamini kabisa kama wavuvi wetu wataelimishwa basi wataelimika kwa msingi huo sheria hii itakuwa haina shida sana katika utekelezaji wake, maana sheria inakuwa na matata pale ambapo walengwa wakiwa hawajafahamu, basi pale inakuwa pana mvutano na patakapokuwa na mvutano sasa itabidi utumiaji wa sheria hii ndio uwekwe vizuri. Lakini ikiwa wananchi wataelimika basi sheria itakuwa haina kazi kubwa sana ya kutoa mambo ya adhabu na vitu vingine.

Mhe. Mwenyekiti, tunachokizungumzia ni uharibifu, lakini katika sheria kadiri nilivyoiangalia haraka haraka kuna uharibifu wanaotumia mabunduki, kuna uharibifu wanaotumia magesi na kuna waharibifu wanaotumia nyavu hizi za kukokota na mambo kadhaa. Katika sheria humu kuna kipengele kimoja nilikiona kwamba vitakapokutwa vitu hivi kwenye chombo ndipo pale ambapo itahesabika kwamba mtu huyo kahalifu sheria.

Kwa hivyo, nadhani tusifike huko kwa sababu vitu hivi vingi ni vya kuagiza, lakini kwa nini sheria haikumtambua huyu muagizaji, kwa nini hatuwezi tukapambana na uagiziaji na tukapiga marufuku huu uagiziaji. Kama hatuna uwezo wa kupiga marufuku basi tufike pahala tuweke vikwazo ambapo hata muagiziaji atashindwa kuagiza.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni tulikuwa tunazungumzia suala la utumiaji wa misumeno ya moto na tukafika pahala serikali ikatuambia kwamba kuna utaratibu maalum kama sikosei kuipiga marufuku hii misumeno ya moto. Sasa kama hivyo ndivyo, kwa nini sheria haitambui nayo kupiga marufuku uingizaji wa vitu hivi. Kwa sababu nadhani hilo ni jambo la msingi la kuweza kupiga marufuku uingizaji wa vitu hivi, kulikoni kuviachia vikaingia ndani ya nchi baadae ndio tukavivizia wakati wa utumiaji.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niseme kwamba kifungu cha 22 kimeelezea kitendo cha kukamata samaki wachanga waliochini ya hali ya ukuaji wao, kitendo hiki kinapigwa marufuku. Lakini Mhe. Mwenyekiti, sheria hii imekubali kwamba kuna suala la ufugaji wa samaki.

Sasa naamini kwamba kitendo cha kupiga marufuku ukamataji wa samaki wachanga, lakini sheria ikaruhusu kitendo cha ufugaji. Kwa sababu ili samaki umfuge ni lazima umkamate tena umkamate katika hali ya uchanga. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anifafanulie hili.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza awali kwamba mchango wangu sio mkubwa ni mdogo sana na baada ya kupewa elimu nikaelimika vya kutosha, kitendo ambacho mimi binafsi naahidi kwamba nitakuwa askari nambari moja wa kuilinda sheria hii kwa kuelimisha.

Vile vile wakati mwengine wavuvi wangu wa maeneo ya Wesha, kwa sababu katika jimbo langu ninao wavuvi wengi katika maeneo ya Wesha, watakapokuwa na haja maalum ya kupatiwa vifaa na kupatiwa baadhi ya mahitaji, basi naahidi kwamba nitakuwa mstari wa mbele kumwendea Waziri, Naibu Waziri pamoja na Mkurugenzi ili katika kuisimamia sheria hii na wao wafaidike na wafaidike na hali yao ya kuwa na bahari katika eneo lile.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naomba niseme kwamba kwa niaba ya wananchi wangu na mimi naiunga mkono sheria hii kwa asilimia mia kwa mia, ahsante.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu kukupongeza katika kiti hicho ulichokikalia na tukutakie kila la heri, yale yote ambayo yanawajibika uweze kuyakamilisha.

Mhe. Mwenyekiti, pili nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote ambao walishiriki katika kuitayarisha sheria hii ambayo imesema kwamba sheria hii katika madhumuni na sababu imesema kwamba sheria hii nambari 8 ya mwaka 1988 imepitwa na wakati na sasa hivi tunatengeneza sheria mpya ambayo itakwenda na wakati. Hilo nalishukuru,

wenzangu wamesema wamechelewa, lakini waswahili wanasema kawia ufike, nadhani imekuja katika kipindi kizuri na sisi kama wahusika kwa upande mmoja tutasaidia katika kuifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi jimbo langu eneo kubwa linatumika na ukanda wa pwani, kuanzia Bububu, Fuji mpaka Nyanjale Kiombamvua eneo lote ni la bahari na ninao wavuvi wengi hata mimi nimeshawahi kuvua, lakini kipindi hicho tena nilikuwa sijapata sheria yoyote ilikuwa tunavua tu. Lakini sasa hivi kila tukienda mbele yale ambayo yote yanaleta matatizo yanawekewa utaratibu uliokuwa mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze pia serikali kwa kuliona hili, kwa sababu sheria hii kama tutaisimamia basi pia itaongeza mapato ya serikali na itaongeza kwa njia mbili kubwa. Kwanza ni kukata leseni za uvuvi, lakini pia leseni za vyombo. Sasa hayo mawili yataongeza katika kutunisha mfuko wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii ikishapitishwa pia imefungua milango wazi ya kuita wawekezaji, kwa sababu hapa kwetu uwekezaji mkubwa tunakimbilia kwenye biashara za maduka na mahoteli. Lakini nadhani ikijulikana sheria hii na wenzetu wawekezaji na tukawatafuta wakaja kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu na tukaweza kuneemeka na sisi hapa petu.

Pia nashukuru kwamba katika maandalizi ya sheria hii tunaambiwa kwamba wameshirikishwa wenyewe wahusika, wavuvi, wenyeviti wa kamati za uvuvi na kwa sehemu zote mbili Unguja na Pemba. Tunashukuru na tunaomba kwamba tuipongeze wizara kwa jitihada iliyofanya, lakini pamoja na hayo bado wizara isichoke katika kutoa taaluma kwa sababu ukimchukua mwenyekiti wa kikundi pengine katika kitongoji kimoja, inawezekana pengine wavuvi wengine wasipate hiyo taaluma, lakini nadhani kazi iendelee kupitia vikundi wavuvi wote waweze kufahamu sheria.

Kwa sababu wenzetu wengi wanaokwenda baharini huwa wanakwenda kutafuta riziki na sio wengi wanaosema watafute kitabu cha sheria nisome, sidhani kama wako wanaofanya hivyo. Kwa hivyo, nadhani itakuwa ni jukumu letu kutoa taaluma hii ili wenzetu sheria hii isiwakwaze, waweze kujua hili linatakiwa na hili halitakiwi, hili la kufanya na hili tusifanye.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea baada ya dibaji hiyo sasa niende kwenye mswada wenyewe. Sina mchango mkubwa kwa sababu na mimi ni mjumbe wa kamati, tayari nimeshachangia, lakini wananchi wangu wameniambia tuna wasi wasi wa mambo mswada ukiletwa rasmi basi ukatusemee. Kwa hivyo, na mimi nashukuru na nitajaribu kuzungumza kidogo kidogo ili tuweze kufahamiana.

Kwanza nije ukurasa wa 18 katika kifungu 24, katika kifungu cha pembeni ambacho kinasema; “Samaki wanaokamatwa wanaweza kuuzwa”. Sasa naomba ninukuu halafu nitowe maelezo yangu juu ya suala hili, kifungu 24 kinasema hivi;

Kifungu cha 24

> “Samaki au kitu chochote kinachoharibika kilichokamatwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 23, kinaweza kuuzwa katika mnada kwa maelezo ya Mkurugenzi na mapato yatakayopatikana yatahifadhiwa katika mfuko mkuu wa serikali”.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani hii si mbaya sana, lakini nahisi tunafanayakazi ambayo si yetu. Kwa sababu kwanza mtu ukimkamata na kosa jambo la mwanzo umpeleke Kituo cha Polisi na kule ndiko kwenye utaratibu wa kuanza kufungua kesi tena wanao utaratibu wao.

Kwa hivyo, ningeshauri kwamba labda hivi sasa taasisi hii inayohusika na mambo haya kwa kuwa wanapata wafadhili wengi. Nadhani ni vyema wangejenga sehemu moja ya jogofu ya kuweza kuweka baridi pale kikikamatwa kitu kama hiki usiku na pengine mpaka kufika asubuhi kitakuwa kimeshaharibika kwa ajili ya kupelekwa polisi, basi kikahifadhiwa pale na kusubiri muda, lakini mtu au mtuhumiwa akapelekwa kabisa polisi, atakaa kule na kupumzika na wale samaki watahifadhiwa pahala. Wakati wa kuandika maelezo basi wanakwenda kule na kuonekana kile kitu.

Kutokana na hali hii nafikiri ushauri wangu utakuwa ni mzuri, kwamba masuala haya tuwaachie Mahakama, ili kuondosha utata baadaye. Lakini kama wataalamu wameona kwamba hili halina tatizo, basi mawazo hayo nimepewa na wananchi wangu kama itawezekana hivyo ni vyema kutengeza eneo maalum la baridi, kikipatikana kitu cha kuharibika na utaratibu haujatima kwenda Mahakamani kinahifadhiwa, muda ukifika kinapelekwa Mahakamani na kutolewa uamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kama utaratibu huo utakuwa mgumu na uwezo haupo na tuanze hivi pia sina mashaka makubwa. Isipokuwa huo ni ushauri kama itawezekana Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho na baada ya kuzungumza na watendaji ikiwa litawezekana, basi atatueleza na tunaweza kubadilisha kidogo.

Nikiondoka hapo niende kwenye Sehemu ya Sita Makosa na Adhabu katika kifungu cha 28, kifungu cha pembeni adhabu ya kuvua kwa kutumia baruti na vitu vya sumu. Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu na baadaye nitoe maelezo.

Kifungu cha 28 kinasema hivi:-

> "Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti yoyote ya kifungu cha 20 cha sheria hii, atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atastahili kutozwa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiozidi shilingi milioni 10 au kifungo cha muda usiopungua miezi mitatu na usiozidi miaka mitano au adhabu zote mbili faini na kifungo".

Mhe. Mwenyekiti, si jambo baya mtu kufanya kosa na kuweza kupewa adhabu, lakini tuangalie ukubwa wa kosa lenyewe vile vile. Kwa sababu hapa imezungumziwa uvuvi wa baruti na sumu na wenzangu wamezungumza hapa kwamba hivi sasa wavuvi wengi walikuwa wakitumia masuala haya na sasa linaondoshwa kabisa kisheria. Kwa kuwa bado wengine watakuwa sheria hawajaipata uzuri, basi inaweza mambo haya yakawakumba na baadaye yakawa matatizo makubwa.

Vile vile kama mtu wa kawaida anayo baruti na wengine wanao uwezo mkubwa kuliko yule, lakini wote wamaekewa adhabu moja. Kwa hivyo, ninashauri kwamba pengine ingeelezwa baruti hii mtu anakutwa nayo kwenye maeneo gain? Kwa sababu wako wengine wanavua kwenye bahari kubwa huko na wengine wanaweza kwenda maji madogo tu.

Nafikiri ni vyema ikafanywa tofauti baina ya yule mwenye kwenda bahari kubwa na kutumia vyombo vikubwa zaidi na huyu ambaye ni mnyonge wa Mungu anayekwenda kutarazaki. Kwa hiyo, ingefanywa tofauti kidogo kama inawezekana kwa mawazo yangu na mawazo hayo pia nimesaidiwa na wenzangu.

Jambo jengine kwenye kifungu cha 20 ambalo limetajwa na wenzangu tayari wameshazungumza kwamba anaweza mtu akakutwa na hiyo sumu au mitego isiyoruhusiwa ndani ya chombo, tukisema ndani ya chombo kwamba tayari ameshaingia kwenye ngarawa au ngwanda anakwenda kuvua. Lakini vitu hivi kama walivyozungumza wenzangu kwamba inawezekana mtu akawanavyo nyumbani, sasa akitokanavyo nyumbani lazima atakwenda navyo kule.

Kwa hiyo, je katika utaratibu huu wa wauzaji pamoja na waagiziaji nao tutawafanya nini ili tuweze kuzuia suala hili, kwa sababu tukizuia kule vinakotoka nafikiri havitofika pwani wala kwenye chombo.

Kutokana na hali hiyo, niungane na wenzangu waliotangulia kwamba tungefanya utatatibu wa kupiga marufuku kwa wafanyabiashara kuagiza vitu hivi. Nadhani hii itasaidia katika kurahisisha utekelezaji wa utaratibu wa sheria yetu.

Mhe. Mwenyekiti, tunashauri hivyo kama itawezekana itasaidia, kwa sababu tukizuia kitu kisije nafikiri hakitatumika. Lakini tukikiacha kuja na halafu mtu akikitumia ndio pengine lawana na adhabu, basi itakuwa tunamsulubu mtu ambaye hakutegemea kutenda kosa. Sasa ikiwezekana na hilo basi mnaweza kuongeza kipengele kwamba kupiga marufuku kwamba vitu hivyo visije.

Nikiendelea na mchango wangu ambao si mkubwa sana nije kwenye ukurasa wa 20 kuhusu Msamaha. Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu.

> Kifungu cha 33 kinasema hivi:
>
> > "Waziri kwa maslahi ya taifa anaweza kutoa msamaha kwa mtu au taasisi yoyote juu ya sharti lolote la sheria hii au kanuni zitakazotungwa".

Mhe. Mwenyekiti, msamaha unakubalika na wala si jambo baya. Lakini sheria nyingi yamo haya na tunazungumza sana hapa kwamba wakati mwengine msamaha unapunguza sana mapato katika Mfuko wetu Mkuu wa Serikali. Kwa kweli Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha hutoa mifano mingi. Kwa mfano, kipindi kilichopita ni fedha nyingi sana zimesamehewa katika masuala mbali mbali.

Kwa hivyo, nataka nitoe indhari na hapa kwamba misamaha hii lazima itizamwe kwa mantiki na kuweza kuleta neema kwa nchi yetu, vyenginevyo wengi watajipenyeza kwenye misamaha na halafu tuweze kukosa mapato.

Mhe. Waziri namuomba kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba hizo kanuni kama utatunga ama kuna utaratibu wa sheria unaokuruhusu, lakini misamaha iwe na mipaka yake, tukisema msamaha tu hauna mpaka, basi mapato mengi yatapitia huko. Hili nashauri kama uwezekanao huo upo, wewe ni binaadamu unazo hekima pamoja na washauri unaweza kulifanya katika hali nzuri zaidi.

Sasa nije ukurasa wa 21 kifungu cha 35 kuhusu kutatua makosa nje ya Mahakama. Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu.

> Kifungu cha 35 kinasema hivi:
>
> > "Ikiwa mtu amefanya kosa kwa mujibu wa sheria hii na akakiri kwa maandishi kushughulikiwa kosa lake kwa mujibu wa kifungu hiki, Mkurugenzi anaweza:-
> >
> > > (a) Kumaliza kosa kwa kukubali malipo ya fedha yanayolingana na uharibifu uliosababishwa".

Kwa hivyo, hapa Mkurugenzi amapewa idhini kama mtuhumiwa mwenyewe hakutaka kupelekwa polisi alimalize yeye. Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mkurugenzi anayo mambo mengi na tukianza kumuongezea kazi inaweza kuwa tatizo, isipokuwa nikipewa maelezo mazuri zaidi siwezi kukataa, kwa sababu polisi wapo na Mahakama zipo na yeye afanye Mahakama ya nje, basi watu wote watakimbia kwenda Mahakamani na kwenda kwake.

Sasa itakuwa baada ya kufanya mambo ya kiafisi yanayohusika na utendaji kwenda mbele yeye atakuwa anahukumu kesi.

Mhe. Mwenyekiti, na hili naomba wataalamu wakae na walitizame tena kama litakuwa na tija juu ya sheria yetu basi liendelee, ikiwa kuna tatizo tuliondoe na hali ibaki kama kawaida kesi zote zipitie polisi na baadaye ziende Mahakamani na Mkurugenzi afanyekazi nyengine za kitaifa.

Mhe. Waziri nadhani mtakaa pamoja na wataalamu wako kwa ajili ya kulitafakari, kama itawezekana basi tuweze kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria yetu iweze kutekelezeka.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa nikimalizia mchango wangu nizungumzie kuhusu suala la mwani. Kwa kweli mwani unalimwa baharini na huko ndiko watu wanakovua, lakini hivi sasa kumekuwa na changamoto kubwa kamba mwani unalimwa maji makubwa na majina ya mwani wataalamu ndio wanayajua na mimi si mtaalamu wa mwani.

Kwa hivyo, ninashauri na zoezi hili likaende kidogo kidogo, kwa sababu si wengi wakulima wa mwani wakawa wanaume na kwenda maji mengi, kwani wakulima wengi wa mwani ni wanawake. Sasa kama kutakuwa na nyenzo za kusaidiwa na kufika huko maji makubwa basi tunashauri wizara isaidie, ili wanawake na wao wapate kuneemeka katika ulimaji wa mwani.

Kwa sababu sehemu nyingi za mashariki watu wengi wanalima mwani na wanapata kazi kubwa, kwa kuwa ardhi yao sehemu kubwa ni ya jiwe. Mhe. Mwenyekiti, naomba na hili lizingatiwe kwa manufaa ya wananchi wetu kuweza kufikia malengo yao waliyoyakusudia.

Mhe. mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo mfupi na mimi niliona nitie baraka pamoja na maagizo niliyopewa maagizo yangu. Kwa kumalizia naomba wenzangu tuuchangie mswada muhimu na umekuja kwa wakati muafaka. Kwa hiyo, naunga mkono mswada kwa asilimia mia moja *(Makofi)*.

Nakushukuru, ahsante sana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia jioni ya leo.

Mhe. Mwenyekiti, bahari ndio rasilimali kubwa au ni moja katika rasilimali kubwa tuliyonayo. Tumepita katika karne ya kuitizama bahari kama ni mwenzetu, lakini hatukujua mambo mengi kuhusina na bahari. Baada ya kipindi hicho kupita na kufikiria kwamba bahari ni shamba ambalo unalokwenda kuvuna bila ya kuliangalia basi kipindi hicho kimepita. Sasa tunavyoiangalia bahari tunaitizama kwamba ni shamba ambalo unaweza kwenda kuvuna, lakini ikiwa utalishughulikia.

Kwa hivyo, nafikiria kwamba jambo la mwanzo kabisa linalotakiwa, ili sheria hii na nyenginezo zinazokuja baadaye ni kutoa elimu na wala sio kwa wale wavuvi tu, lakini kutoa elimu kwa wananchi wote kwa jumla, ili kuweza kufahamu nini bahari.

Kwa kweli tunasafiri asubuhi na jioni na tunapitia huko baharini, lakini bado wengi hatujaifahamu bahari. Kwa hiyo, wito wangu wa mwanzo kwa Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti ni kwamba bado wizara yake inalo jukumu kubwa la kuimarisha taaluma ya bahari. Hilo la mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, pili ni jambo la kusikitisha, licha ya kuzungukwa na bahari yote hiyo inayoanza bahari ndogo ndogo mpaka tunaingia kwenye bahari kuu, bado mchango wa bahari katika pato la taifa kwa takwimu tulizozipata hivi karibuni kutokana na maandishi ya Benki Kuu ni asilimia 1.3 ya pato la taifa. Kwa maana ya kwamba uvuvi unachangia asilimia 1.3 ya pato la taifa.

Hii inaonesha kwamba tunayo misimamo miwili ambayo inayopingana, kwa nini inapigana na halafu tutapata chanzo chake kinatoka wapi? Kwanza tunasema bahari inavunwa sana, ndio maana tunaweka vizingiti vya kuhifadhi, lakini wakati huo huo inachangia pato dogo sana katika pato la taifa, yaani mchango wake ni mdogo sana. Kwa kweli hii inaonesha kwamba hatujafanya utafiti wa kutosha wa kuingia katika bahari kuu na kupata ile hazina tuliyonayo.

Suala hili lilidhihirishwa hata huko nyuma mimi binafsi Mhe. Mwenyekiti niliwahi kuuliza swali je katika hizi taratibu zote za bahari kuu sisi kama Zanzibar tumewahi kuingia mkataba na kampuni au watu wowote kwa ajili ya kutusaidia katika uvuvi wa habari kuu. Jibu lake kwa wakati huo ilikuwa bado sijui mpaka hivi sasa, labda Mhe. Waziri wakati wa kufanya majumuisho yake anaweza kutuambia.

Sasa swali ikiwa bahati kuu tunajua kwamba inayo hazina na ndiyo iliyotuzunguka tunachelewa nini kuingia mkataba na makampuni, ili wao wakapata chao na sisi tukapata chetu, badala ya kukiachia na pengine kuchukuliwa na wao tu kwa kupita na kuvua katika bahari ambayo sisi hatuna ulinzi mkubwa nayo.

Lakini wale tutakaoingia mkataba nao, kwa sababu wao watakuwa wameshakata leseni, yaani wanatoa na kuchangia, basi sisi itakuwa ni rahisi kuwafuatilia na wao pia watakuwa ni walinzi wa sehemu hiyo. Kwa sababu akiingia mwengine watakuwa na haki ya kusema kwamba anaingia kuvua bila ya leseni na hali ya kuwa wao wamekata leseni *(Makofi)*.

Kwa hivyo, wakati huu tunamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba aangalie sana tusichelewe kiasi hicho na kusubiri vibua tu na haki ya kuwa pengine nguru, jodari pamoja na samaki wengine mbali mbali wakubwa nadhani wapo huko.

Katika miaka ya 1980 niliwahi kuzungumza na mzee mmoja ambaye hivi sasa ni marehemu na Mwenyezi Mungu ampe safari njema, alikuwa akifanyakazi katika hii iliyoitwa *Fisheries* na kulikuwa na meli ndogo iliyorithiwa kutoka kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Meli ile ilikuwa na uwezo wa kufanya utafiti kwa kutumia nyenzo mbali mbali ya aina ya samaki waliopo hapa, katika miaka ile walisema kwamba waligundua kuwa kuna samaki wanao umri mpaka miaka 200 hawajawahi kuvuliwa hapa Zanzibar katika bahari kuu. Sasa inawezekana sisi tunashughulikia vibua wa mwaka mmoja au mmoja na nusu, lakini bado kuna samaki bahari kuu wenye umri kama huo *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba sheria hizi ziturahisishie kuweka utaratibu mzima wa kuitizama hii bahari, ndio madhumuni ya sheria. Kwa kweli ni kuweka utaratibu wa kuiangalia ile bahari, vipengele vyake pamoja na kufanya utaratibu na wananchi wetu kuweza kuufuata utaratibu ule. Lakini wakati ule ule na sisi kitaifa tutizame bahari ile inatupa faida kiasi gani katika kuongeza pato la taifa pamoja na *protein* kwa watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nalitaja hili sijui utaratibu wa hapa uko vipi? Kwa sababu sijakaa Ng'ambo, kwa hiyo utaratibu pamoja na mambo yao siyajui sana. Lakini kwenye vijijini vyetu Mhe. Mwenyekiti kuna hawa wanaotembeza samaki kwa masusu na wako wengine wanatembeza dagaa kwa pakacha.

Sasa kuna mtu mmoja ambaye ametembea siku moja na ikawa tunazungumza ilikuwa wakati wa jioni, aliniuliza hebu kisia lile dagaa liliomo kwenye

pakacha ile linaweza kufika kilo ngapi? Vile vile aliniambia umewahi kukisia ni watu wangapi wanaouziwa pakacha ile mpaka ikamaliza, yaani ni nyumba ngapi? Kwa hiyo, aliniambia ile ndio *kilogram* ya walaji wetu, yaani pakacha lina uzito wa *kilograms* 10 au 15 za dagaa, lakini anatembeza nyumba 20 au 30 ama 40. Kwa maana hiyo, ule ndio uwezo wa watu wetu kula kile kitoweo, pengine nusu kilo ya kitoweo inaliwa na watu 7 au 10 mpaka 15, yaani ndivyo wanavyotowea watu wetu na wala tusikatae *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tufikie wakati tuwe na kiwango cha kuwatizama watu wetu tuwalishe angalau *protein* kiasi gani kwa siku. Unajua unapozungumza na kumuona mtu basi mara moja unakumbuka kitu, kwa sababu nimemuona rafiki yangu Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Timu ya mwanzo ya madaktari wa Kitaliana iliyokuja pale Chakechake na hiyo ilitokezea kweli hasa na wala mimi siwezi kusema uongo Mhe. Mwenyekiti katika chombo kama hiki. Sasa walikwenda watu kwa ajili ya kusaidia watu damu, namshukuru sana Mhe. Waziri kwamba sasa ameweka Benki ya Damu, tena naomba sote tuichangie, ili iweze kufanikiwa *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, umuhimu wa ile Benki ya Damu inaueleza hivi sasa. Kwa hivyo, walipokwenda kupimwa wale, wakaambiwa nyinyi ndio mnakuja kusaidia wakati nyinyi wenyewe mnataka kusaidiwa. Daktari wa Kitaliana anawaambia kama nyinyi mnapima kwa ajili ya kumsaidia huyu mgonjwa wenu, basi tulieni na nyinyi tuwaite watu waje wakusaidieni *(Kicheko/Makofi)*.

Kwa sababu kitoweo kinaliwa kidogo, yaani tunakula chakula kingi kama vile wali au ugari lakini kitoweo kidogo cha kunyufua. Sasa bahari imetuzungumza basi ifike wakati tuangalie angalau kwa mtu mmoja ale robo kilo ya samaki, nadhani tunaweza kusema tupo pahala pazuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kujua kwamba tuongeze pato la taifa pamoja na kuongeza *protein* kwa watu wetu. Kuna ibara 2 ya mswada huu, napenda nitoe fikra yangu kama ile niliyoitoa wakati wa kamati, kwa sababu tunakua na tunataka suala hili liwe kubwa zaidi, basi ningelitegemea katika kipindi hiki cha kuleta mageuzi haya ya sheria hii mpya basi idara hii ikawa mamlaka.

Idara hii hivi sasa inajihisi ni idara, lakini masuala yake ni ya mamlaka. Kwa nini ikajidhihirisha kwamba ni idara, kwa sababu Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira anaitegemea idara hii kwa kumuendeshea baadhi ya mambo, kwa sababu imepata msaada. Wakati siku msaada ule utakaposita basi itataka wenyewe iwe mamlaka, kwa sababu akenda kupangiwa bajeti na Mhe. Waziri atatiliwa kidogo, yaani shilingi mbili tu.

Kwa hivyo, tungeliifanya mamlaka wakati huu ambapo inajiweza hata ikawa wale wafadhili wakatuona kwamba tumeshajiweza na wakaondoka, basi tayari tumeshakuwa na uwezo wa kuendesha ile mamlaka yetu.

Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa na Idara ya Maji na tuliambiwa mambo ya kiwa mazuri basi iitwe Mamlaka ya Maji. Sasa kwa sababu maji yalikosekana wakawa na wasi wasi hawa watu wa Idara ya Uvuvi itakapoitwa Mamlaka, uvuvi unaweza kukosekana.

Kwa kweli naomba suala hili lifikiriwe zaidi pamoja na kwamba tunaita idara, lakini bado naona ukuaji wetu na mategemeo yetu ni kwamba hii Idara ya Uvuvi ikue kiwango hicho, basi tuliitegemea iwe ni Mamlaka ya Uvuvi Zanzibar.

Vile vile kama Mhe. Assaa Othman Hamad (Waziri Kivuli wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira) alisema kwamba iwe na Chuo cha Uvuvi. Chuo kile kinaweza kuanza na hatua ndogo na baadaye kikakua na wala chuo kile hakina haja ya kuwa na walimu waliokuwepo muda wote pale pamoja na mambo mengine, isipokuwa ni walimu wanaotokana na fani mbali mbali tu.

Mhe. Mwenyekiti, vyuo vya wenzetu hivi sasa nje vinaajiri walimu kidogo sana wale wenyewe, lakini walimu wengi wanaokwenda pale wanakuwa ni *parttime*. Kwa hivyo, inawezekana mwalimu anafanyakazi nyengine au anasomesha sehemu nyengine na kwenda pale kwa wakati wake aliopangiwa, hivi ndivyo vyuo vinavyotufaa sisi kwa sababu ya udogo wetu.

Kwa mfano, tunaweza kuwa na wafanyakazi wazuri katika Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira wanafanyakazi zao za baharini pamoja na nyengine, lakini anajua siku ya Jumanne na Alkhamis ninavyo vipindi katika chuo, basi anajipangia *programs* zake na anakuwa ni *tutor* pale.

Kwa hivyo, ni muhimu madhali wizara nyengine ikiwamo hii Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira imeona kwamba kuna haja ya kufanya Chuo cha Kilimo na wale wa habari wakasema Alhamdulillah na sisi tuwaite wanahabari na wale wa Afya tuwe na Chuo cha Afya, basi kwa nini kusiwe na Chuo cha Uvuvi kumekosekana nini? Hilo jengine Mhe. Mwenyekiti.

Nadhani ingelikuwa ni mamlaka ungekuwa na uwezo wa kupanga mambo yake uzuri zaidi.

Utoaji wa Leseni kifungu cha 3. Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar inakabiliwa na tatizo kubwa ambalo mpaka wenyewe Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji wanakubali tatizo hilo la kwamba kila mtu

anatoa leseni, hajulikani hasa mwenyewe mara huchafukiana. Sasa kwa sababu idara hii imejiwekea utaratibu wa kutoa leseni itabidi wazungumze vizuri na mamlaka nyengine ili isiwe mvuvi anaambiwa wewe umechukuwa leseni Idara ya Uvuvi, sisi ni Halmashauri ya Mji tuna leseni yetu, yule mwengine anasema wewe si unafanya biashara ukishavua, sisi Wizara ya Biashara tunataka leseni yetu. Suala la leseni linataka lipatikane.

Sisi katika kamati yetu Mhe. Mwenyekiti, tumelisisitiza sana, mara ya kwanza ulikuwemo katika kamati yetu, baadae ukatukimbia, lakini Mwenyezi Mungu kakujaalia baada ya kutukimbia umepanda mpaka umekuwa malaika sasa unatutizama. *(Kicheko)*

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hili tunalijua kwamba suala la leseni humu imetajwa, lakini inataka kutizamwa kila mahali, hakuna pahali wavuvi wakishakata leseni wanapokwenda kusumbuliwa tena? Toka mwanzo ijulikane ili pasahihishwe, ikiwa Halmashauri ya Mji au Manispaa, Wizara ya Biashara au *ZRB*, wote wanawaita kwa sababu leseni yenyewe inategemea, ikiwa leseni yenyewe ni meli za kigeni pato lake ni kubwa *ZRB* anakwambia lete huku, shilingi milioni tano hizo utachukua wewe? Lete huku. Kwa hivyo, tukubaliane tokea mwanzo nani anatoa leseni na *authority* yake ni hii na inajulikana kila pahala.

Tatizo hilo hilo la *coordination* Mhe. Mwenyekiti, limeukumba huu mradi wa *MACEMP*. Kwa bahati hii Idara ya Uvuvi ilipata bahati ya kupata msaada kutoka kwa *World Bank* na wengineo. Lakini kulikuwa na mradi wa kujenga soko la kisasa na la matengenezo mazima ya samaki mpaka watakaposafirishwa, kukawa na migogoro ya ardhi na Mhe. Waziri analijua vizuri, kukawa na vitu vinafishwa hapo kati kati. Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu ya mwisho iligundua kwamba muda wa ujenzi wa lile soko ulipita kwa hivyo zile pesa zikarudi kwa wafadhili kutokana na mgogoro kwamba hawakupata kiwanja.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tulipokwenda Mwanza kama kamati niliambiwa mimi kwamba hizo pesa hazikurudishwa Japani kwa sababu wenyewe walikuwa ni Wajapani. Wajapani wakishatoa pesa ndio wameshatoa nikaoneshwa waliona soko lile pale liko Mwanza. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwa sababu nasikia kutokana na taarifa tulizopata kutokana na kamati kwamba kuna utaratibu mpya sasa wa kuanzishwa tena ule mradi wa pahali pengine.

Hapo pahali pengine ikiwa wafadhali wameshapapenda basi tuhakikishe Mhe. Waziri unapapata, bila ya hivyo tutaonekana vipi sisi mbele ya uso wa dunia kwamba fedha za wafadhili zinakuja, mradi wa ujenzi unafika mpaka muda zinamaliza halafu pesa zinarudi na hapakujengwa kitu chochote. Mhe.

Mwenyekiti, soko hilo lilikuwa litusaidie kupata angalau hayo mapanki kwa sababu wangevuliwa samaki wakubwa ile minofu inasafirishwa. Kwa hivyo, tungevuliwa japo yale mapanki.

Mhe. Mwenyekiti, nasikia mimi lugha hii sijui ikiwa baraza halilitaki neno hili la mapanki ni kwamba wale samaki wakishatolewa ule utanda wake huku na huku hubakia mkia na kichwa na ule mfupa wa kati kati wenye miba, yale ndio yanaitwa mapanki. Kwa hivyo, angalau hayo mapanki tungekula tukapata ile protini. Kwa hivyo, katika hali yote hii ya kuimarisha hii sheria na mambo ya uvuvi nayo yanataka yaimarishwe liwepo hilo soko.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kuleta majumuisho yake atueleze kwamba wamefika kiwango gani cha huu mradi ili sheria yetu tunayoitunga ya kuimarisha uvuvi na kuweka hali nzuri ya mazingira ya uvuvi, basi tuweze kuiamini wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi napenda niunge mkono huu mswada na naamini kwamba una watendaji wazuri ukiongozwa na Mkurugenzi wake na timu yake nzima kwa sababu kama ni peke yake hata ingekuwa na uhodari gani asingeweza. Isipokuwa inaonesha kwamba *coordination* yao ni nzuri ndio maana mimi nikasema pale kwamba isingestahiki kuitwa idara ingeitwa mamlaka kwa sababu sisi tunapokwenda katika ziara huwa tunaangalia mambo mengi wengine huwa hawajui tunayoyaangalia.

Mhe. Mwenyekiti, pia huwa tunaangalia hata ule mpango wanaotupangia, unaweza kwenda pahala ukajua hasa kwamba hapa hapana kitu. Kwa hivyo, tunapokwenda ukaipanga ile safari kama ni ya siku moja au siku mbili tunasoma mengi na tunayaona mengi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono hii hoja tunachokiomba ni kwamba sheria zetu ziweze kulingana na sheria zinazokubalika katika Jamhuri ya Muungano ili kusijekuwa na mivutano hasa wakati wa kutiliana mikataba na mataifa mengine au mashirika mengine au makampuni mengine. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hapa ndio penye matatizo ukianza kupoteza *confidence* inakuwa hawaji tena kwako. Mhe. Mwenyekiti, ikiwa sheria zetu zinaogongana na sheria za muungano halafu sisi tukawa tunapoteza *confidence* basi huku itakuwa hawaji tena wataelekea kule ambako wao wana *confidence*. Kwa hivyo, mimi naomba tupigane nazo na ikishindikana tuleteeni humu katika Baraza watakaokuwepo watapigana nazo itaondolewa katika *list* ya muungano. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia juu ya mia.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuunga mkono hoja hii iliopo mbele yetu, pia nikupongeze kwa kukalia kitu hicho cha Baraza kwa kweli umependeza na umestahiki kwa sababu tumechagua sisi wenyewe na leo umeanza kazi kwa hivyo nafikiri huo ndio mwanzo mwema tuna safari ndefu, Mwenyezi Mungu akuzidishie.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwajaalia wenzetu wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira wakiongozwa na Mhe. Waziri, Katibu Mkuu lakini kwa leo pamoja na wenzetu watu wa Idara ya Uvuvi kwa kutuletea mswada huu mbele yetu. Kwa kweli wamefanya kazi kubwa na inayotuhusu katika maisha yetu ya kila siku. Kazi waliyoifanya sio ndogo kwa hivyo na sisi lazima tuwachangie ili kuona inapokwenda kwa wananchi kufanyiwa kazi iwe imekamilika, kasoro zitakazokuwepo ziwe za kibinadamu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa niaba ya wananchi wangu nakubaliana na mswada huu, natanguliza kuunga mkono hoja hii mia juu ya mia, naogopa baadae nikipanda jazba ya mazungumzo nikasahau kuja kuunga mkono.

Mhe. Mwenyekiti, tunazungumzia sheria mpya ya uvuvi, pia tunaweka kando sheria ambayo imetufikisha hapa. Kwa hivyo, mimi mawazo yangu ni kuwa tunaunda sheria mpya sio kama ile ya mwanzo haifai au haikufanya kazi, lakini ina mapungufu tunaunda sheria mpya ambayo itatuwezesha sasa hivi kutuweka katika hali ya kisasa. Mhe. Mwenyekiti, tukianzia na sheria ya zamani ni kwamba imefanya kazi kubwa kwanza taaluma kwa wavuvi wetu au niseme kwa wananchi wetu.

Kwa sababu elimu iliyotolewa katika sheria hii ya mwanzo ni pana sana imeanzia kwenye mambo ya uvuvi, hatari ya kuvua kwa mitego ya haramu na mengineyo. Pia namna ya matumizi ya mitego yenyewe na namna ya ukulima wa mwani elimu hiyo nayo imetolewa kuwa ni namna gani matumizi ya mikandaa na mikoko na mengineyo. Kwa hivyo, mheshimiwa sheria hii ambayo tunasema tuiweke kando imepiga hatua kubwa kwa wananchi wetu na kwa kweli imetusaidia sana.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa tumepanua akili kutaka mambo mapya kwa sababu ya utafiti wa kutosha umefanywa. Tunawashukuru wenzetu wa idara hii pia mafanikio yaliyopatikana yamewaendeleza na kuweka uwezo kwa wavuvi wetu, hivi sasa vijana wengi wanaipenda kazi hii ya uvuvi. Kwa mfano, Mhe. Mwenyekiti, nenda hapo Mjini Mkongwe sasa hivi vijana wadogo wote sasa hivi huwakuti, wote wameshajitia kwenye mitwumbwi wanakwenda kuvua asubuhi na mchana wanaleta samaki, jioni utawaona wamevalia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, zamani kazi za uvuvi na kilimo vijana walikuwa hawataki, lakini sasa hivi imekuwa ni ajira kubwa. Hii ni kwamba baada ya wenzetu kutoa taaluma ya kutosha kwa wananchi walifikiri labda kazi ya uvuvi wenyewe ni watu wazima tu au watu wa shamba, lakini taaluma imekwenda kwa wananchi sasa hivi lile pengo la tatizo kubwa la ajira sekta hii ya uvuvi imelipunguza.

Mhe. Mwenyekiti, hali ya kipato kwa wavuvi wetu nayo ni afadhali, wavuvi hivi sasa wanaweza kwenda kwa chombo cha kutumia tanga pia wana uwezo wa kutumia *machine* kwenda kwa urahisi na kurudi pale ambapo upepo unakuwa shwari wanaweza kufika mapema kufika sokoni na kuuza bidhaa yao ya samaki bila ya kuharibika.

Mhe. Mwenyekiti, katika fani nyengine ya kilimo cha mwani sheria ambayo tunaiweka kando imefanya kazi kwenye eneo hilo. Kwanza kulikuwa na uwelewa mdogo juu ya kilimo hiki, wachache tulizoea mwani wa kwenda kuokota tu pale na baadae kuanika sasa hivi tumejua namna gani wananchi wameelewa kwa kuelimishwa na hivi sasa wanaweza kuupanda na sasa hivi tunasema ni kilimo. Mhe. Mwenyekiti, kilimo hiki cha mwani kimeanzia *stage* mbali mbali tangu ya kuweka vijiti na kufunga mbegu hivi sasa katika jimbo langu vijiti havitumiki tena wanatumia mawe na mipira kwa kuzalisha mwani. Hii faida inakuja kutokana na kuhifadhi mazingira kwa sababu ili upande konde kubwa ya mwani unataka utumie vijiti vingapi, na vijiti ni misitu.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuokoa misitu isipotee wenzetu wameweza kuwapa taaluma wananchi wetu sasa hivi wanatumia mawe ambayo yako mengi baharini pamoja na nchi kavu. Kwa kuchukua mawe ya nchi kavu ukapeleka baharini huwa unaongeza eneo la kuishi samaki kwa sababu samaki hawezi kuishi mahala peupe wanaishi kwenye mawe. Kwa hivyo, mawe haya ambayo wanapeleka wakulima wa mwani yanakuza mwani na wakati huo huo yanakuwa ndio nyumba ya samaki. Hii ni taaluma ambayo wamepewa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sheria ambayo sasa hivi tunaiweka kando tumeweza kupata taaluma nzuri ya uhifadhi wa mazingira yetu ya miti ya mikoko na mikandaa ambayo yametuzunguka. Mhe. Mwenyekiti, watu walikuwa wanajikatia ovyo miti hii, bahari inachukua wakati wake kufanya sehemu zile kuwa kame na baadae kutokea mmong'onyoko wa ardhi. Kwa hivyo, sasa hivi wananchi wetu wameweza kufundishwa namna gani ya kuhifadhi mazingira hayo ya mikoko na namna ya kuvuna ili waweze kupata miti iliyopevuka na baadae kupanda miti mengine ili shughuli za kilimo ziwe endelevu.

Mhe. Spika, tuhakikishe kuwa wenzetu hawa sio wametuletea sheria mpya kama ile nyengine haikufanya kazi, ilifanya kazi na faida zake ni kama hizo ambazo nimeanza kuzieleza. Mhe. Mwenyekiti, kwa nini sasa umeona wakati wa kuleta sheria mpya. Mhe. Mwenyekiti, binadamu siku zote anahitaji zaidi, leo ukipata shati utasema kwa nini sikupata na koti, ukipata na koti utasema kwa nini sikupata kofia.

Kwa hivyo, wenzetu hawa wamefikiria mbali, ili wakaweza kuona kwamba sasa hivi lazima wafanye mageuzi katika sheria yetu na kuweza kutosheleza ni kwamba wananchi wetu kwa mujibu wa wakati ulivyo inabidi waelimishwe vya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi napongeza sana kwani sheria hii mpya itatanua wigo katika kufanya mambo yetu ya utafiti. Kwa hivyo, naamini sheria hii imeipa uwezo Idara yetu ya Uvuvi kufanya utafiti hasa kwa kushirikiana na wataalamu wetu wa ndani na nje, taasisi za kijumuiya na za kimataifa na wengineyo wapenda maendeleo ambao marafiki wa Zanzibar watasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili mimi nitakuwa na moja tu ambalo nitapenda Mhe. Waziri anitoe wasi wasi kuhusu hili neno bahari. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri aliitafsiri ardhi wakati huo alipokuwa Waziri wa Maji kwamba ni sehemu ya mwisho wa maji mpaka yanapofikia maji na mita mia moja.

Kwa hivyo, sasa hivi ninaomba anisaidia yuko Wizara ya Kilimo je, bado maelezo ndio yale yale au wapi atasema mwisho wa bahari na maji namuomba anisaidie akija akifanya majumuisho kwa sababu mambo haya kila mmoja anatafsiri vyake kutokana na mazingira yake.

Tunaona hata wakati wa kupewa wawekezaji mbali ya pale utaona wamepewa uhuru wa mita mia moja kutoka baharini na kwa sasa hivi hii sheria mpya wenzetu wa bahari wamepewa mamlaka ya kuweza kuihifadhi na kuweza kuiendeleza. Mhe. Mwenyekiti, katika hatua hiyo kwenye eneo hili nitaomba anisaidie wapi bahari yetu itakuwa inaanzia kutokana na nchi kavu ili isilete matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 3 kinahusiana na mambo ya leseni. Ni kwamba utaratibu wa kuweka leseni ni mzuri mimi nauopongeza na uendelee. Kwa sababu kwanza tunaweza kusajili na kuweka data zetu kujua vyombo vingapi tulivyonavyo na ni vya aina gani. Pia itatusaidia hata mwenyewe uwe mvuvi chombo chake kitakapopotea akitoa alama ya nambari yake ambayo kwa mujibu wa sheria hii ya leseni lazima iandikwe kwenye chombo basi kinapopotea kinatajwa na kinaweza kuonekana mara moja. Wakati huo huo inakuwa ni kumbukumbu nzuri kwa Idara yetu ya Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, zoezi hili liendelee kuvisajili vyombo vyote vya uvuvi wasione hiki kidau cha nini kukisajili, lakini umuhimu wa kusajili upo. Hata kwenye matatizo ya kumiliki mtu anaweza chombo changu hiki na wakati hakuna *document* ambayo inaweza kumuhakikishia mmiliki wa chombo kile.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, suala la kusajili vyombo natoa wito kwa wananchi wetu waitikie kwenda kusajili vyombo vyao ili viwe salama kwao pia viwe na kumbukumbu katika Idara yetu ya Uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, leseni hizi ni kwa ajili ya vyombo vyetu lakini kuna leseni zinatolewa kwa vyombo ambavyo vinavua bahari kuu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi maoni yangu hivi sasa iko haja ya kuwekewa kanuni au masharti kwa sababu baadhi ya wajumbe nimewasikia wakizungumza hapa. Mhe. Mwenyekiti, ni lazima tuanze kujua kiwango cha bidhaa au mali anayokwenda kuvuna kwa hivyo nafikiri kuwe na utaratibu baada ya shughuli zake za uvuvi huyu tuliyempa leseni amekaa miezi mitatu au sita kule bahari kuu wakati wa kuondoka, basi lazima kuwe na mawasiliano na hapa petu na tulichopata tuweze kukiwekea utaratibu mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, pia alete sehemu ya mzigo huu hasa samaki wakati na sisi tunahitajia kwa matumizi yetu ya ndani na kilichobakia kiwekwe nje. Mhe. Mwenyekiti, haitokuwa na faida kumuachia mtu hapa anavua samaki halafu wote achukue wakati sisi hapa tunakula vyakula ambavyo havina kitoeo itakuwa si vizuri.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema wawekezaji ambao tunaowapa leseni ya kuvua bahari kuu basi walete mzigo hapa nusu tuuziwe sisi ili tupate vitoeo na kilichobakia ndio wakauze huko kwao au kwengineko.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo watoe nafasi ya ajira kama kuna meli ya watu 50 basi japo watu 25 tumwambie chukua wananchi wetu ili wapate ajira na pia watapa ujuzi wa namna inavyovuliwa bahari kuu pindipo serikali itakapokuwa na uwezo. Kwa misingi hiyo mheshimiwa mimi ndio nasema kuwa watu ambao watapewa leseni za uvuvi wa bahari kuu lazima wawekewe masharti maalum ambayo mbali ya kufaidika na fedha ya leseni lakini tutapata faida kubwa ya ajira, kitoeo pamoja na elimu.

Mhe. Mwenyekiti, sheria ambayo iliyopita na hii ya sasa zinatilia mkazo uhifadhi wa bahari, niwapongeze sana Waheshimiwa wote waliotilia mkazo uhifadhi wa mazingira ya bahari. Kwa sababu tegemeo letu kubwa sasa hivi ni bahari, hasa kwa vile nchi yetu ni kisiwa ardhi tuliyonayo ni ndogo, asilimia 90 ya watu wa kisiwa hiki wanategemea kilimo na mifugo na waliobakia wanategemea uvuvi kwa kutumia bahari. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ardhi

yetu hii tunafanyia mambo mengi, ujenzi unakwenda sana mji umeshafika Tunguu, patakuja na viwanda lakini bahari ni sehemu ya ardhi kwa hivyo sisi tutaelemea huko.

Kama hatua hizi ambazo wenzetu wanazozichukua hatukuziheshimu za kuhifadhi bahari yetu kwa kweli tutakuwa pahala pabaya. Kwa hivyo, mheshimiwa mimi naipongeza sana wizara kufikiria jambo hili la kutilia mkazo uhifadhi wa bahari. Mhe. Mwenyekiti, tunaona faida wa zile sehemu ndogo tu tulizofanyia utafiti, Ghuba ya Chwaka na Mnemba wavuvi wametononoka, bahari nayo sasa hivi imeweza kukua imekuwa na samaki wa kutosha, wavuvi wanakwenda wanarudi angalau wanapata kuuza chochote.

Mhe. Mwenyekiti, upande wa kwetu ambako natoke mimi tuna Hifadhi ya Minai hii imetusaidia sana na kamati wajumbe wake ambao wamejieleza katika semina tuliyofanyiwa na Wizara ya Kilimo kwa kweli wanajitahidi na inafaa nimuombe Mhe. Waziri awaendeleze zaidi ili waweze kupata taaluma kwa sababu kwanza elimu yao kubwa lakini wana kazi kubwa, kazi ya kuongoza wenzao ambao bado hawajaelimika ni kazi kubwa kweli kweli.

Mbali ya taaluma tuliyowapa ya semina, lakini hata kama kuna mafunzo maalum ya miezi sita au tisa basi Makatibu Watendaji wa Kamati zetu za Uvuvi za Kanda waongezewe taaluma, ili wakafanye kazi hiyo na kwa kweli watawasaidia wenzetu wa Idara ya Uvuvi na Idara ya Uhifadhi.

Mhe. Mwenyekiti, katika Wilaya ya Mjini hapa tunalo eneo la Chumbe, ni sehemu ndogo lakini hii sehemu iliyohifadhiwa ni kwa mazalio ya samaki na tunaona. Wenzetu wa Wilaya ya Mjini wamefaidika sana, si aghlabu wavuvi wa mjini kwenda wakarudi watupu, kwa lugha ya kipwani kule kwetu tunasema kurudi kau. Kwa sababu eneo lile samaki wakishazaliwa wanakua na wanasambaa kwa hivyo, wao wanawapata, sasa muda wote wanao kwa sababu pale pahala pa mazalio hapajaharibiwa.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, utafiti wa aina hii napendekeza na maeneo mengine yote yaliyopo basi japo sehemu ndogo kuweko na sheria japo ngumu zitazowabana wananchi lakini faida ionekane kwa wote, kuwa samaki wale wanapatikana na kuacha wavuvi wetu ambao wanakwenda katika hali ngumu ya baridi, upepo, mahala hakuna hata pa kushika wanarudi kau kama siku moja au mbili hawajapata kitu. Nafikiri tukihifadhi maeneo yale ya mazalio ya samaki yataondoa tatizo hilo kwa wavuvi wetu na kusononeka.

Mhe. Mwenyekiti, juhudi za kutokana na uvuvi ule tuliouzowea wa kihori na mshipi nao tumepiga hatua. Mhe. Mwenyekiti, naishukuru sana wizara hii, hasa kupitia Mkurugenzi wake wa Idara ya Uvuvi kwa kuandaa programu mbali mbali na kutafuta misaada ambayo wananchi wetu wanafaidika nayo.

Programu au mradi wa *MACEMP* imekuwa ni muokozi kwa Wazanzibari. Waliokuwa hawamiliki vyombo sasa hivi haijambo wanamiliki japo si cha peke yake, katika watu 20 mnapewa chombo kimoja ambapo mkiambiwa mnunue nyinyi wenyewe hata miaka kumi mchange hamkipati, huu si msaada mdogo, kupewa nyavu za kamili, mashine, pesa za tanga, wakati mwengine hata kama hutokea hasara kuharibika nyavu zenu pia mnaweza kupewa tena nyengine ili kuhakikisha mwananchi unapata kufanya kazi kila siku. Hili si jambo dogo.

Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mkurugenzi wa Idara hii anavyolisimamia vyema jambo hili. Kwa kweli wakulima wetu wa mwani, wavuvi wetu wanamsifu, na sisi kama ndio tunaowawakilisha ni vyema kutumia jukwaa hili kumsifu Mkurugenzi huyu wa Idara ya Uvuvi jinsi anavyotekeleza majukumu yake kwa wavuvi wetu. Kwanza hana hiyana, mwenye huruma, mfuatiliaji.

Lakini la pili hili litaungana na kifungu cha 35 ambacho alikigusia Mhe. Ali Abdalla. Hata namna ya wale wenye kufanya makosa anavyoshughulikia. Mhe. Mjumbe hapa alishauri kwa nini wanaofanya makosa hawapelekwi kituoni wakapelekwa huko? Lah, idara yetu hii ni ya wananchi inashughulika na wananchi, laitani ingekuwa tunaweka askari kama wanavyowekwa askari wa *traffic* kuangalia magari, wavuvi wetu wote leo wangekuwa wako jela. Lakini idara hii imeweka utaratibu wa kuyashughulikia yale makosa madogo madogo na kusuluhishwa, kwa wavuvi wenyewe lakini baina ya wavuvi pamoja na wawekezaji. Idara hii imejitahidi kusuluhisha.

Mhe. Mwenyekiti, hili nalo mimi nasema zuri na liendelee, mambo ya kupelekana polisi labda kwa wale wakorofi, lakini pale panapotokezea makosa madogo madogo idara inaweza kuya-*handle*, Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri tuendelee kushirikiana nao hawa, kwa sababu ndio tunawafunza. Pale pakiwa na mkorofi kweli lazima atapelekwa huko, lakini kama bado hajawa na ukorofi bahati mbaya tu imetokezea, utaratibu wanaotumia sasa hivi wa kusuluhisha au wao kesi zile kuzihukumu kwa kutoa adhabu ndogo ndogo mimi nasema uendelee.

Eneo la mwisho Mhe. Mwenyekiti, nasema sheria hii itoe uwezo wa mashirikiano, tuoneshe namna gani tutaweza kushirikiana na majirani zetu wa Tanzania Bara na Kenya. Kwa sababu bahari hii tunatumia sote, samaki ni viumbe wanakwenda huku na huku, haiwezikuwa sisi tunahifadhi wao wanaharibu, lazima tuwe tunashirikiana tuwe na msimamo mmoja, sheria

zinazofanana na hata katika kuwatafuta wale wahalifu tuwe tunashirikiana ili sote tuweze kufanikiwa. Kusema kweli Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa katika mazingira haya sisi na wenzetu wa Tanzania Bara naona bado yako finyu sana mashirikiano haya. Wenzetu kule katika kuhifadhi mazingira ya mabomu na sumu wamekuwa *serious* mpaka wanatumia wanajeshi, wana faiba zinakwenda kama upepo. Sasa uharibifu wa mazingira yale wa mabomu wamekimbilia visiwa vyetu vya hapa, sisi hatuna hivyo, najua na jeshi ndio Jeshi la Tanzania na linatulinda kwa nini haliwezi kufika au tukatumia uwezo na wao wakaweza kufanya doria na huku.

Hata hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu wanasimamia vikali ndio maana wanakuja huku basi na sisi tuwe *serious*, tutumie vyombo vyetu hivi tuwape uwezo tuhakikisha kwamba kule wanabanwa na huku wabanwe.

Wananchi wetu wa Zanzibar wameshaelimika juu ya kuhifadhi mazingira ya bahari. Lakini ndugu zetu huko wanakuja kikamilifu, wanakuja na boti na *hours power* arubaini arubaini mbili wameziweka, wanakuwa na silaha, ndio. Sasa kwa hao wetu tunaowapa vihori vidogo wanarudi nyuma hasa katika visiwa vya Pungume na Kwale. Kwa hivyo, suala hili katika kuwapa uwezo watu kwa kuhifadhi mazingira basi sheria na vitendea kazi vikiriwe.

Lakini pia katika hiyo bahari kuu tutazungumza kama nilivyozungumza wakishachukua mali ile watuletee huku, basi wanaweza kupeleka chombo chengine huko wakasema tumepata tani mia moja hali ya kuwa wamepata tani elfu moja wakasafirishia kwa chombo chengine nje. Kwa hivyo, lazima na sisi tuwe na vyombo vikubwa ambavyo askari wetu wanaweza kufika kule waliko, hizi boti za KMKM kusema kweli hazina uwezo wa kufika huko, huko kufika kwa tabu kwa bahari iliyoko huko, sasa kufika kwa tabu je itaweza kumfukuza mhalifu ambaye yeye kajiandaa vizuri? Hivyo, na hili Mhe. Waziri ili na sisi tuweze kuitumia bahari kuu lazima tuweze kuidhibiti, tuwe na vyombo vilivyokuwa imara kabisa.

Najua askari wetu tunao madhubuti, lakini hawana vyombo vyenye uwezo wa kuweza kukumbana na maharamia. Lakini pia ule mtandao wa kimataifa nao basi tuupongeze ambao unasaidia. Kama hivi karibuni tumesikia meli moja ambayo inapeperusha bendera ya Tanzania ikaweza kukamatwa na wenzetu, tupongeze juhudi zinazochukuliwa na serikali yetu na serikali jirani juu ya kupambana na maharamia.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri mchango wangu, imani yangu ni kuunga mkono huu mswada. Kwa sababu huu unatuhusu sana kwa wavuvi wetu, wakulima wa mwani, sasa zaidi nitatilia mkazo suala la utafiti kwenye sheria hii mpya hasa kwenye masoko ya mwani.

Masoko ya mwani yamekuwa tatizo hasa kutokana na bei, kazi ya ukulima wa mwani ni ngumu lakini tija yake ni ndogo na inapoteza nguvu za wananchi wetu. Kwa hivyo, eneo hili lifanyiwe utafiti wa kutosha, mwani gani ambao utakuwa na bei kubwa, nchi gani itakuwa na soko zuri ili mwani wetu tupeleke huko. Lakini pia tusikubali tu wale wafanyabiashara na bei zao, lakini na sisi kwa sababu kuna mtandao wa *internet* basi kila siku Idara yetu ya Uvuvi pamoja na Wizara ya Biashara ihakikishe bei za nje tulinganishe na zile wanazouzia wananchi wetu hapa zinafanana ili wasiumizwe? Na kama hapana budi basi tufanyiwe utaratibu tuwe tunaununua mwani huu kama zamani.

Kwa sababu zamani palipokuwa hapana masoko serikali katika kutumia chombo chetu cha *ZSTC* na siku hizi biashara yake ndogo, kwa nini haiingii ikanunua huko pwani? Karafuu sasa hivi hakuna, mwani nao ni zao na kile ni chombo cha biashara, Mhe. Waziri kwa nini wasinunue. Basi mimi ningeiomba *ZSTC* kwa sababu zao la karafuu siku hizi limepungua basi biashara nyengine ya kilimo ni mwani. Hilo liwe soko la uhakika wananchi wetu wasipunjwe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nikushukuru sana kwa kunivumilia, lakini pia nimpongeze sana Mhe. Waziri, niendelee kumshukuru na kumpongeza Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi na wenzake kwa kazi zao za kila siku nzuri sana wananchi wanazithamini.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwenye hoja hii ya mswada mpya naunga mkono kwa asilimia mia moja. ahsante sana.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nichangie mambo machache sana katika mswada huu. Lakini kabla ya kuchangia nakushukuru na wewe, leo kwa kupata nafasi kwa mara ya mwanzo kukalia kiti hicho kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii imekuja katika wakati ambao tuna matatizo ya kiuchumi na rasilimali yetu kubwa ni bahari na mchango mkubwa katika uchumi wetu tunategemea kilimo. Lakini bahati mbaya tukiziangalia takwimu hizo za uchangia wa uvuvi katika pato la taifa bado ni dogo mno. Juzi tulipokuwa na semina tuliuliza suala hilo na tukajibiwa hapa, ni asilimia ndogo sana.

Sisi Zanzibar kwa sababu ni kisiwa tumezungukwa na bahari, tulikuwa tunafikiria kwamba tegemeo letu kubwa katika mchango wa pato la taifa kutokana na kilimo basi lingetoka baharini zaidi kutokana na upana wa rasilimali hii ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia, kuliko hata ile rasilimali ya ardhi ambao kwa kweli ni ndogo kwa Zanzibar. Lakini mambo yamekwenda kinyume nyume.

Mhe. Mwenyekiti, inaonekana kwamba bado kunahitaji nguvu kubwa sana katika kuendeleza harakati hizi za uvuvi ili ziweze kusaidia uchumi wetu na ziweze kuleta tija kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nchi kama Comoro ni nchi ndogo sana kuliko Zanzibar, lakini huwa tunasikia wafanyabiashara wanakwenda Comoro kwenda kuchukua kamba ambao wametengenezwa Comoro. Sasa sisi hujiuliza, hawa Comoro nchi kama yetu na sisi kwa kweli ni nchi kubwa zaidi kuliko Comoro, lakini naweza ku-*manage* kuna viwanda vya kutengenezea samaki. Ni utaratibu upi ambao umefanyika pale? Ni wananchi wenyewe au ni uwekezaji ambao umekuwa *promoted* pale na nchi ile inanufaika kwa viwanda.

Nimetoa mfano huo tu kwa sababu ndio ambao uko karibu sana na mazungumzo yangu, lakini naamini pengine ziko nchi nyengine ndogo zaidi labda pengine kama Maldives ambazo ni nchi za visiwa pengine zina maendeleo makubwa zaidi, lakini kwa leo sina ushahidi huo mkubwa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba inaonesha na hili hatuwezi kulifanya kwamba ni jukumu la Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira peke yake au ni jukumu la Idara ya Uvuvi, lakini inaonesha ndani ya mipango yetu ya kiuchumi katika nchi hatujaipa umuhimu harakati hizi za uvuvi. Kwa sababu ni mambo tuliyoyarithi kwa wazee wetu basi tumeyaachia yaende kama yaendavyo tu, watu wajitafutie riski basi waweze ku-*survive*. Lakini matumizi yakiwa madogo ya rasilimali ambayo ndio Mwenyezi Mungu aliyokujaalieni katika nchi, hiyo huwa ni dalili kubwa sana ya utumiaji mdogo wa rasilimali na kurejea nyuma kimaendeleo.

Nitoe mfano wa uwekezaji ambao tunauona katika Shirika la Meli katika vyombo vya baharini ambavyo ni vya usafirishaji. Zamani tulikuwa tunategemea meli zetu hizi za serikali tu, lakini baadae vikaja vyombo hivi vidogo vidogo ambavyo vinakwenda. Vyombo hivi vingi vinamilikiwa na hawa matajiri au wafanyabiashara wa hapa hapa ndani. Sasa suala tujiulize, kwa nini wachague kwenda katika vyombo hivi vya usafirishaji wa abiria na wasichague asitokezee hata mmoja akasema hapana, mimi badala ya kununua meli ya abiria nanunua meli ya uvuvi japo ya *size* ndogo tu. Tunajiuliza maswali kama hayo tunasema ni nini kinachotokea katika kufikia maamuzi haya kwa wafanyabiashara wetu?

Sasa inawezekana sababu zikawa ziko nyingi, lakini tunaona moja katika sababu ambayo iko wazi kabisa ni namna ambavyo hatujalenga kama serikali kuwahamasisha wale wenye fedha kidogo ambao wanaweza wakawekeza wakaweza kuingia katika nyanja hii ya uzalishaji.

Nakumbuka maamuzi ya hawa wafanyabiashara kuleta vyombo vile yalikuja baada ya kufanywa utafiti mkubwa na *DANIDA*. Na *DANIDA* ikaonesha ile *potential* ambayo itakuwepo, tena ilichukua muda kidogo vyombo vile kuingia. Kwa sababu *research* ile ilifanywa mwaka 1990 na vyombo hapa nadhani viliingia miaka miwili au mitatu baadae. Lakini wafanyabiashara walikuwa wanaitumia ile *document* ya kuona namna ambavyo *potential* ya usafirishaji iliyopo na *prospect* ambazo baadae zinaweza zikaja.

Sasa humu katika kazi za idara hii imetajwa kwenye kifungu cha 5(1)(f), kufanya tafiti za kisayansi au shughuli nyengine zo zozote kwa ajili ya usimamizi bora wa shughuli za uvuvi. Mimi nilikuwa napendekeza, ungefanywa utafiti kama uliofanywa kwa Shirika la Meli, tuombe hawa wahisani wetu watusaidie tuwe na *document* ambayo inaonesha hasa *potential* ya mazao haya ya baharini na ni namna gani tunaweza tukawafanya wawekezaji wetu wa ndani kwanza waweze kuwekeza katika *area* hii ya *fishing*.

Nilifikiria kwamba hili ni jambo lililo muhimu sana sana, kwa sababu ya ukosefu mkubwa ambao upo sio tu kwenye idara hii, lakini kwenye idara nyingi, hasa wa *data's* ambazo zitakuwa zipatikane kutoka kwenye *activity* za uchumi za *grass root* kama hizi ni tatizo sana.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tulionesha hapa wataalam wa kienyeji ambao wanatumiwa katika ku-*control* huu uvuvi ambao tunauita ni uvuvi haramu. Nilikuwa nikitafuta sana kuona hawa wataalamu ambao Makatibu wale waliyooneshwa hapa, ndani ya sheria hii wametambuliwa vipi. Nikaangalia kwenye *definition*, nikaangalia vifungu vyote sijaona.

Kwa hivyo, inaonekana tu, kwamba haja ya kuwa na structure kule chini yak u-control na mimi nasema sio yaku-*control activities* hizi za uvuvi tu, kwa sababu sisi tumelenga zaidi katika ku-*control* uvuvi haramu. Lakini haja ipo ya kuwa na *structure* ambayo inaweza ikasaidiana na idara hii katika kuendeleza uvuvi. *Structure* hiyo lazima iwe *formal structure*, isiwe ni *structure* kama ile ambayo inasaidia shughuli hizi lakini haitambuliwi na sheria.

Mimi nilikuwa nikifikiria kwamba, juzi tulikuwa na semina hapa kuhusu uendelezaji, uharakishaji wa *local government*. Mhe. Mwenyekiti, hili lazima tulipigie kelele sana ndani ya Baraza letu kwamba *local government* hizi lazima *structure* au *reform* yake ijulikane ili tuone *activities* hizi za wananchi hasa zinazokuwa *elected* na *activities* zao za uchumi ambao ni uchumi wa jadi, uvuvi na kilimo utakuwa *coordinated* vipi na ile *structure* ya *local gornment*, ili kuipunguzia kazi idara au kuipa idara njia nzuri zaidi ya kuwafikia wananchi kule chini.

Lakini vile vile *local government* itatusaidia katika kuweka *data* ambazo ni muhimu kupatikana katika idara. Naamini mimi idara utafutaji na uwekaji wake wa *data* hizi za uvuvi zinaweza kuwa ni za matatizo kama ilivyo katika idara nyengine. Na siku nyengine hiyo 1% inayokuwa inatajwa ndio inayochangiwa na uvuvi katika kilimo ikaja ikawa ni ile *estimate* tu ya kawaida lakini sio hasa ile ambayo ni ya uhakika inayotokezea.

Nimesema hilo nilizungumze Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu bado tutakitegemea kilimo hasa sehemu ya uvuvi. Na kwa sisi Zanzibar mimi nafikiri kauli mbiu yetu ingekuwa ni uvuvi kwanza kuliko hata ile kilimo kwanza. Kwa sababu kilimo sisi tulivyozowea ni kilimo kwa maana ya *cultivation* hii ya kawaida, ambayo hiyo *effort* ni nyingi sana za wananchi na zinaonekana wazi wazi.

Mhe. Mwenyekiti, hata kama tungekuwa na *mechanization* ya kilimo, lakini bado *recourses* ya ardhi ingefika pahala sisi inatu-*limit* sana tu, tungefika pahala tukasema tunatumia *technology* kubwa katika ardhi lakini mwisho tungekwenda tukaona *recourse* yetu ya ardhi kwa kweli haiwezi kutufikisha pahala. Lakini kwenye bahari haiku ivyo, kwenye bahari bado ni *unlimited to some extent.* Kwa hivyo, nadhani kilichokuwa kinatakiwa sasa ni kuelekeza *effort* yetu huko.

Mhe. Mwenyekiti, niliona humu limezungumzwa suala la ufugaji wa samaki. Hii ni aina ya kilimo cha samaki ambacho kwetu hakijazoeleka. Zamani lilipokuwa likizungumzwa suala hili lilikuwa linashabihishwa sana na uharibifu wa mazingira. Kwa sababu utakwenda ukate mikoko na mambo kama hayo.

Utakapofika katika suala kama hili lazima tufanye *tradeoff* kati ya kile tunachokipoteza katika uharibifu wa mazingira na ile tija ambayo tunaweza tukaipata kwa wafugaji wa samaki. Na tusije tukasema tu, ufugaji samaki unaharibu mikoko kwa hivyo, unaharibu mazingira moja kwa moja. yawezekana mazingira ambayo yanaharibika kwa ufugaji samaki yakawa hayana hasara kubwa kuliko ile faida ambayo wangeliipata wananchi katika ufugaji wa samaki.

Napenda Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza sana Mhe. Waziri Kiongozi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pamoja na Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira ambao mwezi huu huu tulionao walitembelea katika shamba la ufugaji wa samaki ambalo liko Kikokwe Chambani.

Mhe. Mwenyekiti, pale wananchi wameamua na sijui kama kuna sehemu nyengine labda kwa Zanzibar ambako zinafanywa shughuli hizi, sina uhakika, lakini si mwahala mwingi ambamo kuna *activities* kama hizo. Vijana wengi

kwa kweli waliamua kwenda kule, tatizo linaloonekana katika shughuli hizi za ufugaji wa samaki ambazo humu zimetajwa na pengine zitakuwa ni eneo ambalo litaendelezwa, inaonekana kwamba linahitaji utaalamu mkubwa mno. Pengine ni utaalamu mkubwa mno kuliko hata kwenye kilimo na pengine kuliko hata kwenye ufugaji wa wanyama. Kwa sababu kulea samaki najua kunahitaji taaluma na elimu kubwa zaidi kuliko huko.

Kwa sababu zile shughuli nyengine tumezirithi kwa mababu, inawezekana ukamuona ng'ombe ukajua hali yake ukamtizama tu hivi ukajua kwamb ahuyu ng'ombe wangu hayuko katika hali ya kawaida, na ukaenda kwa madaktari wa kienyeji wakaja wakakutibia, baada ya kumuona. Lakini kwa samaki nadhani hilo ni tatizo kubwa sana. Lakini hata ile hali ya bahari kuisoma mpaka ukaijua tabia zake kwa kweli ni tatizo na tatizo linakuwa kubwa zaidi leo wakati dunia imekubwa na *global women*, ambapo kwa kweli tabia za kila kitu katika nchi zimebadilika.

Zamani wazee walikuwa wakiisoma miongo tu, wanajua kwamba katika mwaka huu kitakachotokezea pengine kuna vitu kama *high tide*, kuna kitu kinaitwa pindua wimbi. Sasa pindua wimbi ni ile *high tide* ambayo inatokezea zamani ilikuwa inakuwa *determined* hasa, wanajua hasa wazee kwamba katika mwaka huu tunayo pindua wimbi. Lakini leo inakuwa ni shida kutokana na kugeuka kwa mazingira ya dunia.

Mhe. Mwenyekiti, *effort* za watu katika ufugaji wa samaki zinaweza zikaharibika sana kutokana na kwamba hatuwezi ku-*focus* mambo haya kwa sababu ni mambo ya utaalamu lakini juhudi za watu bado zinaongezeka katika shughuli hizo.

Niseme tu kwamba kilichotokea katika sehemu ile ya ufugaji wa samaki Chambani ilikuwa ni hilo pindwa wimbwi ambalo lilitokezea na lilipokuja samaki wote ambao walikuwa wanafugwa ni tegemeo sasa karibu kuvuna wote wakaondoka kwa siku moja na hii ni mara ya pili. Mara moja ni wakati ule ambapo kulitokea maji yalipanda sana Unguja na Pemba, hata hapa misukosuko ilikuwa mikubwa tu, nayo ilihatarisha hali ile.

Sasa wananchi wanachofanya pale ni yale mazoea tu tuko karibu na bahari kwa hivyo tunakwenda kufuga samaki. Lakini hawajui bahari itakapokuwa imechafuka *effort* ile ambayo wameiweka pale inaweza ikaondoka kwa wakati gani. Kwa hivyo, nilichokuwa nataka kusema hapa kwa sababu nimeona katika kazi za idara hii itakuwa ni kukuza, kuendeleza, kudhibiti, kufuatilia shughuli zote za uvuvi. Mimi nilikuwa naomba sana shughuli ya ufugaji wa samaki idara hii itusaidie sana kuwaendeleza vijana ambao tayari wamekubali wenyewe kwenda katika shughuli hizi.

Mhe. Mwenyekiti, mradi ule pale unakaribia sasa hivi kilichokwishaingia pale ni karibu milioni 100. Lakini hakifahamiki nini kimepatikana na wengine wanakuwa *discourage* wanaondoka njiani wakati kuna milioni moja zimekwisha kuwa *invested*. Ilipokuwa ikisomwa taarifa wakati wa ziara ya Waziri Kiongozi, kila baada ya mistari miwili Waziri Kiongozi alikuwa ana-*intervene* anasema mbona sijakufahamu, yule msomaji hajafahamika.

Wakati huo risala za sehemu nne zote zilikuwa ziko *clear* lakini hapa kwenye uvuvi kulikuwa kuna matatizo makubwa na hata akageuka Mhe. Waziri Kiongozi akatuuliza sisi. Nyinyi wenzangu mmekwishafahamu, mmesharidhika na hili linaloendelea. Tukamwambia bado yako maswali mengi kujibika. Inaonekana namna gani ambavyo wale watu wamelipenda tu lile jambo lakini utaalam wao mdogo katika kulishughulikia.

Kwa hivyo, mimi nimalizie katika hili kwa kuomba sana idara hii isaidie. Hizi pesa ambazo zimeingia pale na sehemu nyengine za aina ile, pamoja na *effort* kubwa ya watu *in terms of time* ambayo wanaipeleka pale, basi iendelezwe vizuri ili kuwasaidia wasiwe *discourage* kumbe ni kitu ambacho kinaweza kikaleta manufaa.

Mhe. Mwenyekiti, kulitajwa suala la madago hapa. Madago ni sehemu muhimu sana kwa sababu watu huhajiri majumba yao wakaenda wakalala pengine wiki moja au mwezi mzima wanatafuta rizki.

Mhe. Mwenyekiti, madago haya lakini nayazungumza pamoja na madiko ambayo ni vile vituo. Madago na madiko Mhe. Mwenyekiti, yaendelezwe. Yakitokea maradhi ya mripuko sehemu za mwanzo ambazo zinaathirika ni humu kwenye madago kwa sababu ni sehemu ambazo hazikupangika vizuri, hamna vitu vya kuwasaidia hasa wale wanaokwenda kuhamia pale. Yakiwekwa vizuri haya Mhe. Mwenyekiti, yanaweza yaka-*encourage* watu wakakaa muda mkubwa zaidi na uzalishaji pengine unaweza ukawa mkubwa zaidi. Kwa sababu ni mazingira ambayo lazima yawe mazuri ya kuwaweka watu waweze kuzalisha.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona humu masuala haya ya makosa yakitokezea na namna ambavyo adhabu zinatolewa. Mimi napenda tu niseme kwamba makosa haya yakitokezea lazima uadilifu uwe mkubwa katika kushughulikia. Sasa hivi kuna matatizo ambayo yanawapata wachuuzi hawa wenye masusu ya samaki. Anaweza akakamatwa huko na hawa Halmashauri ya Wilaya, ile faini atakayopigwa pale basi ni mtaji wake wa mwaka mzima. Yanatokezea hayo na malalamiko tunayapata.

Hatusemi kwamba zisitozwe faini kwa wale ambao wanaleta matatizo wanakosea, lakini lazima faini zile ziende katika utaratibu ulio mzuri kabisa na ambao hautomfanya yule ambaye anashughulika na ile shughuli yake kukataa tena kuichukia ile shughuli ikawa ni njia ya kummaliza tena katika ile biashara.

Kwa hivyo, sambamba na hili nadhani kwa wale ambao watakuwa wamekosea katika utumiaji huu wa vifaa na tuseme kwamba bado tutaendelea kuwapata watu wa aina hiyo, hasa kwa sababu hatujageuza *alternative way.* Hawa wakianza kupata njia mbadala ambayo ni ya utaalam wa kisasa utakaowasaidia katika kuzalisha mimi naona wataondoka mara moja katika utumiaji huu wa uvuvi haramu. Lakini tuseme kwamba bado tutaendelea kupata matatizo ya aina hii. Lakini utoaji wa adhabu basi uwe ni utoaji ambao hautomfanya mtu kuchukia kabisa.

La mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, juzi niliuliza swali na leo naliuliza tena kwa sababu halikujibiwa kutokana na muda. Wale tuliambiwa ni *semi-industrial* ambao wametajwa sana humu. Tunawaona zaidi pale Dar es Salaam tukipita, hapa Unguja hatuoni, boti zinazoegeshwa hapa ni za abiria tu. Ni kusema *semi-industrial* huku hakuna? Au wanakwenda kuegesha kule kwamba kuna sababu zipi. Au hatujatoa leseni hapa za *semi-industrial.* Kama hakuna hapa bado ni hawa hawa wa kienyeji tatizo liko wapi katika utoaji wa leseni, tatizo liko wapi katika kuwavutia hawa wakafika.

Tunaona kwamba pengine kufika kwao hao kwa sababu sisi wenyewe hatujakuwa na uwezo wa ku-*exploit* ile *resources* katika ile *area* ambayo wangetumia hawa *semi-industrial* lakini ikawa na leo tunawakosa, basi ni kwamba sisi hatuna uwezo wala ile *promotion effort* yetu pia ni ndogo ya kuwapata wale wenzetu kuja wakaweza kuzalisha tukapata angalau faida hiyo leseni.

Mimi naweza kusema kwamba hili litakuwa vile vile ni tatizo. Kwa hivyo, ni vizuri hapa paangaliwe na tuelezwe hasa tatizo liko vipi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi nisifu sana idara hii kwa kuwa karibu na wananchi. Kwa sababu kadri ambavyo wananchi wanapata matatizo katika activities zao haichukui muda idara inafika.

Matatizo haya yaliyotokezea pale Chambani idara imefika mara moja na kuja kuangalia nini kilichoharibika. Lakini tumeona misaada mbali mbali ambayo wamekuwa wakipewa. Fedha zile ambazo zote wame-invest pale ni juhudi ya idara hii ambayo ndio imekwenda pamoja na *MACEMP* na *TASAF*. *TASAF* inaanza kusahaulika sasa hivi lakini *MACEMP* bado inakwenda mbele kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue muda huu mdogo ambao umebakia kwa kuwapongeza sana kwa shughuli zao namna ambavyo wanazisimamia vizuri na wanakuwa karibu sana na wananchi. Ni imani yangu kwamba watazidisha juhudi ili kuona kwamba wananchi wetu wanakwamuka na umaskini.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chambani na hasa kwa niaba ya wavuvi walioko Jambangome, Matele, Mapape, Kikokwe, walioko Mtangani pengine atasema mwenyewe Mwakilishi hapa, naunga mkono mswada huu mia kwa mia, ahsante.

Mhe. Ali Moh'd Bakari: Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala* kwa kutuwezesha kufika sasa hivi tukiwa tuko hai, lakini pia tukawa ni wazima na tukaweza kujumuika hapa kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nikupongeze wewe mwenyewe binafsi kwa sisi kukuchagua wewe kuwa Mwenyekiti na hatimaye leo unaongoza Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba nichukue nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa mashirikiano waliyonayo ya karibu sana na kuweza kutuletea mswada huu ambao una lengo zuri tu la kuweka utaratibu bora kwa suala zima la uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, umekuja mswada huu ambao hatimaye itakuwa sheria ya kuweka utaratibu bora, lakini sijui niseme kama tumechelewa au kitu gani. Hata kama umechelewa lakini jambo bora basi pale lilipoanza ndio linaendelezwa. Kwa hivyo, tunajifunza kutokana na matukio mbali mbali, kwa mfano kuona kwa wenzetu kutokana na kutembea tukaweza kujifunza yale mazuri ambayo wao wanayaendeleza na yanawaletea tija kwa watu wao.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kutokana na mswada huu na yaliyoelezwa ndani ya mswada huu na sheria hizi, kidogo zinaweza zikawa ngumu katika utekelezaji wake hasa ukizingatia mazingira ya watu wetu ambayo tayari huku nyuma wameshayazoea na sasa hivi wanayafanya. Hapa lazima huruma ichukue nafasi kubwa zaidi kuliko hata hii sheria yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi utakumbuka kwamba wavuvi wetu wote katika visiwa hivi wanavua huu uvuvi ambao wameuzoea zaidi ambao sasa hivi unaitwa uvuvi haramu. Sasa basi, katika hali hii bado hatujaweza kuwafikia wavuvi wetu wote tukawabadilishia uvuvi ule tunaouhitaji sisi ambao hatimaye wataepukana moja kwa moja na uvuvi huu ambao wao wameuzoea ambao sasa

hivi ni haramu. Lakini tukianza kutunga sheria hizi ambazo zitawahukumu wao kutokana na uvuvi ule wanaovua, suala la msingi hapa la kujiuliza hatimaye wao wafanye kazi gani. Mhe. Mwenyekiti, mimi sitetei kwamba waharibu mazingira watu hata kidogo. Lakini ninachokitetea hapa ni kwamba bado hatujamudu kuwapangia utaratibu ulio bora.

Mhe. Mwenyekiti, hizi nyavu za macho madogo au za kukokota ambazo zinapigwa vita sasa hivi ule ni aina ya uvuvi tu, si kwamba kila nyavu ndogo basi inaweza kuharibu mazingira. Kwa sababu ile nyavu wanatia mawe mengi sana halafu wao wakazivuta, lakini zile zile zinaweza kuvuliwa kwa utaratibu mwengine na zikawa haziharibu mazingira, itakuwa wao wanakwenda kutafuta samaki wakishawaona wanawatega.

Sasa tatizo linakuja kwamba hizi aina za uvuvi ndio ambao unatuathiri. Lakini ni kwa sababu watu hawajapewa taaluma zaidi ya uvuvi, kwa hiyo wanavua walivyozoea wao na wanavyojua na walivyorithi kutokana na wazee ambao huko nyuma walikuwa wanavua.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni nilipita hapo kwa Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini Mussa Aboud Jumbe kuna maboti mengi sana pamoja na nyavu zake na mashine ambazo wamepewa watu wengi kwa ajili ya kukusudia kupiga vita uvuvi haramu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu katika jambo hili ni kwamba pamoja na jitihada kubwa sana ya serikali kupitia Wizara hii ya Kilimo, Mifugo na Mazingira, nadhani pangefanywa kwanza utaratibu wa kuwajua hawa wavuvi wanaovua uvuvi huu katika nchi hii ni wangapi na wako wapi na wapi, ili zile boti moja kwa moja zikawafikia wao. Kwa sababu inaonekana kwamba hizi boti zinavyotolewa zinatoka kwa vikundi zaidi kuliko wale ambao wao ni wavuvi wa kawaida na wanaharibu haya mazingira.

Sasa jambo hili tunaweza kufanya jitihada kubwa ya kuona kwamba tunapeleka haya maboti, lakini kumbe tunaowapa maboti sio wale wavuvi ambao wanaharibu haya mazingira, ni wavuvi ambao wamejikusanya vikundi kwa sababu ya shida mbali mbali na wako katika ukanda wa uvuvi wakaja wakaomba na wakapewa. Kwa kuwa hakufanyiki uchunguzi wowote wa kujua kwamba wao ndio wana nyavu za kuharibu mazingira, lakini utaratibu ni kuwasaidia watu kutokana na umaskini wakawa wanapewa hizi nyavu.

Kwa hiyo, bado mimi nadhani tuandae utaratibu wa kuwajua wale watu wa uvuvi huu ambao hatimaye unaharibu mazingira na kusababisha athari kubwa kwa viumbe vidogo vidogo vya baharini. Hii itatusaidia zaidi kujua kwamba wako wapi na wapi tuwape kipaumbele kuliko hawa ambao wanajikusanya

katika vikundi. Wakati mwengine kujuana tu, kama mimi namjua Mkurugenzi nikishakusanya kikundi changu namwendea nikamwambia bosi sasa naomba unisaidie unipatie nyavu akanipa zile nyavu. Sasa mimi siharibu mazingira kwa sababu sivui, lakini wako watu wanaharibu mazingira na wanavua uvuvi huu ambao unapigwa vita wao hawapewi wala hawajui wapi waende wakaombe ili wapate hizi nyavu. Wao wataendelea kuharibu mazingira sasa sheria hii hawa itawahukumu na itawafunga.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri aone haja ya kushirikiana na watendaji wake kushuka chini zaidi kwenda kuangalia maeneo hayo ya madiko kwa sababu madiko yao wao wanayajua.

Kwa mfano, ukanda wangu wa Tumbe. Kule Tumbe watu wengi wanavua uvuvi huu ambao sasa hivi unaitwa uvuvi haramu. Mimi ikija sheria hii itabidi kwa vyovyote niwatetee, lakini nitawatetea kitu ambacho tumeshakipitisha kwa hiyo wakati mwengine na mimi kitanisuta. Kwa sababu nitaambiwa wewe si umekipitisha si ulikuwemo? Kwa utaratibu wa sasa hivi itabidi lazima ninyanyue mkono kuikubali. Sasa ikija kwamba mtu wangu ameshafanya kosa nitawezaje kumtetea.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya hisani niliyonayo na Mhe. Waziri sitaacha kukaa nisinyanyue mkono, lakini mimi namshauri tu kwa imani aliyonayo na nia ya serikali ya kuwasaidia watu wake katika visiwa hivi, basi bado nia hiyo hiyo ibaki kuwepo. Mimi nadhani washuke chini wafanye utaratibu zaidi wa kuwajua watu walipo na wapi wawasaidie mwanzo.

Kwa sababu katika maisha ya wanadamu wote tunatofautiana katika hali, kuna wengine wanakwenda pwani wanapata samaki, kuna wengine wanakwenda pwani wanakaa siku tatu hawajapata samaki. Lakini akimkuta samaki mchanga kwa sababu siku nyengine hajavua basi itabidi lazima amvue ili apate kijio na watoto wake.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwakilishi utamalizia kesho tukijaaliwa.

Mhe. Ali Moh'd Bakari: *Inshaallah*. Kwa hiyo, siungi mkono mpaka hiyo kesho. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza nakushukuruni sana kwa mashirikiano yenu. Kwa kuwa leo ilikuwa siku yangu ya mwanzo kukalia kiti hiki lakini nimeondoa woga, naona kumbe ninaweza.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 31/03/2010 saa 3.00 asubuhi)